

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 28 Aprili, 2022

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

NAIBU WAZIRI WA MADINI:

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

MHE. EDWARD O. KISAU K. n. y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

MHE. DANIEL B. SILLO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko huo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

SPIKA: Ahsante sana tunaendelea, Katibu!

NDG. BAKARI KISHOMA- KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali tutaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI. Mheshimiwa Francis Isack Mtinga Mbunge wa Iramba Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 108

Vigezo vya Mgawanyo wa Watumishi Wapya

MHE. FRANCIS I. MTINGA aliuliza: -

Je, Serikali inatumia vigezo gani katika mgawanyo wa Watumishi wapya kwenye Halmashauri hususani walimu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Silinde, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

la Mheshimiwa Francis Isack Mtinga Mbunge wa Jimbo la Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiajiri watumishi hususani Walimu kulingana na bajeti iliyotengwa kwa mwaka husika. Baada ya kuajiri walimu hugawanywa kila Halmashauri kwa kuzingatia idadi ya mikondo, kila shule kuwa na Walimu wasiopungua Nane na Uwiano wa Mwanafunzi kwa Mwalimu (*Pupil Teacher Ratio*) kwa shule za Msingi.

Mheshimiwa Spika, kwa shule za sekondari vigezo vinavyotumika kugawa Walimu ni kubainisha idadi ya wanafunzi wanaosoma somo kwa kila kidato, kukokotoa idadi ya mikondo ya madarasa ya wanafunzi kwa kila kidato (mkondo mmoja kuwa na wanafunzi 40 kuanzia Kidato cha Kwanza hadi cha Nne na wanafunzi 35 kwa Kidato cha Tano na Sita. Kubainisha idadi ya vipindi vinavyotakiwa kufundishwa kwa kila somo kwa kuzingatia maelekezo ya mtaala na ukomo wa vipindi anavyofundisha Mwalimu kwa kila somo. Kadirio la juu mwalimu anatakiwa kufundisha vipindi vya dakika 40, thelathini na kadirio la chini visipungue ishirini na nne.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Francis Mtinga swali la nyongeza.

MHE. FRANCIS I. MTINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali katika suala la mgawanyo, napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri katika mgawanyo uliopita wa Walimu ajira zilizopita, Halmashauri yangu ya Mkalama ilipata walimu 12 tu ikilinganisha na Halmashauri zingine ambazo zilipata zaidi ya walimu 40.

Je, unatuambia nini katika mgawanyo huu unaokuja kuhusu Halmashauri yangu ya Mkalama kwani tuna upungufu wa Walimu zaidi ya 800 katika Halmashauri yangu?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis Isack Mtinga Mbunge wa Jimbo la Iramba Mashariki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kuzingatia vigezo vya kupeleka Walimu ambao watapata nafasi hiyo katika Halmashauri zote nchini kulingana na mahitaji. Tunatambua kwamba changamoto bado ni kubwa na mahitaji ya walimu bado ni makubwa lakini kwenye hizi tutaendelea kutenda haki. Kwa hiyo nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaleta kulingana na idadi na mahitaji ya eneo husika. Kwa hiyo, siyo wote 800 lakini ni wale ambao watatosheleza kwa wakati wa sasa. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya Mbunge wa Meatu sasa aulize swali lake.

Na. 109

Ahadi ya Ujenzi wa Daraja Mto Semu – Meatu

MHE. LEAH J. KOMANYA aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya ujenzi wa daraja la juu Mto Semu katika Kijiji cha Mwamanongu Meatu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya Mbunge wa Jimbo la Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa fedha 2005/2006, Serikali kupitia Mfuko wa Barabara ilijenga daraja la chini (*drifting*) lenye urefu wa mita 100 kwa gharama ya Shilingi Milioni 105 ili kurahisisha mawasiliano katika Kijiji cha Mwamanongu.

Mheshimiwa Spika, *TARURA* inaendelea na upembuzi yakinifu (*Geotechnical Investigation*) kwa ajili ya kuanza kazi ya usanifu ili kupata gharama za ujenzi wa daraja la juu katika Mto Semu lililopo katika Kijiji cha Mwamanongu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa usanifu wa Daraja hili, Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa hili daraja.

SPIKA: Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, swali la nyongeza.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ni kweli wiki moja iliyopita tumepokea Milioni 43 kwa ajili ya kuanza kazi zilizoainishwa hapo. Kutokana na umuhimu wa daraja katika mto huo uliosababisha Mheshimiwa Rais Samia Suluhu kuahidi daraja la juu mwaka 2015.

Je, Waziri uko tayari kufika katika Kijiji hicho ukajionea adha inayokata mawasiliano ya Kata Nne na Wilaya?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Maafisa kutoka Wizara ya Ujenzi walifika kukagua hilo daraja pamoja na barabara. Ninataka kujua Je, ni lini Serikali itaipandisha hadhi hilo daraja kuwa *TANROADS* ili tuweze kupata fedha za kutosha kuihudumia barabara hiyo kutokana na umuhimu wa kiuchumi wa Wilaya ya Meatu na Mkoa wa Simiyu kwa ujumla?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya Mbunge wa Meatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, niko tayari nitakwenda katika eneo lake kama alivyoahidi, kwa hiyo nitafika kwenda kujionea hiyo hali halisi anayoizungumza Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapokea maombi yote na tunatambua kwamba kuna maombi mengi sana ambayo Halmashauri na Mikoa kupitia Bodi ya Barabara yameyafikisha kwa ajili ya kupandishwa hadhi. Kwa hiyo, Serikali inaendelea kuyafanyia kazi na mara watakapokuwa wamemaliza kujiridhisha maana yake barabara hizo zitapandishwa hadhi. Kwa hiyo, siyo kwamba Serikali inapuuza ni kwa sababu tunafanya tathmini tunaangalia uwezo wa kifedha ili kazi hiyo inapokamilika maana yake na hizo barabara iweze kutengenezwa kulingana na hiyo hadhi.

SPIKA: Mheshimiwa Joseph Mkundi swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Daraja la Mto Nabili linalounganisha Kata ya Bukindo, Kata Nkilinezi ni muhimu sana kwa mawasiliano ya wananchi wa maeneo haya.

Ni lini Serikali itatupatia pesa kujenga daraja hili?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

la Mheshimiwa Joseph Mkundi Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimwondoe tu hofu kwamba tumepokea hiki kilio chake na tutakifanyia kazi, kwanza tutawatuma watu wetu wakafanye tathmini na kuona fedha kiasi gani zinahitajika kwa ajili ya ujenzi wa daraja hili. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Benaya Kapinga, swali la yongeza.

MHE. BENAYA L. KAPINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Je, ni lini Serikali itatoa fedha za dharura tayari tulishaandika andiko kwa ajili ya barabara ya Kambarage – Maperera – Litoho - Mgumbo pamoja na Mkongotingisa kwenda Muungano, kwa sababu mvua bado zinanyesha na barabara hizi zinataka kutoweka? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benaya Kapinga, Mbunge wa Mbinga Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ambayo ameanisha Mheshimiwa Mbunge ambayo ipo katika mpango wa Serikali ninaamini kabisa kwamba tuko katika hatua za mwisho za kutafuta fedha ili kuhakikisha hiyo barabara inafanyiwa kazi. Kwa hiyo, nimwondoe hofu mara tutakapopata hiyo fedha maana yake tutaanza ujenzi. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu hayo kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mheshimiwa Dokta Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Vunjo, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Profesa Ndakidemi.
Na. 110

Serikali Kuingia kwenye Biashara ya Gesijoto

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI K. n. y. MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuingia kwenye biashara ya Gesi Joto (*Carbon Trading*)?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dokta Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, biashara ya gesijoto ilianzishwa chini ya Mkataba wa Kyoto unaozibana nchi zilizoendelea kutekeleza miradi ya kupunguza uzalishashaji wa gesijoto (*Clean Development Mechanism – CDM*) ili kusaidia nchi zinazoendelea kuleta maendeleo endelevu bila kuchafua mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa Tanzania inaingia na inanufaika na biashara ya hewa ukaa, Ofisi ya Makamu wa Rais iliandaa Mwongozo wa Taifa wa Biashara ya Hewa Ukaa kwa mwaka 2016. Tanzania inayo miradi mitatu ya biashara ya gesijoto inayotekelezwa nchini. Hadi sasa jumla ya tani 900,000 za gesijoto zimeshauzwa kupitia miradi ya uzingatiaji wa kupunguza gesijoto inayotekelezwa nchini.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, aidha, miradi minne ya biashara ya soko hiari ya gesijoto imeelekezwa nchini tangu mwaka 2009 na jumla ya tani 1,456,600 za gesijoto zimepunguzwa na kuuzwa kupitia utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais inafanya mapitio Mwongozo wa Taifa wa Biashara ya Hewa ya Ukaa ili kuwezesha taifa na wananchi wake kushiriki kikamilifu na kunufaika na biashara hii. Aidha, katika kuboresha ushiriki, Wizara ya Maliasili na Utalii inaandaa mwongozo maalum wa usimamizi wa misitu ambayo itashiriki biashara ya gesijoto nchini. Ninakushukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Profesa Ndakidemi swali la nyongeza.

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana na ninamshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, biashara hii huwa inahusisha upandaji na utunzaji wa miti. Je, Serikali haioni umuhimu wa kusukuma hii biashara iende katika maeneo ya Kilimanjaro inayopakana na Mlima Kilimanjaro ili kwanza tutunze ule msitu ili Mlima usiharibike na wananchi wa Kilimanjaro wajipatie kipato?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nikiri na niseme kwamba ipo haja ya mradi huu kwenda Kilimanjaro kwa lengo na madhumuni ya kuhifadhi na kutunza mazingira.

Mheshimiwa Spika, pia kuna haja ya mradi huu kupelekwa Kilimanjaro na tutakwenda kuhakikisha

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

tunapeleka ili lengo na madhumuni wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro na vijiji vilivyomo ndani ya Mkoa huo waweze kunufaika, kwa sababu mradi huu si kwamba tu unanufaisha Serikali Kuu lakini hata vijiji vidogo vidogo vinanufaika kupitia mradi huu, kwa sababu kuna asilimia maalum huwa inapangwa kwenye mradi huu.

Mheshimiwa Spika, tayari tumesha-*practice* katika Mkoa wa Katavi, Manyara na Mikoa mingine. Tumeona tayari zipo shule, yapo maji safi, zipo zahanati zilizojengwa kutokana na asilimia ya mradi huu. Ninakushukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Lazoro Justin Nyamoga swali la nyongeza.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Kilolo yupo mwekezaji anaitwa Udzungwa *Corridor* na tayari anapanda mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya biashara hiyo. Kwenye vivijiji vinavyozunguka kuna misitu mingi ya asili inayofanana na hiyo hiyo inayopandwa.

Je, Serikali sasa ina mpango gani wa kuhakikisha ile misitu ambayo wanavijiji wameitunza na yenyewe inaingia kwenye huo mfumo wa biashara badala ya kutegemea tu ile ambayo Mwekezaji anawekeza na anapanda miti ile ile? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lazoro Nyamonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza katika kitu ambacho tunakithamini sana ni upandaji wa miti. Pili tunashughulika

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

na suala zima la kuishughulikia miti. Kwa hiyo, kikubwa nimwambie misitu yote ya asili kama ambavyo nimeeleza katika jibu la msingi kwamba sasa hivi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii, tumeshaandaa muongozo wa usimamizi wa misitu yote ili lengo na madhumuni tuingize kwenye mpango huo pia tuweze kunufaisha vijiji vilivyozunguka na pia tunufaishe Serikali, pia tutunze na tuhifadhi mazingira. Ninakushukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Cecilia Paresso swali la nyongeza, haya ahsante sana. Mheshimiwa Asya swali la nyongeza.

MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kama tunavyotambua huu mradi wa uvunaji wa hewa ya ukaa ni muhimu sana kwa Taifa letu, inasaidia kupunguza masuala mengi ambayo yanasababishwa na uchafuzi wa kimazingira.

Mheshimiwa Spika, swali langu, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia akinamama ambao wamejitolea kwa makusudi kupanda miti ya mikoko Zanzibar katika Vijiji vya Bwimbwini, Bweleo na maeneo mengine na hawa wanawake wanapata changamoto mbalimbali kuhusu kupata miti na mambo mengine ili ile miti kuweza kustawi vizuri. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia akinamama hawa? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, asante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asya, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Kaskazini Unguja kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii nimpongeze sana Mheshimiwa Asya amekuwa mmoja wa miongoni mwa vinara ambao wanapambana na suala zima la uhifadhi wa mazingira katika Mkoa wa Kaskazini. Kikubwa tuna mikakati mingi ya kuhakikisha kwamba tunawasaidia akinamama kwa sababu tumegundua kwamba ni moja ya miongoni mwa vinara wazuri wa uhifadhi wa mazingira na kupambana dhidi ya mabadiliko ya tabia ya nchi.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, kuwapa elimu kwa sababu tumegundua kwamba akinamama wengi wana juhudi, wana jitihada na wana hamu ya kuhifadhi mazingira, lakini tumegundua utaalum kidogo umepungua, kwa hiyo tunawapa taaluma.

Mheshimiwa Spika, la pili, tumefikiria pia kuona namna ya kuwasaidia kuweza kupata mitaji ili lengo na madhumuni yaweze kufanya hizo kazi zao za uhifadhi wa mazingira vizuri. Nakushukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Ulyankulu sasa aulize swali lake.

Na. 111

Kuwapa Uraia Wananchi Zaidi ya 6,000 kutoka Burundi waliopo Ulyankulu

MHE. REHEMA J. MIGILLA aliuliza:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Je, ni lini Serikali itawapatia uraia wananchi 6000 kutoka Burundi waliokamilisha mchakato wa maombi ya uraia katika Jimbo la Ulyankulu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-
Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Ulyankulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wananchi wapato 6,000 kutoka Burundi wamekamilisha mchakato wa maombi ya uraia katika Jimbo la Ulyankulu. Wananchi hao walikuwa watoto wa wakimbizi wa Burundi wapatao 162,156 waliopewa uraia mwaka 2009/2010. Wananchi hao pamoja na watoto wapatao 6,620 waliozaliwa baada ya wazazi wao kuwasilisha maombi ya uraia, waliwasilisha maombi ya uraia Serikalini.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi wananchi hao walikamilisha kujaza ipasavyo fomu za maombi ya uraia na kuziwasilisha Serikalini. Maombi yao yalifanyiwa kazi na kwa sasa yapo katika hatua za maamuzi. Mara maamuzi yatakapofanyika, wananchi hao 6,620 watajulishwa hatma ya maombi yao.

SPIKA: Mheshimiwa Rehema Migilla swali la nyongeza.

MHE. REHEMA J. MIGILLA: Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kuishukuru Serikali kwa kukubali maombi ya hawa raia wangu, lakini swali langu lilitaka ni lini huu mchakato utakamilika na kwenye majibu hawajaonesha. Sambamba na hilo nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza; Jimbo langu la Ulyankulu katika hizo Kata tatu asilimia 99 ya mwananchi hao kwa sasa ni raia wa Tanzania. Ikijumlisha

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

raia tajinisi na raia wazawa kabisa wa Tanzania lakini wananchi hawa wanaishi chini ya Sheria Na.9 ya wakimbizi ambayo sheria hii sasa inazuia kufanya shughuli zozote za maendeleo ikiwa sambamba na uwekezaji na kufanya shughuli nzuri za kuleta maendeleo kwa wananchi wetu. Sasa je, kwa sasa Serikali haioni kuna kila sababu ya kufuta hii Sheria Na.9 ambayo inazuia maendeleo na uwekezaji kwa wananchi wetu wakati huo Serikali inakwenda kujipanga kwenye zoezi zima la sensa ili kupanga shughuli za kimaendeleo? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, Waziri amesema kwamba hawa raia 6,620 ni watoto wa raia wa Tanzania, yaani wazazi wao kwa sasa ni raia wa Tanzania halafu watoto ni wakimbizi. Sasa je, kwa sababu mchakato hauieleweki utakamilika lini, kwa nini sasa hatuoni haja ya UNHCR kuwahudumia hawa wananchi kwa kuwapatia *package* inayowapatia wakimbizi kwenye makambi mengine ya wakimbizi? (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Migilla, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza, kuhusu umuhimu wa kufuta Sheria Na.9 ili waruhusiwe kufanya vitu vya maendeleo kwenye makazi yale nadhani Mheshimiwa asubiri tutakapokamilisha kuwapatia uraia wote *then* hatua za marekebisho ya sheria husika zitafuata. Lakini kama tunakiri kwamba bado watu wengine hawajapewa uraia itakuwa ngumu sana hilo kulitekeleza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, watoto hawa wapate *package* kutoka UNHCR, hilo tutalizungumza, lakini nadhani Mheshimiwa Mbunge jambo la msingi ilikuwa kuharakisha wapate uraia wao ili wa-*enjoy* haki nyingine kama raia kuliko hilo la *package* lakini maadam Mheshimiwa Mbunge ameliuliza hapa, tutafanya mawasiliano na wenzetu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wa *UNHCR* kuona uwezekano wa kuzingatia hili ombi lake. Nashukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Agneta Lambert swali la nyongeza.

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Uraia pacha imekuwa ni kilio cha Watanzania walio wengi. Nini kauli ya Serikali rasmi kuhusiana na jambo hili? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, unao uhuru wa kujibu hilo swali kwa sababu ni mahsusni ama lijibiwe kama swali la msingi? Unao uhuru.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba nimwombe Mheshimiwa Lambert swali hili ni mahsusni, liwasilishwe ili lifanyiwe utafiti hatimaye liweze kujibiwa ipasavyo hapa Bungeni. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi tunakushukuru kwa majibu hayo kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Waziri, naona kuna swali lako lingine. Mheshimiwa Mohammed Jumah Soud, Mbunge wa Donge sasa aulize swali lake.

Na. 112

Vigezo vinavyotumika kuanzisha Vituo vya Polisi

MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH aliuliza:-

Je, Serikali inatumia vigezo gani kuanzisha vituo vya polisi katika maeneo ambayo idadi ya watu na vitendo vya uhalifu vinaongezeka?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu kwa swali hilo.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Jumah Soud, Mbunge wa Donge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vigezo vinavyotumika kuanzisha vituo vya polisi ni ongezeko la watu, ongezeko la matukio ya uhalifu, umbali kati ya kituo kimoja cha polisi na kingine, uwepo wa miundombinu ya Serikali, shughuli za kibiashara pamoja na maeneo ya kimkakati kwa ajili ya ulinzi na usalama wa nchi, likini pia uwezo wa kibajeti na utayari wa wananchi na mamlaka zao za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, nia ya uanzishwaji wa kituo cha polisi huwasilishwa kwenye Kamati ya Usalama ya Wilaya. Kikao kikiridhia, hoja hupelekwa kwenye Kamati ya Usalama ya Mkoa, kisha ushauri wao huwasilishwa kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi kwa ajili ya utekelezaji ikiwa ni pamoja na mipango ya ujenzi, kupeleka Askari na vitendea kazi. Nashukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Mohammed Jumah Soud swali la nyongeza.

MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa wananchi wa Jimbo la Donge wanatembea masafa marefu kufuata huduma za kipolisi katika Vituo vya Polisi vya Mkokotoni na Kituo cha Polisi cha Mahonda na kwa kuwa uhalifu na halikadhalika idadi ya watu wameongezeka katika maeneo mbalimbali ya Jimbo la Donge. Je, Serikali haioni haja ya kufanya kazi na wananchi wa Jimbo la Donge kuweza kujenga kituo katika maeneo hayo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Kituo cha Polisi cha Mahonda ni kituo kikongwe toka kipindi cha ukoloni na kituo hiki hakijafanyiwa ukarabati mkubwa kwa kipindi kirefu. Je, Serikali ina mpango gani wa kukifanyia

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

marekebisho makubwa Kituo cha Polisi cha Mahonda pamoja na nyumba za wafanyakazi ili kuweza kukidhi kupambana na masuala ya uhalifu ambayo yanaongezeka siku hadi siku? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Soud, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu umuhimu wa kujenga Kituo cha Polisi eneo la Donge ambalo ametaja vigezo vitatu vya masafa marefu lakini kuwepo kwa uhalifu, kujenga kituo pale tutawasiliana na Kamisheni ya Polisi Zanzibar wafanye utafiti kuona umuhimu wa kujenga pale ili iweze kuingizwa kwenye bajeti hatimaye ujenzi uweze kufanyika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili la kuchakaa kwa Kituo cha Polisi Mahonda, namwomba Mheshimiwa Mbunge, tutaituma Polisi Kamisheni Zanzibar kwa kauli yangu niombe Polisi Zanzibar wafanye uthamini wa Kituo cha Polisi Mahonda kwa madhumuni ya kubaini mahitaji ili tuweze kuingiza kwenye mpango wa ukarabati. Nashukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Kunti Majala, swali la nyongeza.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kata ya Soya, Wilaya ya Chemba ni kati ya Kata ambayo inahudumia wafanyabiashara wa mazao pamoja na wafanyabiashara wa mifugo, lakini Kata hii haina kituo cha polisi pamoja na kwamba kutokuwepo kwa kituo cha polisi michakato aliyoisema Naibu Waziri hapo tulishaikamilisha. Je, ni lini sasa Serikali itapeleka kituo cha afya, samahani, Kituo cha Polisi kwenye Kata ya Soya ili kukidhi mahitaji na matakwa ya usalama wa Jeshi la Polisi ya kulinda raia na mali zao? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Spika, nashukuru maana mwanzoni afya ilinichanganya kidogo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kunti Majala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ikiwa kuna mahitaji makubwa ya kujenga Kituo cha Polisi Kata ya Soya, nishauri mamlaka za utawala, kwa maana ya Serikali ya Mtaa Chemba lakini na uongozi wa Wilaya kupitia Kamati yao ya Usalama wajenge hoja hii kama nilivyoeleza, wanyambue mahitaji yao ili wawasilishe kwa *IGP*, then taratibu ya kuingiza kituo hiki katika mpango wa ujenzi iweze kufikiwa. Hata hivyo, kama tulivyokwisha sema kwenye majibu ya maswali yaliyotangulia, tunahamasisha ushiriki wa Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na wananchi waanze ujenzi ili Serikali isaidie kukamilisha vituo hivi wakiwa na haja ya kuwa na kituo cha polisi. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaelekea Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 113

Ucheleweshaji wa Viuatilifu vya Zao la Korosho

MHE. MAIMUNA S. MTANDA aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje katika kuondoa changamoto ya ucheleweshwaji wa viuatilifu kwa wakulima wa zao la korosho?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe, majibu.

WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa huko nyuma kumekuwa na ucheleweshwaji wa viuatilifu. Katika kuondoa changamoto ya ucheleweshwaji wa pembejeo unaosababishwa na mlolongo mrefu wa manunuzi kutoka kwa mzalishaji hadi kumfikia mkulima, Serikali inasimamia uagizaji wa pembejeo kwa kupitia Kamati ya Pamoja ya Pembejeo inayoundwa na Vyama vya Ushirika ambavyo kimsingi ni wakulima wenyewe. Kutokana na utaratibu huo, jukumu la Serikali ni kufuatilia mchakato huo ili manunuzi yafanyike kwa muda muafaka na pembejeo kuwafikia wakulima kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2022/2023 Vyama Vikuu vimeagiza *sulphur* ya unga tani 25,000, viuatilifu vya maji lita milioni 1.5 pamoja na mabomba ya kupuliza 35,000 kwa ajili ya msimu wa 2022/2023 na hadi kufikia Aprili moja jumla ya tani 1,600 na lita 730,724 tayari zimeshapokelewa na kiasi kilichobaki kinatarajiwa kupokelewa kufikia mwisho wa mwezi Mei.

SPIKA: Mheshimiwa Maimuna Mtanda, swali la nyongeza.

MHE. MAIMUNA S. MTANDA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini Serikali ilituhakikishia kwamba kwa msimu wa 2022/2023 pembejeo zitafika kwa wakati kwa sababu upulizaji baadhi ya maeneo huanza mwezi Mei. Kwa takwimu ambazo Mheshimiwa Waziri amezitoa, ukiangalia *sulphur* imefika tani 1,600, bado tani 23,400 lakini viuatilifu vya maji hadi sasa vimefika lita 730,724 bado lita 770,000. Je, Serikali imejipangaje ili kutokurudi kule ambako mwaka jana tulipata changamoto sana ya upatikanaji wa mapema wa pembejeo hizi?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kwamba, Taasisi ya TPRA ime-*test* baadhi ya pembejeo ambazo zimefika na kukuta kuna changamoto ya baadhi ya kutokidhi vigezo na kwamba pembejeo hizo zirudishwe zilikutoka. Je, Serikali inatuambiaje hizo pembejeo hazitarudi kwa mlango mwingine kwenda kwa wakulima? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Kilimo majibu.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maimuna, Mbunge wa Newala Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu viuatilifu ambavyo vimekuwa na mashaka kwanza nilihakikishie Bunge lako siyo viuatilifu vya msimu wa 2022/2023, bali ni viuatilifu ambavyo vilikuwa *procured* kwa ajili ya msimu wa 2021/2022 na sasa hivi kama Serikali tulichokifanya, viuatilifu vyote ambavyo vilikuwa vina mashaka juu ya ubora vinakusanywa na kuhifadhiwa katika ghala moja katika Mkoa wa Mtwara chini ya usimamizi wa Serikali. Kwa hiyo nataka nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba viuatilifu hivi havitarudi kwa mlango wa nyuma kwenda kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, kuhusu viuatilifu ambavyo vimeshafika ni ukweli kwamba mwaka jana tulikuwa na tatizo na mwaka jana tenda ilitangazwa mwezi Aprili lakini msimu huu tenda tulizitangaza toka mwezi Januari na mpaka sasa mahitaji ya viuatilifu asilimia 50 ya mahitaji ya viuatilifu vya maji tayari viko Mkoa wa Mtwara na hivi vingine tunatarajia vitafika *late* tarehe 30 Mei na vitashushwa katika Bandari ya Mtwara.

Kwa hiyo, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na niwahakikishie wakulima wa korosho, wote watapata viuatilifu vilivyokuwa *allocated* kwa wakati bila shaka. Pia mwaka huu tumeongeza idadi ya viuatilifu vya maji ili kumpa mkulima matumizi ya viuatilifu vya maji zaidi kuliko matumizi ya *sulphur* ambayo kwa utafiti wa *TARI* Naliendele matumizi ya viuatilifu vya maji ni bora zaidi kuliko *sulphur* na ndomana mwaka huu tumetoa idadi kubwa ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

viuatilifu vya maji. Kwa hiyo nataka nimhakikishie Mbunge na wakulima wa korosho kwamba hatutakuwa na matatizo tuliyo *experience* mwaka jana.

SPIKA: Mheshimiwa Yustina Rahhi, swali la nyongeza kwa kifupi.

MHE. YUSTINA A. RAHHI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa pembejeo za kilimo wakati wa msimu wa kilimo hususan mbolea. Sasa tunapoelekea msimu wa kilimo, Serikali imejipangaje kupambana na changamoto hiyo? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, majibu kwa kifupi.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, changamoto ya msimu uliopita ya upatikanaji siyo suala la *availability*, tatizo kubwa lilikuwa ni gharama. Mbolea ilikuwepo ndani ya nchi lakini uwezo wa wananchi kununua ulikuwa ndiyo tatizo kubwa. Nataka tu nimwambie Mheshimiwa Mbunge, maelekezo ya Mheshimiwa Rais yako wazi, msimu wa kilimo unaokuja wa 2022/2023, Serikali sasa hivi tuko kwenye majadiliano ndani ya Serikali ili kuona njia ambayo itapunguza bei ya gharama ya mbolea kwa wakulima ili wakulima waweze kuinunua mbolea na waweze kuitumia kwa wakati.

SPIKA: Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Wakulima wengi ambao wanatumia hivi viuatilifu wanahatari kubwa ya kupata magonjwa yasiyoambukiza ikiwemo kansa, mtindio wa ubongo na mengine kutokana na kutokutumia ipasavyo viuatilifu hivi. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha inawalinda wakulima kiasya katika matumizi haya ya viuatilifu? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, majibu.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Paresso kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli viuatilifu vikitumika vibaya vinakuwa na madhara kama jambo lolote lile, hata chakula watu wakila vibaya kunakuwa na madhara.

Kwa hiyo tunachokifanya kama Serikali ni kwamba tunatoa mafundisho kupitia *Tanzania Plant Health Authority* iliyokuwa *TPRI* huko zamani na baadhi ya mazao sasa hivi tumeanza utaratibu wa ku-*train* vikundi vya vijana ambavyo vinapewa mafunzo maalum na *TPRI* na kupewa leseni kwa ajili ya kufanya kazi za kupulizia viuatilifu.

Mheshimiwa Spika, vile vile tumeanza kuwataka wasambazaji wa viuatilifu wanapotengeneza vifungashio watumie lugha ya Kiswahili kutoa maelezo ambayo namna ya mkulima kuchanganya ili iwe rahisi mkulima anaponunua kile kiuatilifu kuweza kufanya kazi ile yeye mwenyewe na kupata mwongozo badala ya kutumia lugha ya Kiingereza ambapo inakuwa ni vigumu kuongoza. Kwa hiyo huo ndiyo utaratibu tumeanza na viuatilifu vyote kuanza sasa vinavyosajiliwa *TPRI* hata vilivyokwisha sajiliwa na nipitie Bunge lako hili kumwagiza Mkurugenzi Mkuu wa *Tanzania Plant Health Authority* atekeleze maagizo ya Serikali kwamba viuatilifu vyote vifungashio viandikwe kwa lugha kwa Kiswahili ili mkulima aweze kusoma na kuelewa. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Anastazia Wambura, swali la nyongeza.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kumekuwa na tatizo la wakulima kugaiwa kiasi kidogo sana cha viuatilifu ukilinganisha na kile kiasi ambacho kimefika katika maeneo husika.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba wakulima wanapata kile kiasi ambacho wanastahili?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, majibu kwa kifupi.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, hivi tunavyoongea sasa hivi tumeiagiza Bodi yetu ya Korosho, lakini vilevile kwa ajili ya kuweza kupata *the light data base* ya wakulima na ukubwa wa mashamba yao, tunashirikiana na Halmashauri za Wilaya na Serikali za Mkoa kupitia vyama vyao vya ushirika. Cha kwanza, tunachukua takwimu za uuzaji kupitia vyama vya ushirika ili kumjua mkulima na idadi ya uzalishaji wake.

Mheshimiwa Spika, cha pili, kuanzia msimu wa mwaka 2022/2023 Serikali itatenga fedha kwenye bajeti yetu ya kuzipatia Sekretarieti za Mikoa pamoja na Vyama Vikuu vya Ushirika ili zoezi la usajili wa mashamba ya wakulima na utambuzi wa wakulima liweze kufanyika vizuri ili kujua mahitaji halisi ya pembejeo ambazo wakulima wataigawa.

Kwa hiyo, kuna uwezekano kukaendelea kuwepo kwa changamoto kwa muda, lakini ni jambo ambalo tunalolifanyia kazi. Naamini kwamba ndani ya kipindi cha mwaka mmoja au miwili zoezi la usajili wa utambuzi wa wakulima litakuwa limekamilika na tutaondokana na hili tatizo.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri ahsante kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini sasa aulize swali lake.

Na. 114

Ujenzi wa Kiwanda cha Mbolea Kilwa Masoko

MHE. ALLY M. KASSINGE aliuliza:-

Je, mazungumzo ya Serikali na wawekezaji kujenga Kiwanda cha Mbolea Kilwa Masoko kwa kutumia gesi asilia yamefikia wapi?

SPIKA: Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Kigahe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa viwanda vya mbolea na namna uzalishaji wa mbolea nchini utakavyoongeza tija kwa wakulima na hatimaye kupata mavuno mengi na viwanda kupata malighafi za kutosha kwa ajili ya kuchakata. Serikali inaendelea na majadiliano na wawekezaji mbalimbali wakiwemo Kampuni ya Dangote, Elsewedy na PolyServe ili kuharakisha uwekezaji wa Kiwanda cha Mbolea Kilwa Masoko.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

MHE. ALLY M. KASSINGE: Mheshimiwa Spika, ahsante na naipongeza Serikali kwa majadiliano yanayoendelea kati yake na wawekezaji, japo nasikitika kwamba ni karibu mwaka sasa tangu mazungumzo hayo yameanza. Kwa hiyo, kwa umuhimu wa mahitaji ya mbolea nchini, naomba basi mchakato huu ufanyike kwa haraka ili tutatue tatizo kubwa la wakulima ambao wanakosa pembejeo za mbolea msimu mpaka msimu.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mheshimiwa Waziri mwaka 2021 kupitia Bunge hili aliahidi kuja Kilwa ili kuona

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mchakato wa uanzishwaji wa kiwanda hiki, lakini nadhani kutokana na majukumu alishindwa kupata nafasi hiyo. Sasa je, yupo tayari baada au ndani ya Bunge hili wakati mchakato wa majadiliano unaendelea, kufuatana nami kwenda Kilwa Masoko ili kuona maendeleo ya maandalizi ya kiwanda cha mbolea?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara naona yote ni maombi, siyo maswali.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIAHARA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naamini Serikali yetu ni sikivu chini ya Rais wetu Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, tutaharakisha majadiliano haya ili tuweze kufanikisha uwekezaji huu muhimu mapema.

Mheshimiwa Spika, nikijibu swali la pili, naomba nimwahidi, kwa kweli tangu mwaka 2021 hatujapata nafasi, lakini naamini mwaka huu nitakwenda. Nakushukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Tunza Malapo, swali la nyongeza.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwa Kiwanda cha Mbolea Kilwa, ni sawa kabisa na ilivyo na uhitaji wa Kiwanda cha Mbolea Mtwara, hususan Jimbo la Mtwara Mjini kwa sababu malighafi ipo. Sasa tu nataka kujua, ni lini Serikali itajenga kiwanda hicho kwa sababu kitaongeza ajira na wakati huo huo itawezesha nchi kupata mbolea kwa ajili ya kilimo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIAHARA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Uwekezaji Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tunza Malapo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi, Serikali ina nia njema kuhakikisha tunavutia wawekezaji wengi kuwekeza katika viwanda vingi ikiwemo viwanda vya mbolea.

Mheshimiwa Spika, pia hili la Mtwara nalo tunalichukulia kwa umuhimu wake kwamba tutaendelea kutafuta wawekezaji zaidi ili weweze kuwekeza Mtwara na maeneo mengine ambayo yana malighafi kwa ajili ya kuzalisha mbolea. Nakushukuru.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Nyasa, sasa aulize swali lake.

Na. 115

Kukamilisha Ujenzi wa SIDO – Nyasa

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha SIDO Wilayani Nyasa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Nyasa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2022/2023 Wizara kupitia shirika la kuendeleza viwanda vidogo (*SIDO*) imetenga jumla ya shilingi milioni 950 kwa ajili ya kuboresha

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

miundombinu ya mitaa ya viwanda. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi milioni 100 ni kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Mafunzo na Uzalishaji cha *SIDO* Wilayani Nyasa. Hivyo, pindi fedha hizo zitakapopokelewa, ujenzi wa kituo hicho utakamilika. Nakushukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, swali la nyongeza.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nashukuru kwa majibu yenye matumaini kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Maswali yangu mawili ya nyongeza ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni mtindo kabisa wa Wizara hii kuanzisha majengo na kutokumaliza kwa wakati kwa sababu ya kutokupata mgao unaotakiwa kutoka Serikali Kuu, kwa maana ya Wizara ya Fedha: Je, kwa mwaka huu wa 2022, hiyo shilingi milioni 100 iliyoahidiwa ni kweli itatolewa? Naomba *commitment* ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili ni kwamba, Wilaya ya Nyasa haina kabisa chuo chochote kinachotoa mafunzo kwa sasa hivi ikiwemo haya ya ujasiliaamali: Je, *SIDO* kwa kuwa jengo bado halijakamilika, mtaweza kwenda kutoa mafunzo hayo angalau kila mwezi mara moja wakati tukiendelea na huo ujenzi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara majibu.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIAHARA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Stella Martini Manyanya, Mbunge wa Nyasa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa fedha kwa maana ya kukamilisha vituo vingi vya mafunzo na uzalishaji ambavyo vimeanzishwa katika wilaya na mikoa mbalimbali. Ni nia ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Serikali na sasa tunaamini tutapata hizo fedha ili kukamilisha kituo hiki na vingine ambavyo bado havijakamilika.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, nachukuwa maombi ya Mheshimiwa *Eng. Stella Manyanya* kwamba tuanze sasa kuona namna ya kuanza kutoa mafunzo ya uzalishaji katika maeneo ambapo kuna wajasiliamali wengi ikiwemo katika Jimbo hili la Nyasa ambapo wajasiliamali hawa watapata mafunzo kupitia *SIDO*.

Mheshimiwa Spika, nawaagiza *SIDO* waanze sasa kupitia utaratibu ambao siyo rasmi, badala ya kusubiria majengo, waanze kutumia majengo ambayo Halmashauri zinaweza zikatupa kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa wazalishaji katika maeneo yote ikiwemo katika Jimbo la Nyasa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo, kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Kishapu, sasa aulize swali lake.

Na. 116

Hitaji la Maji Kutoka Ziwa Victoria – Kishapu

MHE. BONIPHACE N. BUTONDO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka maji ya Ziwa Victoria kwenye Kata 24 zilizopo katika Tarafa tatu Wilayani Kishapu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa maji, Mheshimiwa Mahundi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Nyangindu Butondo, Mbunge wa Jimbo la Kishapu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jukumu la Serikali ni kuhakikisha wananchi katika maeneo ya Mijini na Vijijini wanapata huduma ya uhakika ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, kazi itaendelea kuhakikisha Kata 24 za Wilaya ya Kishapu zinapata huduma ya maji safi na salama na kufikia lengo la asilimia 85 ifikapo mwaka 2025.

SPIKA: Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

MHE. BONIPHACE N. BUTONDO: Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mafupi na mazuri. Pia naipongeza sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo inashughulika na changamoto kubwa ya maji na wananchi wa Jimbo la Kishapu kwa ujumla. Tangu mwezi wa pili tarehe 11 mkataba baina ya *Emirates Builders* wenye thamani ya Shilingi bilioni 6.5 umesainiwa kwa ajili ya usambazaji wa maji ya Ziwa Victoria katika Kata nne; Kata ya Laghana, Mwamashare, Igaga, na Ngofila.

Swali: Je, Serikali iko tayari kuhakikisha kwamba inatoa ile 20% kama *advance payment* ili mradi huu uanze kutekelezwa kwa wakati kwa maana Mkandarasi mpaka sasa yuko *site*?

SPIKA: Uliza swali la pili Mheshimiwa.

MHE. BONIPHACE N. BUTONDO: Mheshimiwa Spika, swali la pili. Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuambatana nami kwenda Jimboni kuona changamoto zilizoko katika Jimbo la Kishapu na kuhakikisha kwamba atasukuma kazi hii kwa haraka ili mradi maji yaanze kutoka katika Jimbo la Kishapu?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.
(*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Butondo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *advance payment* tayari zimeanza kutolewa kwa Wakandarasi wote, naamini *Emirates* naye atakuwa katika *list*. Suala la kuambatana naye ni moja ya majukumu yangu, hakuna shaka. Nitafika kuhakikisha mradi unatekelezwa. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, swali la nyongeza.

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria unaotoka Mangu kwenda Ilogi ni mradi uliochukuwa muda mrefu sana kutoka 2016. Mwaka 2021 niliua swali la msingi juu ya mradi huo wa maji. Waziri akaniambia Juni mwaka 2021 mradi ule ungezinduliwa. Sasa ni lini Serikali itazindua mradi wa maji unaotoka Mangu mpaka Ilogi. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Iddi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, miradi hii ya Ziwa Victoria tunaendelea kuitekeleza. Ipo katika hatua mbalimbali kwa kila eneo, lakini maji ya Ziwa Victoria yataendelea kutumika vizuri, kuhakikisha huduma ya maji safi na salama itapatikana.

Mheshimiwa Spika, ni hivi karibuni uendelezaji na utekelezaji wa mradi huu unaendelea kufanyiwa kazi.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Jafari Chege, swali la nyongeza.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Moja ya vijiji vilivyoathirika na machafuko ya Mto Mara ni pamoja na Kijiji cha Kwiguse, Marasibola na Kyamwame na Serikali iliahidi kupeleka maji mbadala kwenye vijiji hivi ambavyo havitumii maji haya kwa sasa. Nataka nijue Serikali imefikia wapi kwenye mpango huu wa kuhakikisha wale wananchi wanapata maji safi na salama?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, hilo swali pia ni mahususi. Kama unayo majibu, ujibu; kama huna hayo majibu ya kupeleka maji mbadala kwenye hicho Kijiji, kwa sababu ni suala linalohusu jambo mahususi lililotokea, unao uhuru wa kumwomba Mbunge alete swali la msingi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nimepokea, tutawasiliana na Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, swali la nyongeza.

MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO: Mheshimiwa Spika, nilitaka kujua Serikali ina mpango gani wa kulipatia Jimbo la Mbagala maji safi na salama yene uhakika?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maeneo hayo ya Mheshimiwa Mbunge tayari kuna miradi inayoendelea, ipo kwenye utekelezaji hatua za mwisho. Hivi punde maji safi na salama yataunganishwa katika *existing lines* ili wingi wa maji uweze kuongezeka kwa wananchi. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Felista Njau, swali la nyongeza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. FELISTA D. NJAU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Katika Jimbo la Kawe Kata ya Wazo, mitaa ya Nyakasangwe, Mivumoni na Salala, miundombinu ya maji kwa maana matenki tayari imeshajengwa. Ni lini sasa Serikali itahakikisha maji yanatoka katika mitaa hiyo ili kuwaletea wananchi wale nafuu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Felista Njau, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maeneo yote ya Kawe miradi iko mwishoni. Hata jana tu nimemwona Mkuu wa Mkoa akiwa na watendaji wetu wa DAWASA wakifuatilia kule, hivyo miradi iko mwishoni. Muda siyo mrefu maji ya kutosha safi na salama yataanza kutoka.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo, swali la nyongeza.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Wilaya ya Muleba iko kando kando mwa ya Ziwa Victoria, na tuna mradi wa kuvuta maji kwa ajili ya Kata sita za Wilaya ya Muleba; usanifu umekamilika.

Je, ni lini sasa Serikali itatekeleza huo mradi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali Mheshimiwa Mbunge wa Muleba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mara usanifu wa mradi unapokamilika, tunatarajia tuwe na kipindi kifupi cha mwezi mmoja au miwili kuona sasa tunatumia maandiko ya Mhandisi Mshauri ili mradi uanze kutekelezeka. Hivyo, kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

sababu usanifu umekamilika, tupo katika utaratibu wa kuona sasa tunapata mkandarasi aje kutekeleza huu mradi.

SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda.

Na. 117

Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria – Bunda

MHE. BONIPHACE M. GETERE aliuliza:-

Je, mpango wa kupeleka maji ya Ziwa Victoria kutoka Bunda Mjini kwenda Vijiji 33 vya Tarafa ya Chamriho umefikia hatua gani?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniface Mwita Getere, Mbunge wa Jimbo la Bunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha huduma ya maji katika Tarafa ya Chamriho ambapo katika mwaka wa fedha 2021/2022 inatekeleza ujenzi wa miradi mipya mitatu ya Kirolerl - Kambubu, Mariwanda na Sanzate pamoja na ukarabati wa mradi wa maji wa Nyang'aranga ambayo itatoa huduma ya maji kwa wananchi wapatao 12,648.

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kuhakikisha Wananchi wa tarafa ya Chamriho wanapata huduma ya maji safi na salama na yenye kutosheleza. Katika kutimiza lengo hilo, taratibu za kumwajiri Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kufanya usanifu wa mradi wa maji wa kutoka Ziwa Victoria zinaendelea. Matarajio ni kuanza ujenzi wa mradi katika robo ya pili ya mwaka wa fedha 2022/2023.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, swali la nyongeza.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, nawapongeza Wizara ya Maji, wanafanya kazi vizuri sana; na waendeleo kufanya hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Kwa kuwa huu mradi wa maji wa Ziwa Victoria kutoka Bunda Mjini kwenda Bunda Vijijini ni wa muda mrefu sana na una baraka zote za Waziri wa kwanza na Waziri aliyepo sasa hivi Mama Samia Suluhu Hassan, sasa Wizara ipo tayari kuweka mchakato wa *single source* ili kumpata mkandarasi wa haraka zaidi wa kutekeleza mradi huu?

Mheshimiwa Spika swali la pili; kwa kuwa tuna miradi kichechefe katika vijiji vya Kata ya Nyamswa; vijiji vya Makongoro A, Makongoro B, na Bukama na Vijiji vya Mgeta na Nyang'aranga; sasa ni lini Waziri atafika eneo hilo kusikiliza kero za wananchi kwenye miradi mibovu ya siku nyingi?

SPIKA: Haya, ahsante sana. Kwenye swali lako la kwanza Mheshimiwa Getere umesema Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, ndiye Waziri aliyepo? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Waziri wa Maji ni Mheshimiwa Aweso. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili Mheshimiwa Gitere kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kupokea pongezi zake. Niseme, tuendeleo kushirikiana. Lengo ni kuona

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

tunafikisha maji safi na salama kwa wananchi na kuwatua akina mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bunda Mjini kuelekea vijijini kutumia *single sources*; nimepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kwa sababu lazima tuajiri mhandisi mshauri ili aweze kutufanyia upembuzi yakinifu na kutuandalia maandalio ya kazi. Baada ya kumpata Mheshimiwa Mbunge wazo lako tutalifanyia kazi kwa kulipa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi chefuchefu, ni lengo la Wizara kuimaliza miradi chefuchefu yote, hivyo kufika kwenye maeneo ambayo bado maji ni tatizo ni moja ya majukumu yangu nikuombe Mheshimiwa Mbunge, mara baada ya Bunge hili la bajeti, mwezi wa saba tutaona namna njema ya kufika maeneo yote ambayo yanamiradi ambayo haifanyi vizuri.

SPIKA: Mheshimiwa George Mwenisongole, swali la nyongeza.

MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada kubwa za Serikali kusambaza maji vijijini jitihada hizi zinaweza kuwa bure iwapo gharama ya kuunganishiwa maji kwenye nyumba za wananchi hazitashuka. Je, Serikali haioni sasa ni wakati umefika wa kuangalia hizi gharama za kuunganishiwa maji kwa wananchi, *especially* wananchi wa vijijini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa George Mwenisongole kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, gharama za uunganishi Wizara tunaendelea kuzipunguza kwa kuzisogeza bomba kuu ambalo litambunguza umbali wa kutoka kwenye *main line* kwenda kwa watumiaji, na tayari kazi hii imeanza katika

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

maeneo mbalimbali. Hivyo, ninatarajia kuwa hata katika jimbo lake pia huduma hii itamfikia.

SPIKA: Mheshimiwa Boniventura Kiswaga swali la nyongeza.

MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru ni lini Serikali itapeleka maji katika Kata ya Kisesa Bujorwa Bukandwe Bujashi ambazo zina matatizo ya maji?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Boniventura Kiswaga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maeneo yote ambayo bado miradi haijaanza ama miradi imeanza lakini ipo kwenye utekelezaji tutakavyopata fedha, ndani ya mwaka huu wa fedha na mwaka ujao tutakuja kuendelea na kazi ya usambazaji wa maji.

SPIKA: Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, swali la nyongeza.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Mji wa Tarime ilipaswa upate maji kutoka Ziwa Victoria kwenye mradi wa miji 21 na Waziri wakati wa bajeti iliyopita aliahidi hapa kwamba kufikia Septemba utakuwa huo mradi umeshaanza na kuelekea matumaini ya kumalizika, lakini mpaka sasa hivi bado haujaanza. Sasa, ni lini huu mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda mji wa Tarime utakamilika?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Matiko kama ifuatavyo: -

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, ni miji 28 siyo miji 21. Miji 28 itaanza kutekelezwa hivi punde kabla ya mwaka huu wa fedha kuisha.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwa Wabunge na majibu kutoka upande wa Serikali. Ninayo matangazo hapa mbele, tutaanza na tangazo la wageni.

Kwanza ni wageni walioko Jukwaa langu pale juu. Wapo wageni 15 wa Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro ambaye ni Waziri wa Katiba na Sheria na hawa ni Watendaji Wakuu wa Wizara hiyo; yupo Bi. Mary Gasper Makondo ambaye ni Katibu Mkuu, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Dkt. Khatibu Malimi Kazungu ambaye ni Naibu Katibu Mkuu, yupo pia Mheshimiwa Jaji Gerson Johh Mdemu ambaye ni Jaji Mfawidhi Mahakama Kuu Kanda ya Dodoma, Yupo Mheshimiwa Jaji George Masaju Jaji Mahakama Kuu Kanda ya Dodoma. karibu sana. *(Makofi)*

Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Tunaye pia Prof. Elisante Ole Gabriel Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania. Tunaye pia bwana Wilbert Martin Chuma ambaye ni Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, karibu sana. Tunaye pia Mheshimiwa Jaji Mstaafu January Msofe ambaye ni Mwenyekiti wa Tume ya kurekebisha Sheria, tunaye pia bwana Sylvester Mwakitalu ambaye ni Mkurugenzi wa Mashtaka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka. karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Bwana Mohamed Hamis Hamad ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Tume Haki za Binadamu na Utawala Bora. Tunaye pia Bi. Angela Kemanzi Anatory ambaye ni Kabidhi Wasii Mkuu na Mtendaji Mkuu Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhadini. karibu sana. Tunaye ndugu Patience Kilanga ambaye ni Katibu Mtendaji Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, tunaye pia Mheshimiwa Jaji Dkt. Benhaji

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Masoud ambaye ni Mkuu wa Chuo Taasisi ya Uanasheria kwa Vitendo. Tunaye Bwana Onorius Njole ambaye ni Mwandishi Mkuu wa Sheria Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro anao wageni wengine ambao ni familia yake na hapo yupo, Mke wake Bi. Florah Ndumbaro, yupo kaka yake Kaka yake bwana John Ndumbaro, Dada yake Dkt. Dafina Ndumbaro, Shemeji yake Ndg. Candida Myovela, Pamoja na watoto wake Ndg. Daniel Ndumbaro na Bryan Ndumbaro na wapo wadau kutoka *UN-Women*, LSF na TAWLA wote wasimame kwa Pamoja. Karibuni sana sana wageni wote wa Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro.

Waheshimiwa Wabunge, hizi kelele ni kwamba hamjamuona Bi. Florah Ndumbalo ama, hamjamuona Watoto wanatunzwa jamani. *(kicheko/Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, Wageni 35 wa Mheshimiwa Almas Maige ambao ni wanafunzi wa Chuo kikuu cha Dodoma wanaotokea Jimbo la Tabora Kaskazini, Mkoa wa Tabora. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Mgeni wa Mheshimiwa Priscus Tarimo ambaye ni mwanafunzi wa Masters Chuo cha Uhasibu Arusha. Tunao wageni wengine 15 wa Mheshimiwa Priscus Tarimo ni wachezaji wa Ofisi ya Katibu Tawala kutoka Moshi Mkoa wa Kilimanjaro wakiongozwa na Ndugu Evelyne Mmari, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Ngw'asi Kamani ambaye ni Mwenyekiti wa UVCCM Mkoa wa Mwanza Ndugu Jonas Lufunguro. Karibuni Sana *(Makofi)*

Tunao Wageni sita wa Mheshimiwa Rehema Migilla ambao ni marafiki zake kutoka Mkoa wa Tabora. Karibu sana. *(Makofi)*

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Tunao Wageni wawili wa Mheshimiwa Timotheo Mnzava ambao ni marafiki zake kutoka Tansia ya Ujenzi Jijini Dar es Salaam. Karibu sana. (*Makofi*)

Wageni Waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi 120 na walimu 20 kutoka Shule ya Sekondari Mwanzi iliyoko Wilaya ya Manyoni Mkoani Singida. Karibu sana. (*Makofi*)

Tunao Wanafunzi 100 kutoka Chuo Kikuu cha Mipango Mipango, eh! Hivi Mipango ni Chuo Kikuu cha Mpingo? Naona hapa kimeandikwa Chuo Kikuu sasa nisije nikakipa hadhi ya kuwa Chuo Kikuu ikawa mtihani. Wanafunzi 100 kutoka Chuo cha Mipango. Karibuni sana sana sana. (*Makofi*)

Ahsanteni sana Wageni wetu karibuni sana Bungeni tunaamini mtajifunza mawili matatu mkiwa hapa.

Ninalo tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote na Watumishi wa Bunge kwamba leo tarehe 28 Aprili, 2022 kutakuwa na *Iftar* iliyoandaliwa na *Fountain Gate Academy* katika viwanja vya Bunge, pale ambapo huwa tunafanyia hii lbada ya *Iftar*. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge mnakaribishwa sana leo mara baada ya kuahirisha Shughuli za Bunge kukaribia hapo kwenye *Iftar* ambayo ametuandalia ndugu yetu kutoka *Fountain Gate Academy*. Kwa hiyo mnakaribishwa sana Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge ninalo tangazo lingine hapa; Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa hayupo Dodoma. Kwa hivyo kwa kuwa hayupo Dodoma nafasi yake ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bunge ameikamisha kwa Mheshimiwa Captain Mstaafu George Huruma Mkuchika. Kwa hiyo mnamuona hapo amekaa kwenye kiti kinachomstahili. Ahsante sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na ratiba yetu punde lakini niwakumbushe, kwamba kumekuwa na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

utaratibu; sisi tunasema ndio wazazi wa Kiswahili duniani na si tu Afrika Mashariki. Sasa Mheshimiwa Mbunge wewe upo hapa kwa niaba ya wananchi wako kama mwakalishi wao. Kwa hivyo ukisamama hapa tena ukasema kwa niaba ni kama vile nafasi yako huamini kama wewe ni mwakalishi wa hao wananchi. Kwa sababu wameshakutuma wewe ndiyo maana unasema swali langu kwasababu wewe wale watu umewabeba upo nao.

Kwa hiyo hakuna kwa niaba mara mbili; na hata mawaziri mnapowasikia hapa Naibu Waziri anasema kwa niaba ya Waziri kwa sababu yeye si Waziri ni Naibu Waziri wewe upo kwa niaba ya Wananchi wako kwa hiyo huna haja ya kusema kwa niaba tena kwa sababu hiyo nafasi wamekupa wananchi wako uwawakalishe humu ndani. *(Makofi)*

Lingine Kiswahili hapa nasikia miradi kichefukichefu ni miradi chechefu hamna miradi kichefuchefu. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge Kiswahili tukitumie kwa ufasaha sisi wenyewe hamna miradi kichefuchefu ni miradi chechefu. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na ratiba iliyombele yetu.

Katibu.

NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI: Hoja za Serikali; makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2022/2023

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nimeuona Mheshimiwa Tabasam amesimama.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Spika, nasimama kwaajili ya jambo mahsusini ninaloendelea katika nchi hii kwa Kanuni ya 54 (1) (2) na (3) na Kanuni ya 55.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa la bei za mafuta katika nchi hii ambalo linaendelea kwa kasi kubwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

na kutokana na hali hii ni kwamba mafuta yaliyoagizwa katika *tender* za tarehe 28 Mwezi wa tatu *tender* ile ilichezwa. Asubuhi ilitoka *tender* nyingine na jioni *tender* nyingine. Matokeo yake ni kwamba...

SPIKA: Mheshimiwa ngoja Mheshimiwa Tabasam mambo unayozungumza ni mazito sana haya. Na hapa mezani mimi kama Spika sina taarifa hiyo mahsusi ya *tender* kuchezewa.

Sasa kama unayo taarifa hiyo hapo niletee hapa niwe nayo kama huna taarifa hiyo hatuweze kuendelea na hili jambo kwa hayo maelezo yako ya mwanzo kabisa, ya kwamba *tender* ilichezwa, mimi taarifa hizo sina.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Spika, jana nilikuandikia nikakuletea *memo* hapo.

SPIKA: Mheshimiwa Tabasam naomba ukae. Waheshimiwa Wabunge amesimama Mheshimiwa Tabasam hapa kwa mujibu ya kanuni ya 54 akitueleza kwamba analo jambo la dharura ambalo anataka tuahirishe shughuli zetu hapa ili tusikilize hiyo hoja yake ili tuweze kuona namna ambavyo Bunge hili linaweza kujadili hiyo hoja ili tuishauri Serikali kuchukua hatua mbalimbali ama tuiagize Serikali kuchukua hatua mbalimbali zile ambazo haziwezi kuchukuliwa katika utaratibu wa kawaida.

Sasa katika maelezo yaliyopo katika kanuni yetu ya 54 inataka mimi nimsikilize Mbunge halafu nikishaelewa hiyo hoja yake nimpe nafasi atoe hoja halafu akitoa hoja iunge mkono; ndio utaratibu wa kanuni ya 54 lakini matumizi ya kanuni ya 54 yanataka masharti ya kanuni 55 yawe yamekamilishwa ndipo hiyo hoja iletwe ili Bunge lijadili kama hoja ya dharura.

Sasa ile amesimama tu naanza kumsikiliza ili nijiridhishe hiyo hoja itolewe kwa Bunge au hapana amesema mambo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mazito sana hapa ambayo mpaka mimi yananipa wasiwasi wa kuendelea kumsikiliza kwenye hiyo hoja yake. Wakati namuuliza kama anayo taarifa aniletee anasema aliniandikia sasa ujumbe alioniandikia jana ni kama hayo maneno hayo kwanza aliyoyasema saa hizi hayakuwepo yeye alisema tu nataka kutumia kanuni ya 54 nisimame niseme jambo la dharura.

Kwa hiyo hana taarifa yoyote aliyoniletea mimi kwamba *tender* ilichezewa.

Kwa hiyo jambo hilo siwezi kuliruhusu hapa kwa sababu ni mambo mazito ambayo tutapelekana sehemu ambayo yeye atatakiwa apelekwe kwenye kamati akaanze kuleta ushahidi na mambo kama hayo.

Kwa hiyo siwezi kuliruhusu jambo hilo kuzungumzwa hapa mpaka nitakapopata huo ushahidi. (*Makofi*)

Katibu.

NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI

HOJA ZA SERIKALI

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge Hoja za Serikali Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro aje awasilishe hoja yake.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili ya kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mpango wa Bajeti wa Wizara na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza mwaka mmoja tangu ashike nafasi ya kuongoza nchi yetu.

Katika kipindi hicho tumeshuhudia mafanikio makubwa katika sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Sheria. Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wenzangu kuendelea kumuomba Rais wetu kwa Mwenyezi Mungu amjalie kila la heri katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wao mahiri katika kulitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba kukupongeza wewe binafasi Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa na Bunge na kupata ushindi wa kishindo. Kuchaguliwa kwako kunaonesha imani kubwa waliyonayo Wabunge ya kuliongoza Bunge hili kwa umahiri mkubwa. Aidha nimpongeze Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb) kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile niwapongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Katiba na Sheria Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba, na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge la Bajeti Mheshimiwa Sillo Daniel Baran Mbunge wa Babati Vijijini, Makamu Wenyeviti pamoja na Wajumbe wa Kamati hizo kwa ushauri na maelekezo ambayo yamewezesha Wizara na Taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai Mbunge, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha Mbunge, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni matumaini yangu kuwa Wabunge hawa watashirikiana na Wabunge wengine katika kutekeleza majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini na kuiteua kuongoza Wizara hii ya Katiba na Sheria. Ninaahidi kuendelea kuitumikia nafasi hii kwa uaminifu na uadilifu ili kuwaletea maendeleo wananchi na Taifa kwa ujumla. Aidha, namshukuru na kumpongeza kwa dhati mtangulizi wangu Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu kwa kuingoza Wizara hii kwa umahiri. Vilevile, nimpongeze Mheshimiwa Balozi Daktari Pindi Hazara Chana Mbuge kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Bunge lako lilipoteza Waheshimiwa Wabunge ambao tulikuwa nao katika Bunge hili. Wabunge hao ni Mheshimiwa William Tate Olenasha, aliyekuwa Mbunge wa Ngorongoro na Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (CCM) Mkoa wa Rukwa. Hivyo, naomba nitumie fursa hii kutoa salamu zangu za pole kwako wewe binafsi Mheshimiwa Spika, Bunge lako kwa ujumla, Ndugu, wananchi wa Majimbo husika waliopoteza wapendwa wao. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu hao mahala pema, peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilitunga Sheria ya Usuluhishi, Sura ya 15 na Marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Daawa Sura ya 33 na Kanuni zake. Sheria hizi zinaweka misingi ya utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala za usuluhishi, upatanishi, majadiliano na maridhiano. Hadi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kufikia Machi, 2022 jumla ya Wasuluhishi 192, Wapatanishi 106, Waendesha majadiliano 37 na Waendesha Maridhiano 23 walisajiliwa na kupatiwa vyeti.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 Mahakama ilikuwa na Jumla ya mashauri 241,793. Kati ya mashauri hayo mashauri 178,877 yalisikilizwa na kuhitimishwa. Aidha, Mahakama inaendelea na mipango ya kuboresha matumizi ya TEHAMA ili kuongeza kasi ya kuhitimisha usikilizwaji wa mashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha miundombinu ya utoaji haki, Mahakama ilitekeleza miradi 37 katika ngazi mbalimbali za Mahakama. Hadi kufikia Machi, 2022 miradi hiyo imefikia katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ilivyooneshwa katika ukurasa wa Tisa hadi 11 wa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa kuna uwazi na uhakika katika huduma za Mahakama, Mahakama imeanzisha kituo cha mawasiliano na wateja ambacho kinafanya kazi masaa 24 kila siku. Lengo kubwa la kituo hicho ni kuhakikisha wananchi kwamba endapo hawajaridhika na huduma za Mahakama au wanataka kutoa pongezi au maoni fursa hiyo ipo. Mawasiliano ya simu ya kituo hicho ni nambari 0752 500 400, barua pepe ni maoni@judiciary.go.tz. Huduma hii inatarajiwa kuanza kutumiwa na mahabusu na wafungwa kuanzia mwezi Mei, 2022. Pia na wananchi wote wenye uhitaji huo. Natoa wito kwa Watanzania watumie fursa hii muhimu kutoa mrejesho au maoni kwa Uongozi wa Mahakama ili kuboresha mnyororo wa utoaji haki nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa Sheria za nchi zinakwenda na wakati na zinaakisi sera na vipaumbele vya Serikali kuhusu maendeleo katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, mazingira na teknolojia. Miswada ya Sheria iliyoandaliwa na kupitishwa kuwa Sheria zilizofanyiwa urekebu na zilizotafsiriwa kutoka Lugha ya Kingereza kuwa Kiswahili zimeonyeshwa katika ukurasa wa 11 na wa 12 wa hotuba hii.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Wizara imeendelea kushirikia na kutoa ushauri wa kisheria katika majadiliano mbalimbali ya Mikataba ya Kibiashara, Mikutano ya Kimataifa ya Kikanda na ya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Wizara iliendelea kuratibu shughuli za upelelezi wa makosa ya Jinai kufungua na kuendesha mashauri ya Jinai Mahakamani. Mashauri ya Jinai yaliyoendeshwa katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 yameonyeshwa kwenye ukurasa wa 13 hadi wa 15 katika hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kuiwakilisha Serikali na Taasisi zake kwenye mashauri ya Madai na Usuluhishi kwenye Mahakama na Mabaraza mbalimbali ya usuluhishi ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu masuala ya Kiseru yanayohusu kukuza, kulinda na kuhifadhi misingi ya haki za binaadamu na uratibu wa utoaji wa misaada wa Kisheria. Kazi zilizofanyika na mafanikio yaliyopatikana yameelezwa katika ukurasa wa 16 hadi wa 18 katika hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Kabidhi Mkuu imeimarisha shughuli za usajili wa matukio muhimu ya binaadamu na takwimu za vizazi, vifo, ndoa, talaka na watoto wa kuasili ikiwa ni haki ya msingi wa utambuzi na upatikanaji wa takwimu kwa ajili ya maendeleo ya Taifa. Kazi zilizotekelezwa na mafanikio yaliyopatikana yameelezwa katika ukurasa wa 21 na 23 wa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Kurekebisha Sheria ilikamilisha taarifa nne za tathmini ya utekelezaji wa Sheria ambazo zinahusu mifumo ya Adhabu Mbadala, Sekta ya Utalii, Sekta ya Mifugo na Sekta ya Uvuvi. Kwa upande wa Adhabu Mbadala Sheria zilizofanyiwa tathmini ni pamoja na Sheria ya Magereza Sura ya 58, Sheria

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20, Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi, Sura ya 200, Sheria ya Huduma za Jamii, Sura ya 291, Sheria ya Bodi ya Msamaha, Sura ya 400 na Sheria Ukomo wa Adhabu, Sura ya 90. Vilevile Tume ilifanya tathmini ya Sheria ya Utalii Sura ya 65, Sheria ya Wanyamapori Sura ya 283, Sheria ya Mbuga za Wanyama Sura ya 282, Sheria ya Makumbusho ya Taifa, Sura ya 281, Sheria ya Hifadhi ya Eneo la Mamlaka ya Ngorogoro, Sura ya 284 na Sheria ya Malikale Sura ya 333.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imeendelea kushirikiana na Mataifa mengine katika kupambana na kusimamia kurejeshwa kwa watuhumiwa wa uhalifu katika nchi walizofanya makosa. Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa mkataba wa urejeshwaji wa wahalifu na ushirikiano katika masuala ya Jinai baina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kenya. Wizara ilipokea na kushughulikia maombi matano ya kuwarejeshwa wahalifu wa makosa ya jinai waliokimbilia nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha watumishi wa Sekta ya Sheria wanakuwa na ujuzi na weledi wa kutosha katika kutimiza wajibu wao kwa ufanisi, Wizara kupitia Chuo cha Uongozi wa Mahakama - Lushoto imeendelea kuratibu na kutoa mafunzo endelevu na elekezi ya Kimahakama kwa watumishi wa Mahakama na wadau wa Sekta ya Sheria nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania, imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kutoa mafunzo ya uanasheria kwa vitendo. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 Taasisi imedahili jumla ya wanafunzi 1,507 na imetunuku vyeti kwa wahitimu 293 wanaostahili kusajiliwa kuwa Mawakili na kufanya idadi ya wahitimu waliopata mafunzo kupitia Taasisi hiyo tangu kuanzishwa kwake mwaka 2007 kufikia 7,561. Maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara umeonyesha katika ukurasa wa sita hadi wa 39 wa hotuba hii.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara ilipanga kukusanya Maduhuli kiasi cha Shilingi 12,672,596,000 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato. Hadi kufikia Machi, 2022 jumla ya Shilingi 6,018,450,528 zilikusanywa. Mchanganuo wa maduhuli yaliyokusanywa na kila Fungu la Wizara umeoneshwa ukurasa wa 40 wa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria iliidhinishwa na Bunge jumla ya Shilingi 231,693,745,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 Wizara ilipokea Shilingi 194,115,559,872 sawa na asilimia 84 ya fedha zilizoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022. Mchanganuo wa fedha zilizopokelewa kwa kila Fungu la Wizara umeonyeshwa katika kiambatisho (H) cha hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatika katika kila Wizara ni pamoja na kuimarisha mfumo wa utoaji haki nchini kwa kutumia Lugha ya Kiswahili katika Uandishi wa Sheria na shughuli za utoaji haki Mahakamani. Kuongezeka kwa wigo wa mfumo wa utoaji haki kwa kuwezesha Mwakili wa Serikali kuanza kutoa huduma za Uwakili katika Mahakama za Mwanzo. Kuimarisha mfumo wa utatuzi wa migogoro nje ya Mahakama kwa kutumia njia mbadala ambazo ni majadiliano, maridhiano, upatanashi na usuluhishi. Kuendelea na matumizi ya Lugha ya Kiswahili katika shughuli za Mahakama na Uandishi wa Nyaraka za Kisheria ambao umeongeza uelewa wa Sheria kwa wananchi na hivyo kurahisisha upatikanaji wa haki kwa wakati na kwa gharama nafuu. Kuunganishwa kwa mfumo wa Wakala wa Usajili wa Ufilisi na Udhamini na Mahakama ambapo imerahisisha uhakiki wa amri za Mahakama kupitia njia ya mtandao. Maelezo ya kina kuhusu mafanikio yaliyopatikana yameonyeshwa katika ukurasa wa 42 na 45 wa hotuba hii. Aidha, changamoto za utekelezaji wa majukumu na mikakati ya kutatua changamoto hizo imeoneshwa ukurasa wa 44 hadi 45 wa hotuba hii.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kutoa shukrani za dharti kwa ushirikiano mzuri uliopo kati ya washirika wa maendeleo ikiwa ni pamoja na Benki ya Dunia, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*), Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Wakimbizi (*UNICEF*), Shirika la Umoja wa Mataifa la Wanawake (*UNWOMEN*), Umoja wa Ulaya (*EU*), Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Uingereza (*FCDO*), Mahakama ya Uingereza, Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki, *LSF*, *TAWLA* na Chama cha Mawakili wa Tanganyika (*TLS*). Wadau wengine walioshiriki katika kuleta mafanikio ya Wizara ni pamoja na Kampuni ya Simu ya *TIGO* ambayo imeipatia Ofisi ya Kabidhi Mkuu simu janja 1,046 kwa ajili ya usajili wa watoto chini ya umri wa miaka mitano katika Mikoa Mitatu ya Mwanza, Rukwa na Katavi. Hivyo kufanya jumla ya Mikoa iliyopokea simu janja kwa ajili ya usajili kufikia Mikoa 22.

Mheshimiwa Spika, inatarajiwa kuwa kampuni hiyo itaendelea na kutoa msaada wa simu janja kwa ajili ya usajili wa watoto katika Mikoa Minne (4) iliyobaki ambayo ni Tabora, Kigoma, Kagera na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha Shilingi 12,676,201,000.00 ikiwa ni Maduhuli ya Serikali. Maduhuli yatakusanywa katika kila Fungu la Wizara yameoneshwa katika ukurasa 49 na 50 wa hotuba hii. Ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 272,768,278,800 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya Fedha hizo, shilingi 207,703,708,800 ni za matumizi ya kawaida na shilingi 65,064,570,000 ni miradi ya maendeleo. Mchanganuo wa makadirio ya bajeti kwa Mafungu ya Wizara ni kama ilivyooneshwa katika ukurasa wa 52 hadi wa 50 wa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Viongozi na Watendaji wa Wizara na Taasisi kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Hakika ni kutokana na ushirikiano huo nimeweza kusimama leo hii mbele ya Bunge lako kuelezea mafanikio, mipango na mikakati tuliyonayo katika kuwahudumia wananchi. Hivyo, kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda - Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Ndugu Mary Gasper Makondo - Katibu Mkuu, Daktari Khatibu Malimi Kazungu - Naibu Katibu Mkuu, Mheshimiwa Profesa Ibrahimu Hamisi Juma - Jaji Mkuu wa Tanzania na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, Mheshimiwa Jaji Daktari Eliezer Mbuki Feleshi - Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Mustapher Mohamed Siyani Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Profesa Elisante Ole Gabriel Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, Mheshimiwa Wilbert Martin Chuma - Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Ndugu Sylvester Anthony Mwakitalu - Mkurugenzi wa Mashtaka, Ndugu Gabriel Pascal Malata - Wakili Mkuu wa Serikali, Ndugu Angela Kemanzi Anatory - Kabidhi Mkuu na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhadini, Mheshimiwa Jaji Mstaafu wa Mahakama ya Rufani January Henry Msoffe - Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Ndugu Casmir Sumba Kyuki - Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Mheshimiwa Jaji Mstaafu wa Mahakama Kuu ya Tanzania - Mathew Mhina Mwaimu - Mwenyekiti Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Ndugu Patience Kilanga Ntwina - Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Mheshimiwa Jaji wa Mahakama ya Rufani Daktari Paul Faustin Kihwelo - Mkuu wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, Mheshimiwa Jaji wa Mahakama Kuu - Dkt. Benhajj Shaaban Masoud - Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania, Mkurugenzi na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Jaji Mdemu na Jaji Masaju kwa kuweza kushiriki nasi katika shughuli hii ya leo. Aidha, nawashukuru familia yangu ikiwa ni pamoja na mke wangu Ndugu Flora Ndumbaro na watoto kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia kwa kunivumilia na kunitia moyo wakati ninapokuwa natekeleza majukumu yangu ya kulitumikia Taifa.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, naomba nichukue fursa hii kwa namna ya kipekee kabisa kuwashukuru Wapiga kura wa Jimbo langu la Songea Mjini kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika shughuli za kuleta maendeleo ya Jimbo letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA, MHESHIMIWA
DKT. DAMAS DANIEL NDUMBARO (MB), WAKATI
AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 -
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

A. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa zilizowasilishwa leo katika Bunge lako na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Salamu za Pongezi, Shukrani na Pole

2. Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili ya kujadili taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na mwelekeo wa mpango na bajeti ya Wizara na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Aidha, ninaomba kuwatakia heri ya Mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhani kwa Waislamu wote. Vilevile, nitumie fursa hii kuwatakia wananchi wote kheri ya sikukuu ya Eid.

3. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kutimiza mwaka mmoja tangu ashike nafasi ya kuongoza nchi yetu akiwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kipindi hicho,

tumeshuhudia mafanikio makubwa katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya sheria. Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wenzangu kuendelea kumuomba Rais wetu kwa Mwenyezi Mungu amjaalie kila la kheri katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania.

4. Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wao mahiri katika kuitumikia Taifa letu.

5. Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwako na Bunge na kwa kupata ushindi wa kishindo. Kuchaguliwa kwako kunaonesha imani kubwa waliyonayo Wabunge ya kuliongoza Bunge hili kwa umahiri mkubwa. Aidha, nimpongeze Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania. Vilevile, niwapongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa Babati Vijijini, Makamu Wenyeviti pamoja na Wajumbe wa Kamati hizo mbili kwa ushauri na maelekezo ambayo yamewezesha Wizara na Taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

6. Mheshimiwa Spika, Nitumie fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai (Mb.) kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni matumaini yangu kuwa Wabunge hao watashirikiana na Wabunge wengine katika kutekeleza majukumu yao.

7. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniadini na kuiteua kuiongoza Wizara hii ya Katiba na Sheria. Ninaahidi kuendelea kuitumikia nafasi hii kwa uaminifu na uadilifu ili kuwaletea maendeleo wananchi na Taifa kwa ujumla. Aidha, namshukuru na kumpongeza kwa dhati mtangulizi wangu Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kwa kuingoza Wizara hii kwa umahiri. Vilevile, nimpongeze Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana (Mb.), kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

8. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Bunge lako lilipoteza Waheshimiwa Wabunge ambao tulikuwa nao katika Bunge hili. Wabunge hao ni Mheshimiwa William Tate Olenasha, aliyekuwa Mbunge wa Ngorongoro na Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (CCM) Mkoa wa Rukwa. Hivyo, naomba nitumie fursa hii kutuma salamu zangu za pole kwako wewe binafsi Mheshimiwa Spika, Bunge lako kwa ujumla, ndugu na wananchi wa majimbo husika waliopoteza wapendwa wao. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu hao mahala pema peponi. Amina.

B. DIRA NA DHIMA

9. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria inaongozwa na Dira ambayo ni Katiba na Sheria wezeshi kwa maendeleo ya Taifa. Dira inalenga kuweka mazingira rafiki ya kiseru na ya kisheria ya kuwezesha utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Taifa, kudumisha hali ya amani, utulivu na utangamano wa kitaifa ambazo ni nguzo muhimu kwa mstakabali wa Taifa letu. Aidha, Dhima ya Wizara ni Kuwa na mfumo madhubuti wa Kikatiba na Sheria wenye kufanikisha utekelezaji wa sera na mipango kwa maendeleo ya Taifa. Dhima hii inahimiza ubunifu katika kujenga mazingira wezeshi ya upatikanaji haki na huduma bora za

kisheria kwa wananchi. Aidha, Dira na Dhima hii imeakisiwa katika Dira na Dhima za Taasisi.

C. MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA

10. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria inajumuisha Mhimili wa Mahakama ya Tanzania, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Tume ya Utumishi wa Mahakama, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania na Chuo cha Uongozi wa Mahakama-Lushoto. Katika kutekeleza majukumu yake ya kuhakikisha kuwa nchi inaongozwa kwa kuzingatia Katiba, sheria, Kanuni na taratibu zilizowekwa na vyombo halali vya maamuzi, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Hati ya Mgawanyo wa Majukumu kwa Mawaziri, kupitia Tangazo la Serikali Na. 534/2021 majukumu hayo ni: -

(i.) Kutunga Sera zinazohusu masuala ya kisheria na kusimamia utekelezaji wake;

(ii.) Kushughulikia mambo ya kikatiba;

(iii.) Kusimamia mfumo wa haki na utoaji haki;

(iv.) Uandishi wa sheria;

(v.) Kuendesha mashtaka ya jinai;

(vi.) Kushughulikia uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi;

(vii.) Usuluhishi wa migogoro ya kibiashara, Sheria za kimataifa na Mikataba;

(viii.) Kuratibu masuala ya haki za binadamu na utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria;

(ix.) Kuratibu shughuli za usajili wa matukio muhimu ya binadamu, ufilisi na udhamini;

- (x.) Kuratibu tathmini na maboresho ya Sheria;
- (xi.) Kuratibu ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sheria za Utajiri na Maliasilia za nchi;
- (xii.) Kushughulikia urejeshwaji wa wahalifu na masuala ya ushirikiano wa kimataifa kwenye makosa ya jinai;
- (xiii.) Kuboresha utendaji na maendeleo ya rasilimali watu iliyo chini ya Wizara; na
- (xiv.) Kuratibu shughuli za taasisi, mipango na miradi chini ya Wizara.

D. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

11. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022 umezingatia miongozo mbalimbali ya kisera ya Kitaifa, kikanda na kimataifa. Miongozo hiyo ni pamoja na Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka Mitano 2021/22- 2025/26 ambao unalenga kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 hadi 2025; Maelekezo ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania aliyoyatoa wakati akihutubia Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Aprili, 2021 pamoja na maelekezo ya viongozi wakuu wa Serikali. Aidha, Wizara inazingatia Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia 2030; Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063; Mpango Mkakati wa SADC wa Maendeleo 2020-2030; Mpango Mkakati wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Maendeleo 2021/2022 – 2025/2026; pamoja na Mpango Mkakati wa Wizara wa mwaka 2021/22-2025/26.

12. Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara na Taasisi zake ilibainisha

masuala mahsusi ya kipaumbele kuwa msingi wa kutekeleza majukumu yake. Utekelezaji wa majukumu ya Wizara ni kama ifuatavyo:-

I. Kushughulikia Masuala ya Kiseru ya Sekta ya Sheria na Kusimamia Utekelezaji wake

13. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu masuala ya kiseru na kikatiba ili kuhakikisha kuwa haki inafikiwa na inapatikana kwa wakati na gharama nafuu. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 Wizara iliendelea kuimarisha, kusimamia na kuratibu mfumo wa utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala ndani na nje ya mfumo wa Mahakama. Wizara ilisimamia kutungwa kwa Sheria ya Usuluhishi, Sura ya 15 na Marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Daawa, Sura ya 33. Sheria hizi zinaweka misingi ya utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi, upatanishi, majadiliano na maridhiano. Aidha, Waziri mwenye dhamana na masuala ya Sheria alitengeneza Kanuni za Sheria hizo ili kuwezesha utoaji haki kwa wakati, kupunguza gharama za uendeshaji mashauri, mlundikano wa mashauri na kurahisisha ufikiaji wa haki. Kanuni hizo zimeweka misingi ya ithibati ya watoa huduma za utatuzi wa migogoro na utambuzi wao. Vilevile, Wizara imefanikisha kuweka mfumo wa usajili wa Watatuzi wa migogoro kwa njia mbadala ambapo, jumla ya Wasuluhishi 192, Wapatanishi 106, Waendesha majadiliano 37 na Waendesha Maridhiano 23, walisajiliwa na kupatiwa vyeti.

14. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wadau wa Sekta imeratibu zoezi la maandalizi ya Sera ya Taifa ya Mashtaka ambapo Andiko la Mapendekezo ya kutunga sera hiyo limekamilika. Sera hiyo inalenga kuimarisha huduma za uendeshaji wa Mashtaka ya jinai nchini ili kuhakikisha Serikali inaimarisha hali ya amani na usalama katika jamii. Vilevile, Wizara iliandaa rasimu ya Kanuni za Sheria ya Kuwalinda Mashahidi na Watoa Taarifa za Uhalifu (Sura 446).

15. Mheshimiwa Spika, Kuhusu masuala ya ufuatiliaji haki, Wizara imeendelea kuratibu masuala ya kiseru yanayohusu

utoaji haki kwa kutembelea na kukagua maeneo ya vizuizi ikiwemo Magereza, Mahabusu za watoto na vituo vya Polisi. Aidha, Wizara ilitembelea Mahakama Kuu, Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mwanzo pamoja na vituo jumuishi vya utoaji haki vya Mahakama. Lengo la kaguzi hizi ni kufuatilia utekelezaji wa haki, kuainisha changamoto za kiutendaji na kiupelelezi na kutoa maelekezo stahiki ya kutatua changamoto hizo. Wizara ilikagua utendaji kazi wa Taasisi hizo ili kubaini endapo unazingatia misingi ya Utawala Bora, Utawala wa Sheria na utoaji haki kwa wananchi. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 jumla ya magereza 129 yalikaguliwa ikilinganishwa na magereza 64 yaliyokaguliwa kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021. Aidha, vituo vya polisi 391 vilikaguliwa ikilinganishwa na vituo vya polisi 180 vilivyokaguliwa katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021. Zoezi hilo la ukaguzi wa maeneo ya vizuizi umewezesha kupunguza mlundikano wa Mahabusu kwa kuwaachia huru jumla ya Mahabusu 809. Kwa upande wa Zanzibar vyuo vya mafunzo tisa (9) na vituo vya polisi 17 vilikaguliwa katika mikoa yote ya Zanzibar. Orodha ya vituo vya Polisi na Magereza vilivyokaguliwa na idadi ya Mahabusu walioachiwa huru kwa kila Mkoa imeoneshwa katika Kiambatisho A.

16. Mheshimiwa Spika, Matokeo ya ukaguzi yalionesha kuwa hali ya magereza na vyuo vya mafunzo inaendelea kuboreshwa kwa kuzingatia vigezo vya haki za binadamu ikilinganishwa na kaguzi zilizopita. Maeneo yaliyoboreshwa ni pamoja na haki ya kupata chakula, malazi, afya na haki ya kupata habari. Aidha, kutokana na mapendekezo ya taarifa ya tathmini jitihada zinaendelea kufanyika ili kuboresha hali ya uzingatiwaji wa haki za binadamu katika maeneo hayo.

II. Kusimamia mfumo wa haki na utoaji haki (a) Usikilizwaji wa Mashauri

17. Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu suala la kupunguza mlundikano wa mashauri mahakamani limekuwa ni moja ya vipaumbele muhimu vya Serikali katika kuhakikisha kuwa

wananchi wote wanapata haki sawa na kwa wakati. Kwa kipindi cha kuanzia Mwezi Julai 2021- Machi, 2022 kulikuwa na Jumla ya mashauri 241,793. Kati ya mashauri hayo mashauri 178,877 (sawa na asilimia 74) yalisikilizwa na kuhitimishwa. Mahakama inendelea na mipango ya kuboresha matumizi ya TEHAMA ili kuongeza kasi ya kuhitimisha uskilizwaji wa mashauri.

(b) Kuboresha Miundombinu ya Utoaji Haki

18. Mheshimiwa Spika, Mahakama imeendelea na utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) wa Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Mahakama, ambapo katika mwaka 2021/2022 miradi 37 ilitokelezwa katika ngazi mbalimbali za Mahakama. Hadi kufikia Machi, 2022 miradi imefikia katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo:

i. Miradi iliyokamilika; Ujenzi wa vituo Jumuishi sita (6) vya kutoa haki (JCs) katika mikoa ya Dar es salaam (Kinondoni na Temeke), Dodoma, Morogoro, Mwanza na Arusha; Ujenzi wa Mahakama za Hakimu Mkazi mbili (2) katika Mikoa ya Katavi na Lindi; ujenzi wa Mahakama za Wilaya nne (4) katika wilaya za Bahi, Chemba, Rungwe na Bunda; ujenzi wa Mahakama za mwanzo tatu (3) za Matiri (Mbinga), Hydrom (Mbulu), na Kibaigwa (Kongwa) na ujenzi wa Jengo la Kuhifadhi Kumbukumbu – Tanga.

ii. Miradi inayoendelea; ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mahakama Dodoma ambapo ujenzi wa boma (structure) umekamilika kwa asilimia 100; Ukarabati na upanuzi wa Mahakama Kuu Tabora; ujenzi wa Mahakama za Hakimu Mkazi katika Mikoa ya Songwe na Tabora; Ujenzi wa Mahakama za Wilaya za Nanyumbu, Namtumbo, Same, Tandahimba, Kilindi, Sikonge, Mwanga, Kakonko, Buhigwe, Uvinza, Butiama, Rorya, Itilima, Busega, Songwe, Mbogwe, Nyang'wale, Kyerwa, Misenyi, Gairo, Mvomero, Kilombero, Mkinga, Tanganyika na Kaliua. Miradi mingine inayoendelea ni ujenzi wa Mahakama za mwanzo Mang'ula na Mlimba (Morogoro), Nyakibimbili (Bukoba), Kabanga (Ngara), Chanika (DSM), na Kimbe (Kilindi); na Ujenzi wa bweni la

wavulana katika Chuo cha Uongozi wa Mahakama - Lushoto.

19. Mheshimiwa Spika, Mahakama imeendelea kuanzisha na kuboresha mifumo ya utoaji haki kwa kutumia TEHAMA. Hadi kufikia Machi 2022, Mahakama imeanzisha mfumo wa 'SEMA NA MAHAKAMA' wenye lengo la kupata mrejesho wa huduma zitolewazo, malalamiko na mapendekezo. Aidha, Mfumo wa Madalali wa Mahakama umeanzishwa wenye lengo la kuwasajili, kuwasimamia na kuwatambua. Vilevile, Mahakama imefanya maboresho mbalimbali katika mifumo ifuatayo:

Mfumo wa kielektroniki wa usimamizi na uendeshaji wa mashauri (Judicial Statistical Dashboard System - JSDS II); Mfumo wa Mkutano Mtandao (Video Conferencing) unaowezesha kuendesha mashauri kwa njia ya mtandao; Mfumo wa kielektroniki wa kusajili na kuwatambua mawakili (eWakili); Mfumo wa kutambua Viwanja na Majengo ya Mahakama (JMap) wenye lengo la kutambua hali halisi ya majengo na viwanja vya mahakama ili kuwezesha uandaaji wa mpango wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya mahakama nchi nzima; na Mfumo wa kuratibu na kuhifadhi taarifa za mali na vitendea kazi Mahakamani.

III. Uandishi, Urekebu na Ufasiri wa Sheria

20. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa sheria za nchi zinakwenda na wakati na zinaakisi sera na vipaumbele vya Serikali katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, mazingira na teknolojia. Katika kipindi cha Julai 2021, hadi Machi, 2022, miswada ya sheria 11 iliandaliwa ikilinganishwa na Miswada mitatu (3) iliyoandaliwa katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 sawa na ongezeko la asilimia 267. Miswada iliyoandaliwa ni kama ilivyooneshwa kwenye Kiambatisho Na. B. Aidha, Miswada hiyo 11 iliwasilishwa Bungeni na kusomwa kwa mara ya pili na ya tatu. Kati ya Miswada hiyo, tisa (9) imesainiwa na Mhe. Rais kuwa sheria na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali kama inavyoonekana kwenye Kiambatisho C. Aidha, Sheria Ndogo

542 ziliandaliwa na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali au kutumika kama ilivyokusudiwa ikilinganishwa na sheria ndogo 807 zilizoandaliwa katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 sawa na upungufu wa asilimia 33. Upungufu huo ulitokana na kupungua kwa maombi yaliyopokelewa ya kuandaa Sheria ndogo.

21. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wadau imeendelea na zoezi la kutafsiri sheria kutoka Lugha ya Kingereza kwenda Lugha ya Kiswahili. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 kupitia zoezi hili jumla ya Sheria Kuu 214 zilitafsiriwa kwa hatua ya rasimu ya kwanza. Sheria kuu zilizofanyiwa ufasiri zimeoneshwa kwenye Kiambatisho Na. D. Ongezeko hili limetokana na kutekeleza maagizo ya Serikali kuwa Mahakama zote nchini zienteshe mashauri na kutoa hukumu katika lugha ya Kiswahili. Aidha, katika kipindi hicho, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilifanya urekebu wa Sheria Kuu 46 kama inavyoonekana kwenye Kiambatisho E.

IV. Usimamizi wa Masuala ya Mikataba

22. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imeendelea kushiriki na kutoa ushauri wa kisheria katika majadiliano mbalimbali ya Mikataba ya kibishara, mikutano ya kitaifa, kikanda na kimataifa. Katika kipindi cha Julai, 2021, hadi Machi, 2022 jumla ya Mikataba 1,171 ilifanyiwa upekuzi ikilinganishwa na Mikataba 713 katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 sawa na ongezeko la asilimia 64. Ongezo hili linatokana na ongezeko la miradi inayotekelezwa na Serikali. Mikataba hiyo ilihusisha masuala ya ununuzi, ujenzi na ukarabati wa majengo, utoaji wa huduma za jamii kama vile ujenzi wa shule, hospitali na barabara. Kati ya mikataba hiyo 1,171 mikataba 511 ilithaminishwa katika sarafu mbalimbali katika mchanganuo ufuatao: Mikataba 407 ilikuwa na thamani ya Shilingi Trilioni 116.69; Mikataba 88 ilikuwa na thamani ya Dola za Marekani 3,254,993,763.98 sawa na Shilingi Trilioni 7.44; na Mikataba 16 ilikuwa na thamani ya fedha ya Jumuiya ya Ulaya (Euro) 360,569,062.16 sawa na Shilingi Trilioni 0.92.

V.Utoaji wa Ushauri wa Kisheria

23. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ina jukumu la kutoa ushauri wa kisheria kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na kwa wananchi. Lengo ni kuhakikisha ushauri unaotolewa unazingatia maslahi ya umma na kusaidia Serikali kutoingia kwenye migogoro kwa kuhakikisha sheria, kanuni na taratibu za nchi zinafuatwa. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 jumla ya maombi ya ushauri wa kisheria 1,129 yalipokelewa na kufanyiwa kazi ikilinganishwa na maombi 768 katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 sawa na ongezeko la asilimia 47. Kati ya maombi 1,129, maombi 472 yalihusu maombi ya wananchi 657 yanatoka katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa. Kuongezeka kwa maombi ya watu binafsi kunatokana na mwamko wa wananchi wanaoupata katika maadhimisho mbalimbali ikiwemo Wiki ya Sheria, Wiki ya Msaada wa Kisheria pamoja na makongamano mengine ya kisheria.

24. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilishiriki katika mikutano 402 ya ndani ya nchi ikilinganishwa na mikutano 149 katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 sawa na ongezeko la asilimia 170. Aidha, Ofisi ilishiriki katika mikutano 57 inayohusu masuala ya Kikanda na Kimataifa ikiwemo mikutano ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi zilizopo Kusini mwa Afrika (SADC), Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Umoja wa Mataifa (UN).

VI.Kuendesha Mashtaka ya Jinai

25. Mheshimiwa Spika, Katika kulinda misingi ya utawala wa sheria ambayo ni nguzo muhimu ya kudumisha amani, utulivu na umoja wa kitaifa, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendelea kuratibu shughuli za upelelezi wa makosa ya jinai, kufungua na kuendesha mashauri ya jinai mahakamani. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendesha mashauri ya jinai katika

Mahakama za Wilaya, Hakimu Mkazi, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani ambapo Jumla ya mashauri ya jinai 42,138 yaliendeshwa ikilinganishwa na mashauri 26,993 yaliyoendeshwa katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021. Katika kipindi hiki, mashauri 11,676 sawa na asilimia 28 yalihitimishwa ikilinganishwa na mashauri 12,745 sawa na asilimia 47 ya mashauri yaliyohitimishwa katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021. Kati ya mashauri yaliyohitimishwa, 7,117 yalihitimishwa kwa washtakiwa kutiwa hatiani sawa na asilimia 61 ikilinganishwa na mashauri 6,558 sawa na asilimia 52 zilizohitimishwa kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2020 hadi Machi, 2021 na mashauri 30,462 sawa na asilimia 72 ya mashauri yaliyoendeshwa, yalikuwa yanaendelea mahakamani katika hatua mbalimbali ikilinganishwa na mashauri 14,248 sawa na asilimia 53 ya mashauri yaliyoendeshwa, yaliyokuwa yanaendelea katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Ofisi iliendesha jumla ya mashauri 871 katika Mahakama za watoto (Juvenile Courts) ambapo mashauri 315 yalihitimishwa na mashauri 556 yapo katika hatua mbalimbali mahakamani.

26. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka pia imeendelea kushughulikia masuala ya rushwa kwa kushirikiana na Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU). Katika kipindi husika Ofisi ilifanya kikao na vyombo vya upelelezi ambavyo ni TAKUKURU na Jeshi la Polisi ambapo majalada 28 ya mashauri za rushwa yalifanyiwa mapitio na majalada 14 yaliandaliwa Hati za Mashtaka, majalada sita (6) yalirudishwa kwa ajili ya upelelezi zaidi katika maeneo yaliyobainika kuwa na mapungufu, jalada moja (1) lilifungwa kwa kukosa ushahidi na majalada mengine saba (7) yanaendelea kufanyiwa kazi. Washtakiwa waliotiwa hatiani walipewa adhabu mbalimbali zikiwemo vifungo, faini na mali mbalimbali zilitaifishwa. Kiasi cha Shilingi 1,262,893,030.09 kililipwa mahakamani kama faini katika mashauri 3,895 ikilinganishwa na Shilingi 1,025,498,746.00 zilizolipwa kwenye mashauri 4,211 katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021. Aidha, mali mbalimbali zilitaifishwa na Serikali ikiwa ni pamoja na fedha taslim kiasi cha Shilingi

321,068,400, Dola za Marekani 5,000, nyumba tatu (3), matrekta 24, magari 11, pikipiki tano (5), ng'ombe 25, sukari kilo 238, madini aina ya Almasi Karati 11 na vitendea kazi mbalimbali.

27. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeendelea kutekeleza Progamu ya kutenganisha shughuli za upelelezi na uendeshaji mashtaka kwa kusogeza huduma za mashtaka karibu na wananchi katika ngazi za Mikoa na Wilaya. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 Ofisi za Mikoa Mitatu (3) ya kimashtaka ya Kinondoni, Temeke na Ilala (Kinyerezi) zilifunguliwa. Vilevile uzinduzi wa jengo la Ofisi la Wilaya ya Serengeti mkoa wa Mara na hivyo kufanya jumla ya Ofisi za Mikoa ya kimashtaka kuwa 29 na Ofisi za Wilaya zilizofunguliwa kuwa 14.

VII. Kushughulikia Uendeshaji wa Mashauri ya Madai na Usuluhishi 28.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kuiwakilisha Serikali na Taasisi zake kwenye mashauri ya Madai na Usuluhishi yaliyofunguliwa na au dhidi ya Serikali kwenye Mahakama na Mabaraza mbalimbali ya usuluhishi ndani na nje ya nchi. Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022 Wizara kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliendesha mashauri 701 ambapo mashauri ya madai 590 na mashauri ya usuluhishi 111 ikilinganishwa na Mashauri 543 yaliyoendeshwa katika kipindi cha kuanzia Julai 2020 hadi kufikia Machi 2021 sawa na ongezeko la asilimia 29. Kati ya mashauri 701 yaliyoendeshwa, mashauri 247 yalihitimishwa ambapo Serikali ilishinda mashauri 221 na kuokoa Shilingi Bilioni 236.6.

VIII. Kuratibu Masuala ya Haki za Binadamu na Utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria

(a) Kuratibu Masuala ya Haki za Binadamu na Haki za Watu 28. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu masuala ya kisera yanayohusu, kukuza, kulinda na kuhifadhi misingi ya haki za binadamu. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Wizara iliwasilisha Taarifa ya nchi chini ya Mfumo

wa Mapitio katika kipindi Maalum ambapo kila nchi mwanachama anafanyiwa tathmini ya hali ya haki za binadamu kila baada ya miaka minne. Taarifa ya Nchi ilijadiliwa katika Kikao cha Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa kilichofanyika Geneva, Novemba, 2021. Katika kikao hicho Wizara ilitoa taarifa kuhusu jitihada za Serikali katika kukuza, kuheshimu na kulinda haki za kisiasa, kiraia, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii kama ifuatavyo: -

i. Kuhusu Haki ya Kisiasa, taarifa ilibainisha kuwa uchaguzi mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2020 ulifanyika kwa amani na utulivu,

ii. Kuhusu haki za kiraia Serikali ilieleza kwamba ilifanya majadiliano na vyombo vya Habari ili kuimarisha haki ya uhuru wa kujieleza kwa kuboresha kanuni za Maudhui ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, 2020.

iii. Kwa upande haki za kiuchumi, Serikali ilibainisha hatua ambazo zimechukuliwa kuboresha ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Hatua hizo ni pamoja na kuanzisha mfumo wa malipo kwa kielektroniki wa Ankara za malipo ya kodi za ardhi na kuharakisha usuluhishi wa migogoro ya ardhi. Hatua nyingine iliyobainishwa ni Serikali kuboresha upatikanaji wa maji vijijini kutoka asilimia 47 mwaka 2015 hadi asilimia 70.1 mwaka 2020 kwa vijijini na kwa mijini kutoka asilimia 74 mwaka 2015 hadi asilimia 84 mwaka 2020.

iv. Kwa upande wa haki za kijamii Serikali ilianzisha mfumo wa kuwalea Watoto wanaoishi katika mazingira magumu katika mikoa minne ambayo ni Mwanza, Dar es Salaam, Arusha na Iringa.

30. Mheshimiwa Spika, Katika majadiliano hayo Serikali ilipokea mapendekezo 252 kutoka nchi wanachama yenye malengo ya kukuza na kulinda haki za binadamu na haki za watu. Aidha, Wizara ilitibu upatikanaji wa maoni juu ya mapendekezo hayo na kuwasilisha msimamo wa Serikali kutekeleza mapendekezo 187 kati ya mapendekezo yalipokelewa kwenye kikao cha Baraza la Haki za Binadamu mwezi Machi, 2022. Mapendekezo hayo yatakayotekelezwa

yanahusu masuala ya Haki za binadamu, sera, sheria, kanuni, mikakati na mipango ya maendeleo ya nchi, mila, desturi na utamaduni wa watanzania. Hivyo, Serikali iliweza kutimiza wajibu wake kama nchi mwanachama wa umoja wa mataifa kwenye Baraza la Haki za Binadamu pamoja na kuahidi kutekeleza mapendekezo ambayo yamelenga kukuza na kulinda haki za kisiasa, kiraia, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii kwa maendeleo ya watanzania.

31. Mheshimiwa Spika, Katika kuimarisha utoaji wa elimu kwa umma kuhusu hatua za kulinda na kuhifadhi haki za binadamu, Wizara katika kuadhimisha Miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania bara ilishirikiana na Asasi za Kiraia kuandaa Kongamano la Haki za Binadamu na Miaka 60 ya Uhuru. Lengo la Kongamano hilo lilikuwa ni kujadili mafanikio ya Serikali katika kukuza na kulinda haki za binadamu tangu tulipopata uhuru miaka 60 iliyopita. Katika kongamano hilo Wizara na wadau walieleza mafanikio ya sekta kuhusu haki za binadamu ambayo ni pamoja na kuanzishwa kwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora inayosimamia masuala ya haki za binadamu, Kuanzisha Idara mahususi inayoshughulikia masuala ya kisera kuhusu Haki za Binadamu kwenye muundo wa Wizara ya Katiba na Sheria.

(b) Elimu kwa Umma

32. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilitoa mafunzo kuhusu ukatili wa kijinsia kwa Madiwani na Masheha 243 (wanaume 145, wanawake 88) katika Mikoa mitatu (3) ya Tanzania bara ambayo ni Tabora, Iringa na Dodoma na Mikoa mitatu (3) ya Zanzibar ambayo ni Kaskazini Unguja, Kusini Unguja na Kaskazini Pemba. Mafunzo hayo yaliwajengea uwezo wa namna ya kutatua kero za wananchi kwa kuzingatia haki za binadamu na utawala bora. Vilevile, katika mikoa miwili ya Zanzibar, mafunzo yalifanyika kwa wananchi katika Wilaya nne (4) ambazo ni Magharibi A, Magharibi B, Wete na Chakechake ambapo jumla ya washiriki 509 (231 Unguja na 278 Pemba) walipata mafunzo hayo.

33. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imeandaa na kurusha hewani vipindi kumi na tano (15) vya Radio na vipindi sita (6) vya runinga kuhusu Haki za Binadamu na Utawala Bora na majukumu ya Tume. Katika hatua nyingine, Tume ilitumia njia mbalimbali ikiwemo mitandao ya kijamii kama facebook, twitter na instagram kuhamasisha jamii katika kukabiliana na vitendo vya udhallishaji dhidi ya wanawake na watoto.

(c) Kushughulikia Malalamiko ya Uvunjifu wa Haki za Binadamu na Utawala Bora.

34. Mheshimiwa Spika, Katika kusimamia hifadhi ya Haki za Binadamu na ukiukwaji wa misingi ya Utawala Bora nchini, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2021 hadi Machi, 2022 Tume ilifanya ufuatiliaji wa Malalamiko 569 katika Halmashauri za Wilaya 53 zilizopo katika Mikoa 20 ya Tanzania Bara ambayo ni Arusha, Dodoma, Dar es salaam, Geita, Iringa, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Mara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Ruvuma, Singida, Songwe, Tabora na Tanga na mikoa mitano (5) ya Zanzibar ambayo ni Mjini Magharibi, Kaskazini Unguja, Kusini Unguja Kaskazini Pemba na Kusini Pemba. Katika Malalamiko 569 yaliyofuatiliwa, Malalamiko 337 yalihusu uvunjifu wa Haki za Binadamu na Malalamiko 232 yalihusu ukiukwaji wa misingi ya Utawala Bora. Katika ufuatiliaji huo, Malalamiko 253 sawa na asilimia 45 ya Malalamiko yaliyofuatiliwa yalifanyiwa kazi.

35. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilifanya chunguzi maalumu 16 katika maeneo yaliyohusu migogoro ya ardhi, madai ya fidia na matibabu, matumizi mabaya ya madaraka, kuchukua sheria mkononi na uharibifu wa mazingira. Chunguzi zilifanyika katika Mikoa 11 ya Tanzania Bara ambayo ni Dodoma, Manyara, Kigoma, Njombe, Kilimanjaro, Morogoro, Tabora, Shinyanga, Tanga, Dar es salaam, Mtwara na Mkoa wa Mjini Magharibi Zanzibar. Kupitia chunguzi hizi Tume imesaidia wananchi kutatua kero zinazowakabili na kuzishauri mamlaka za Serikali namna ya kuzingatia masuala ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

(d)Kuimarisha Utoaji wa Huduma za Msaada wa Kisheria

36. Mheshimiwa Spika, Wizara inatekeleza jukumu la kuimarisha usimamizi na uratibu wa huduma ya msaada wa kisheria nchini. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 Wizara imesajili Watoa huduma ya msaada wa kisheria 15 na wasaidizi wa kisheria 56 kwa ajili ya kutoa huduma ya msaada wa kisheria kwa wananchi. Idadi hii inafanya jumla ya Watoa huduma ya msaada wa kisheria waliosajiliwa kufikia 202 na Wasaidizi wa Kisheria 763. Aidha, katika kipindi husika jumla ya wananchi 1,455,566 (wanawake 529,079, wanaume 514,051 na watoto 412,436) walipatiwa msaada wa kisheria. Hii ni ongezeko la wanufaika 1,133,124.00 sawa na asilima 351 ikilinganishwa na idadi ya wananchi 322,442 waliopatiwa huduma ya msaada wa kisheria katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021.

37. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022 Wizara kwa kushirikiana na Mahakama ya Tanzania ilianzisha madawati ya msaada wa kisheria katika vituo jumuishi vya utoaji haki sita (6) katika Mikoa ya Dar es salaam (Kinondoni na Temeke), Arusha, Dodoma, Morogoro na Mwanza. Lengo la kuanzisha madawati hayo ni kurahisisha upatikanaji wa huduma ya msaada wa kisheria mahakamani kwa wananchi wenye uhitaji. Pamoja na kuanzisha madawati hayo, Wizara iliwapatia mafunzo wanasheria na mawakili wanaotoa huduma ya msaada wa kisheria katika vituo jumuishi vya utoaji haki. Aidha, Wizara iliwajengea uwezo Watumishi wa Mahakama wakiwemo Maafisa Utumishi na Watunza Kumbukumbu katika vituo jumuishi vya utoaji haki ili kurahisisha utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria.

38. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi hicho, Wizara iliwezesha kufanyika kwa vikao viwili (2) vya Bodi ya Taifa ya Ushauri wa Msaada wa Kisheria ambapo bodi ilipendekeza kuimarisha uratibu wa msaada wa kisheria ambapo pendekezo hili lilifanyiwa kazi na Wizara imefanikiwa kupata kibali cha kuanzisha Kitengo cha Msaada wa Kisheria katika mwaka

wa fedha 2021/2022. Aidha, mapendekezo mengine yaliyotolewa na bodi yanaendelea kufanyiwa kazi.

39. Mheshimiwa Spika, Katika kuimarisha huduma za msaada wa kisheria, Wizara iliwezesha Wasajili Wasaidizi kukagua utendaji wa Watoa huduma za msaada wa kisheria katika mikoa 26 Tanzania Bara, lengo ni kuhakiki ubora wa utendaji wa watoa huduma hao. Zoezi hili limewezesha kutambua watoa huduma ya msaada wa kisheria waliopo katika kila Halmashauri na utendaji kazi wake ikiwemo kutoa huduma kwa kuzingatia matakwa ya sheria.

IX. Kuratibu shughuli za Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu, Ufilisi na Udhamini;

40. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Wizara kupitia Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu iliimarisha shughuli za usajili wa vizazi, vifo, ndoa, talaka na watoto wa kuasili ikiwa ni haki ya msingi ya utambuzi na upatikanaji wa takwimu kwa ajili ya maendeleo ya Taifa. Ofisi ilitekeleza Mpango Wa Usajili wa Watoto wa Umri Chini ya Miaka Mitano katika Mikoa ya Mwanza, Rukwa na Katavi pamoja na Mpango wa Usajili wa Watoto wenye Umri wa Miaka 5 Hadi 17 walio Shuleni katika wilaya za Mlele, Arumeru, Kahama, Arusha na Misungwi. Hadi kufikia Machi, 2022 jumla ya vizazi 1,173,752 vilisajiliwa.

41. Mheshimiwa Spika, maboresho ya Mfumo wa Usajili wa Matukio ya Vifo yenye lengo la kuhakikisha kila tukio la kifo linasajiliwa mara tu linapotokea, kumpunguzia mwananchi gharama za kupata huduma hiyo pamoja na kupata takwimu za sababu za vifo ili kuweka afua katika huduma za afya, yalifanyika katika Mkoa wa Songwe katika ngazi ya Vituo vya Afya na Ofisi za Kata. Hadi kufikia Machi, 2022 vituo vya usajili vimeongezeka kutoka vituo vinne (4) ambavyo ni wilaya hadi kufikia vituo 130 ambavyo ni Ofisi za Kata 93 na Vituo vya Afya 37 katika Mkoa huo. Jitihada hizo zimewezesha kusajili jumla ya vifo 25,743 katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022.

42. Mheshimiwa Spika, Katika cha kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Ofisi ya Kabidhi Wasi Mkuu ilisajili ndoa 26,303 na talaka 303. Katika jitihada za kuboresha usajili wa matukio hayo, Mfumo wa Usajili wa Ndoa na Talaka kielektroniki umeanzishwa kwa lengo la kurahisisha usajili na upatikanaji wa taarifa hizo nchini. Aidha, mfumo huo umeunganishwa na mfumo wa kielektroniki wa Mashauri wa Mahakama ili kurahisisha upatikanaji na uhakiki wa amri za mahakama kuhusu mashauri yanayohusu talaka. Sambamba na maboresho hayo ya kinfumo, mafunzo kuhusu ufungishaji ndoa yalitolewa kwa Viongozi wa Dini na Serikali katika Mikoa ya Pwani, Kilimanjaro, Iringa, Rukwa na Katavi.

43. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 hati za kuasili watoto 24 zilisajiliwa pamoja na wosia 127 zilitayarishwa na kuhifadhiwa. Elimu kuhusu uandikaji na uhifadhi wa wosia ilitolewa Mkoani Dar es Salaam, Kilimanjaro, Rukwa na Katavi kwa Viongozi wa dini na Serikali. Aidha, elimu ilitolewa kwa wananchi katika maadhimisho ya Wiki ya Wajane mkoani Kagera na Dar es Salaam; na Mkoani Mbeya katika maadhimisho ya Wiki ya Msaada wa Kisheria.

44. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Ofisi ya Kabidhi Wasi Mkuu katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 imesajili Bodi za Wadhamini 90. Ili kuboresha huduma na upatikanaji wa taarifa za Bodi za Wadhamini, Ofisi imeanzisha Mfumo wa kielektroniki wa Usajili wa Bodi za Wadhamini ambao unasaidia upatikanaji na uhakiki wa taarifa za Bodi za Wadhamini kwa wakati pamoja na utoaji vibali vya umiliki ardhi hivyo kurahisisha utoaji huduma na kuongeza maduhuli ya Serikali.

X.Kuratibu Tathmini na Maboresho ya Sheria

45.Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria ilihakikisha sheria za nchi zinafanyiwa mapitio na maboresho ili ziendane na wakati kwa kuzingatia mabadiliko ya maendeleo katika nyanja za kijamii, kiuchumi, kisiasa na

kiutamaduni. Katika kipindi husika Tume ya Kurekebisha Sheria imekamilisha Taarifa kuhusu Mapitio ya Mfumo wa Sheria zinazosimamia Masoko ya Mazao ya Kilimo Tanzania ambapo utafiti ulifanyika katika Mikoa tisa (9) ya Dodoma, Morogoro, Dar es Salaam, Mtwara, Arusha, Kilimanjaro, Mwanza, Iringa na Njombe. Lengo la utafiti huo lilikuwa kubaini changamoto za mfumo wa masoko ya mazao ya kilimo Tanzania na kutoa mapendekezo yatakayohakikisha kunakuwepo mfumo thabiti na endelevu wa masoko ya mazao ya kilimo nchini.

46. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria ilifanya Mapitio ya Mfumo wa Sheria unaosimamia Vyama vya Kijamii ambapo utafiti ulifanyika katika Mikoa saba (7) ya Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Mbeya, Morogoro, Mwanza na Shinyanga. Lengo la utafiti huo ni kubaini changamoto za Mfumo wa Sheria unaosimamia vyama vya kijamii na kutoa mapendekezo yatakayohakikisha kunakuwepo na mfumo thabiti wenye uwazi na uwajibikaji.

47. Mheshimiwa Spika, Kuhusu tathmini ya utekelezaji wa sheria, Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria ilikamilisha Taarifa nne (04) za tathmini ya utekelezaji wa sheria ambazo zinahusu mifumo ya Adhabu Mbadala; Sekta ya Utalii, Sekta ya Mifugo na Sekta ya Uvuvi. Kwa upande wa Adhabu Mbadala, sheria zilizofanyiwa tathmini ni pamoja na Sheria ya Magereza, Sura 58; Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura 20; Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi, Sura 200, Sheria ya Huduma za Jamii, Sura 291; Sheria ya Bodi ya Msamaha, Sura ya 400 na Sheria Ukomo wa Adhabu, Sura 90. Lengo la tathmini ni kupima endapo malengo ya sheria husika yamefikwa ikiwemo kupunguza msongamano wa Wafungwa Magerezani, kupunguza adha ya kupata magonjwa ya kuambukiza kwa Wafungwa na kuipunguzia Serikali gharama za kuendesha magereza.

48. Mheshimiwa Spika, Katika Sekta ya Utalii, sheria zilizofanyiwa tathmini ni pamoja na Sheria ya Utalii, Sura 65; Sheria ya Wanyamapori, Sura 283; Sheria ya Mbuga za Wanyama, Sura 282; Sheria ya Makumbusho ya Taifa, Sura 281; Sheria ya Hifadhi ya Eneo la Mamlaka ya Ngorogoro,

Sura 284; na Sheria ya Malikale, Sura 333. Tathmini katika Sekta ya Utalii ililenga kubaini endapo madhumuni yaliyokusudiwa na Sheria hizo yamefikiwa katika kuboresha na kukuza vivutio vya utalii, kuboresha kipato cha wananchi, kuongeza fedha za kigeni na kuongeza pato la Taifa. Aidha, Tume ilifanya tathmini ya utekelezaji wa sheria katika Sekta ya Mifugo. Sheria zilizofanyiwa tathmini ni pamoja na Sheria ya magonjwa ya Mifugo, Sura 156; Sheria ya Madaktari wa Mifugo, Sura 319; Sheria ya Nyama, Sura 421; Sheria ya Maziwa, Sura 262; Sheria ya Biashara ya ngozi, Sura 120; Sheria ya Ustawi wa Wanyama, Sura 120; Sheria ya Utambulisho, Usajili na Ufuatiliaji wa Wanyama, Sura 184; Sheria ya Matumizi ya Ardhi, Sura 116 na Sheria ya Nyanda za Malisho na Rasilmali za Vyakula vya Mifugo, Sura 180. Dhumuni la tathmini ya sheria zinazosimamia sekta ya mifugo ni kupima endapo malengo yaliyokusudiwa katika sheria hizo yamefikiwa katika kuhakikisha ufugaji unakuwa wa kibiashara na wenye tija kwa wafugaji na Taifa kwa ujumla.

49. Mheshimiwa Spika, Kuhusu tathmini ya utekelezaji wa Sheria zinazosimamia Sekta ya Uvuvi Tanzania, Sheria zilizofanyiwa tathmini ni pamoja na Sheria ya Uvuvi, Sura 279; Sheria ya Usimamizi na Maendeleo ya Uvuvi wa Bahari kuu, Sura 388; Sheria ya Hifadhi za Bahari na maeneo Tengefu, Sura 146; na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania, Sura 280. Dhumuni la tathmini ya sheria zinazosimamia Sekta ya Uvuvi Tanzania ni kupima kufikiwa kwa malengo ya sheria hizo ya kuhakikisha kuwa Sekta ya Uvuvi inakuwa ya kibiashara na kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa buluu wenye kuboresha maisha ya wananchi na kukuza Pato la Taifa.

50. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria ilitoa elimu ya sheria kwa umma kupitia vipindi vya radio, runinga, vipeperushi, maonesho ya wiki ya sheria, na mikutano mbalimbali. Lengo lilikuwa kuongeza uelewa kwa jamii kuhusu Sheria ya Mtoto; Sheria ya Ajira; Sheria ya utatuzi wa Migogoro ya Ardhi; Sheria ya Haki za Walaji na nafasi ya Tume katika maboresho ya sheria nchini. Taarifa za tathmini

hizo zitawasilishwa kwenye mamlaka husika kwa hatua zaidi.

XI. Kuratibu ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sheria za Utajiri na Maliasilia za nchi

51. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za utajiri asilia na maliasilia za nchi kwa kuandaa Mfumo wa Kielektroniki utakaowezesha; kukusanya taarifa zinazobainisha sehemu zenye utajiri na Maliasili za Nchi na aina ya uwekezaji unaofanyika, kusajili mikataba ya utajiri na Maliasilia za Nchi iliyoingwiwa na Wizara, Idara na Taasisi kwa niaba ya Serikali na kupata taarifa za utekelezaji wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi na Umiliki wa Utajiri na Maliasilia za Nchi Sura 449 na Sheria ya Mapitio na Majadiliano Kuhusu Mikataba yenye Masharti Hasi Sura 450 kutoka kwa Wizara, Idara na Taasisi zinazosimamia utajiri asilia na maliasilia za nchi. Aidha, Wizara imeshiriki katika kutoa mafunzo na elimu kwa wadau mbalimbali wanaohusika na masuala ya utajiri asilia na maliasilia za nchi kwa Maafisa wa Serikali 260 kuhusu Sheria ya Mamlaka ya Nchi na Umiliki wa Utajiri na Maliasilia za Nchi Sura 449 na Sheria ya Mapitio na Majadiliano Kuhusu Mikataba yenye Masharti Hasi Sura 450 na nafasi ya maafisa wanyamapori katika kulinda na kuhifadhi wanyamapori kwa mujibu wa sheria hizo. Wizara imesimamia jukumu la kufanya marekebisho ya Kanuni za ushiriki wa Serikali katika shughuli za uchimbaji wa madini nchini kwa mujibu wa kifungu cha 10 cha Sheria ya Madini, 2010. Wizara imeshiriki katika majadiliano na makampuni ya uchimbaji wa madini za Nyanzaga.

52. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kushiriki kuweka mifumo mbalimbali ili kuhakikisha kwamba utajiri na maliasilia za nchi unasaidia kuinua uchumi wa nchi na wananchi kwa ujumla. Wizara inashirikiana na Wizara mbalimbali kuandaa sera na miongozo mbalimbali ambapo katika kipindi husika imeshirikiana na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kuandaa Sera ya ushiriki wa wananchi katika miradi ya kimkakati (Local Content) pamoja na Sera ya uwekezaji.

XII. Kuboresha Utendaji na Maendeleo ya Rasilimali Watu iliyo chini ya Wizara

53. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Wizara imeendelea kusimamia na kuboresha maslahi ya watumishi na utendaji kazi katika kutekeleza majukumu yake. Katika kipindi hicho Wizara ya Katiba na Sheria iliajiri mtumishi mpya mmoja (1) na watumishi wawili (2) walipandishwa vyeo. Aidha, kwa upande wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, zimeendelea kusimamia maendeleo ya rasilimaliwatu kama ifuatavyo: -

i. Tume ya Utumishi wa Mahakama iliajiri jumla ya watumishi 45 wa kada mbalimbali kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 ikilinganishwa na idadi ya ajira ya watumishi 239 wa kada mbalimbali kwa kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021. Vilevile, vikao vinne (4) vilifanyika kushughulikia masuala mbalimbali ikiwemo Uteuzi wa Naibu Wasajili 25 wa Mahakama Kuu ya Tanzania kwa ajili ya kuimarisha utendaji wa Mahakama; Kushughulikia mashauri 21 ya kinidhamu ambapo Mahakimu saba (7) walistaafishwa kwa manufaa ya umma; watumishi watano (5) wasio Mahakimu walifukuzwa kazi na Mahakimu tisa (9) walirejeshwa kazini. Aidha, mtumishi mmoja (1) wa Sekretarieti ya Tume alipandishwa cheo na mtumishi mmoja (1) aliteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimaliwatu;

ii. Ofisi ya Taifa ya mashtaka iliajiri watumishi wapya wanne (4), mtumishi mmoja (1) alithibitishwa kazini na watumishi 19 walipandishwa vyeo;

iii. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliajiri watumishi wapya wawili (2), watumishi wawili (2) walithibitishwa kazini, mtumishi mmoja (1) alipandishwa cheo;

iv. Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliajiri watumishi wapya 23, watumishi 8 walithibitishwa cheo na mtumishi mmoja (1) alipandishwa cheo;

v. Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iliajiri watumishi wapya watano (5), watumishi wawili (2) walithibitishwa vyeo na watumishi wawili (2) walipata uteuzi kuwa Katibu Mtendaji na Naibu Katibu Mtendaji;

vi. Chuo cha uongozi wa Mahakama Lushoto kiliajiri watumishi wapya wawili (2), mtumishi mmoja (1) alithibitishwa cheo na mtumishi mmoja (1) alipata uteuzi kuwa Mkuu wa Idara ya Mafunzo ya Sheria;

vii. Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania kilipandisha cheo watumishi tisa (9); na

viii. Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu ili wathibitisha vyeo watumishi sitini na saba (67), watumishi watatu (3) walipandishwa vyeo, watumishi wawili (2) walisimamishwa kazi na watumishi watatu (3) waliteuliwa katika nyadhifa za Kabidhi Wasii Mkuu, Naibu Kabidhi Wasii Mkuu na Meneja wa Usajili.

54. Mheshimiwa Spika, jumla ya watumishi 1,579 kwa Wizara na Taasisi zake walipatiwa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi. Maelezo ya kina kuhusu maendeleo ya Rasilimaliwatu yameoneshwa katika Kiambatisho F.

XIII. Kushughulikia urejeshwaji wa wahalifu na masuala ya ushirikiano wa kimataifa kwenye makosa ya jinai

55. Mheshimiwa Spika, Tanzania imeendelea kushirikiana na mataifa mengine katika kupambana na kusimamia kurejeshwa kwa watuhumiwa wa uhalifu katika nchi walikofanya kosa. Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa mkataba wa urejeshwaji wa Wahalifu na ushirikiano katika masuala ya mashauri ya jinai baina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kenya. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Wizara ilipokea na kushughulikia maombi matano (5) ya kuwarejesha wahalifu wa makosa ya jinai waliokimbilia nchini kutoka katika mataifa ya Zimbabwe (2), Malawi (1), Uturuki (1) na Kenya (1). Lengo la kurejesha waharifu hao ni kuimarisha ushirikiano wa kisheria na mataifa mengine katika masuala ya jinai na

kudhibiti watuhumiwa wa uhalifu kukimbilia katika mataifa mengine.

XIV. Kuratibu shughuli za Taasisi, Mipango na Miradi chini ya Wizara

(a) Kuimarisha Uendeshaji wa Mafunzo Endelevu na Elekezi ya Kimahakama na Kisheria

56. Mheshimiwa Spika, Katika kuhakikisha watumishi wa Mahakama na wa sekta ya sheria wanakuwa na ujuzi na weledi wa kutosha katika kutimiza wajibu wao kwa ufanisi, Wizara kupitia Chuo cha Uongozi wa Mahakama, Lushoto imeendelea kuratibu na kutoa mafunzo endelevu na elekezi ya Kimahakama kwa watumishi wa Mahakama na wadau wa sekta ya sheria nchini. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 Chuo kimeratibu mafunzo yafuatayo;

(i) Mafunzo endelevu: Wizara kupitia Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto imeendelea kuwajengea uwezo jumla ya wasaidizi wa sheria wa Majaji 84 kwenye eneo la kufanya utafiti wa kisheria ili waweze kuwasaidia majaji ipasavyo katika kutoa haki. Vilevile, jumla ya Mahakimu 200 walipatiwa mafunzo kuhusu uendeshaji wa mashauri ya rushwa na urejeshaji mali zilizopatikana kwa njia ya uhalifu na Mahakimu 36 walipatiwa mafunzo kuhusu uendeshaji wa mashauri yanayohusu ukatili wa kijinsia, na usafirishaji haramu wa binadamu. Chuo kwa kushirikiana na Mahakama kimekuwa kikiendesha mafunzo kwa njia ya mtandao kwa lengo la kuwafikia watumishi wengi na kutoa fursa ya kubadilishana uzoefu. Katika kipindi husika jumla ya Mahakimu 100 waliokasimiwa mamlaka ya ziada na Jaji Mkuu ya kusikiliza mashauri ambayo yanaangukia kwenye mamlaka ya Mahakama Kuu ya Tanzania walipatiwa mafunzo endelevu na kupata fursa ya kubadilishana uzoefu wa namna mamlaka hayo yanavyotumika pamoja na kujadili changamoto na namna ya kuboresha usikilizaji wa mashauri. Aidha, Chuo kiliratibu mafunzo kwa njia ya mtandao kwa majaji, wasajili na Mahakimu wengine wa ngazi mbalimbali

wapatao 150 yaliyolenga utekelezaji wa sheria ya wosia na usimamizi wa mirathi pamoja na kubadilishana uzoefu.

(ii) Mafunzo elekezi: Wizara kupitia Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto iliendelea kutoa mafunzo elekezi kwa Mahakimu wapya 35, Manaibu Wasajili wapya 25, Watendaji wa Mahakama wa kanda na mikoa wapya 11 pamoja na Wakurugenzi wasaidizi watatu 3, mafunzo ya udalali wa mahakama kwa washiriki 30 na wasambazaji nyaraka za Mahakama 16. Katika kipindi husika chuo kwa kushirikina na Mahakama ya Tanzania kupitia ufadhili wa Shirika la UNICEF kiliendesha Mafunzo kwa Wadau wa Haki Mtoto Kanda ya Kigoma wapatao 40 waliojumuisha Mahakimu 15 kutoka Mahakama Kuu Kanda ya Kigoma, Mahakimu 15 kutoka kanda ya Tabora, Maafisa Ustawi wa Jamii watano (5), Waendesha Mashtaka watatu (3) kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Waendesha Mashtaka wawili (2) kutoka jeshi la Polisi. Mahakimu walioshiriki ni wale wenye mamlaka ya kusikiliza mashauri ya mtoto kutoka Mahakama za wilaya na baadhi ya mahakimu wa Mahakama za mwanzo kutoka kanda zilizotajwa.

57. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai, 2021 mpaka Machi, 2022, Wizara kupitia Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto imeratibu ushiriki wa maafisa mbalimbali kutoka Mahakama ya Tanzania na Chuo kwenye vikao na mafunzo yaliyoendeshwa na wadau kama ifuatavyo:-

(i). Mkutano wa wadau (High Level symposium) wa utoaji haki jinai na ulinzi kwa mashahidi, wahanga na washtakiwa ulioendeshwa na Mahakama ya Tanzania kwa kushirikiana na Mahakama ya Uingereza kupitia Taasisi ya Majaji Wastaafu iitwayo Slynn Foundation chini ya ufadhili wa Programu ya Kitaifa ya Kuzijengea Uwezo Taasisi zinazohusika na Kupambana na Rushwa (BSAAT).

(ii). Mafunzo juu ya Uelewa wa utendaji kazi wa Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki, Utawala wa sheria na Utawala bora. Mafunzo haya yaliendeshwa na Mahakama ya Haki ya

Afrika Mashariki kwa kushirikiana na Centre for Public Interest Law na Ford Foundation kwa majaji wa mahakama ya Rufani watatu (3), majaji wa mahakama kuu watatu (3) na Naibu Wasajili saba (7).

58. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa masomo 2021/22 Chuo kimedahili wanafunzi wapya 870 wa Astashahada na Stashahada ya sheria (wanawake 412 na wanaume 458). Kwa upande wa Astashahada ya sheria waliidahiliwa ni 492 (wanawake 224 na wanaume 268) na Stashahada ya sheria mwaka wa kwanza ni 378 (wanawake 188 na wanaume 190). Aidha, wanachuo wanaoendelea na Stashahada mwaka wa pili ni 231 (wanawake 137 na wanaume 94). Jumla ya wanafunzi wote wa Chuo waliidahiliwa katika Astashahada na Stashahada ya sheria kwa mwaka wa masomo 2021/2022 ni 1,101 (wanawake 549 na wanaume 552) ikilinganishwa na udahili wa jumla ya wanafunzi 944 (wanaume 420 na wanawake 524) katika mwaka wa masomo 2020/2021 sawa na ongezo la asilimia 17.

59. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto imeendelea kusimamia haki za mtoto kwa kuandaa na kuzindua Kitabu cha Mkusanyiko wa Mashauri ya Watoto na Taarifa ya Tathmini ya Mafunzo ya Haki za Watoto kwa wadau wa haki za Watoto kwa ajili ya kurahisha rejea kuhusu mwenendo wa mashauri ya watoto.

(b) Kuimarisha Uendeshaji na Usimamizi wa Utoaji wa Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo

60. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kutoa mafunzo ya uanasheria kwa vitendo. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Taasisi imedahili jumla ya wanafunzi 1,507 sawa na ongezeko la asilimia 0.5 ya lengo la udahili wa wanafunzi 1,500. Aidha, katika kipindi husika, Taasisi imetunuku vyeti kwa wahitimu 293 wanaostahili kusajiliwa kuwa mawakili na kufanya idadi ya wahitimu waliopata mafunzo kupitia Taasisi hiyo tangu kuanzishwa kwake mwaka 2007 kufikia 7,561.

(c) Miradi ya Maendeleo Inayotekelezwa na Wizara

61. Mheshimiwa Spika, Wizara na Taasisi zake imeendelea kubuni na kutekeleza miradi ya maendeleo ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 Wizara na Taasisi zake imeendelea kutekeleza miradi ifuatayo:

i. Mradi wa Kujenga Mfumo Endelevu wa Kupambana na Rushwa.

Mradi huu una lengo la kupunguza athari za rushwa ambazo ni kikwazo cha maendeleo na kupambana na umaskini nchini. Mradi huu unatekelezwa na Wizara ya katiba na Sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mahakama ya Tanzania na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka. Kazi zilizofanyika katika kipindi hicho ni pamoja na kutoa mafunzo kwa Mahakimu Wakazi 200 kuhusu uendeshaji wa mashauri ya rushwa na urejeshwaji mali; kuandaa Rasimu ya Mwongozo wa Upelelezi na Uendeshaji wa Mashauri ya Rushwa na mashauri mengine (Standard Operating Procedures – SOPs); kufanya mapitio ya majalada 55 ya mashauri ya rushwa kwa Wakuu wa Mashitaka wa Mikoa mitano (5) ya Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Mbeya na Mwanza kwa lengo la kuwajengea uwezo kwa vitendo na kuimarisha mifumo ya kupambana na rushwa; na kufanya ufuatiliaji na tathmini za Programu ya Kujenga Mfumo Endelevu wa Kupambana na Rushwa Tanzania.

ii. Mradi wa Haki Mtandao (e-Justice).

Mradi huu unalenga kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za kisheria na upatikanaji haki. Aidha, mradi huu unalenga kuunganisha mifumo ya taasisi za utoaji haki kwa njia za kielektroniki ili kuongeza ufanisi, kuharakisha upatinaji wa haki na kupunguza gharama za upatikanaji wa huduma hizo. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 mradi umetekeleza kazi ya usanifu wa mfumo wa kielektroniki wa uangalizi na usimamizi wa utajiri wa maliasilia za nchi. Mfumo huu utawezesha usajili wa Mikataba iliyoingwiwa na

taasisi za Serikali, utambuzi wa maliasilia zote nchini na uwekezaji uliofanyika.

iii. Mradi wa Kuboresha Uwajibikaji wa Kitaasisi katika kupambana na Rushwa na kuongeza Wigo wa Kuifikia Haki.

Lengo la mradi huu ni kuimarisha mazingira ya wananchi kuifikia haki hususan wanawake na watoto pamoja na kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa. Kazi zilizofanyika katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022 ni pamoja na: Kuwezesha utoaji wa huduma ya Msaada wa kisheria ambapo katika maadhimisho ya Wiki ya Msaada wa Kisheria yaliyofanyika nchi nzima jumla ya wananchi 1,455,566 (wanawake 529,079, wanaume 514,051 na watoto 412,436) walipatiwa huduma ya msaada wa kisheria.

iv. Mradi wa kisekta unaofadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto.

Mradi huu unatekeleza Mkakati wa Haki Mtoto wa mwaka 2020/2021 - 2024/2025 pamoja na kuimarisha usajili wa matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu, hususan usajili wa vizazi. Kazi zilizofanyika ni pamoja na Kusajili Vizazi kwa jumla ya watoto 573,888 kupitia Mpango wa Usajili wa Watoto wa Umri Chini ya Miaka Mitano, katika Mkoa ya Mwanza, Rukwa na Katavi na usajili wa vifo 480 katika Mkoa wa Songwe.

v. Mradi wa Uimarishaji wa Upatikanaji Haki za Kisheria Ulinzi wa Haki za Binadamu Tanzania.

Mradi huu unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP). Mradi huu unalenga kuimarisha uwezo wa taasisi za Umma na Asasi za Kiraia (AZAKI) katika kulinda na kutetea haki za binadamu. Kupitia mradi huu Katika eneo la uchunguzi, Tume ilifanya chunguzi maalum tano (5) kuhusu migogoro wa ardhi, matumizi mabaya ya madaraka na mazingira mkoani Dodoma, Morogoro, Tabora, Shinyanga na Manyara. Uchunguzi wa malalamiko haya unaendelea. Kupitia chunguzi hizi, Tume imeweza kusaidia wananchi

kutatua kero zinazowakabili na kuzishauri mamlaka za Serikali namna ya kuzingatia masuala ya utawala bora.

vi. Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za Taasisi zilizokuwa Chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Katika kipindi husika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekamilisha taratibu za awali za ujenzi wa Ofisi Jumishi katika mkoa wa Mwanza, ambapo mkandarasi ameshapatikana na ujenzi unatarajiwa kuanza mwezi Juni 2022.

62. Mheshimiwa Spika, Mchanganuo wa fedha za Miradi ya Maendeleo zilizopitishwa katika mwaka wa fedha 2021/2022 na kupokelewa na Wizara na Taasisi katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 umeambatishwa kwenye **KIAMBATISHO G.**

E. UTEKELEZAJI WA ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI YA MWAKA 2020 HADI MWAKA 2025

63. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutekeleza azma ya Serikali ya Awamu ya sita ya kuhakikisha kwamba inawajibika ipasavyo kwa wananchi kupitia utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, ahadi na maelekezo mbalimbali ya viongozi wa kitaifa. Miongoni mwa ahadi hizo ni pamoja na kuendeleza vita dhidi ya rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma; kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na kuendeleza utawala wa sheria; na kuimarisha mfumo wa utoaji haki. Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022 Wizara katika utekelezaji wa majukumu yake imetekeleza maelekezo mbalimbali ya Ilani ikiwa ni pamoja na yafuatayo:

I. Kuendeleza Mapambano Dhidi ya Rushwa na Ubadhirifu wa Mali ya Umma

64. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Wizara imechukua hatua mbalimbali za kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa na ubadhirifu wa

mali ya umma. Hatua hizo ni pamoja na kuimarisha uwezo wa Mahakama ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi kusikiliza mashauri yanayohusu makosa hayo. Kwa kipindi cha Julai 2021- Machi, 2022 kulikuwa na Jumla ya mashauri 46. Kati ya mashauri hayo, 21 yalikuwepo mwanzoni mwa Julai 2021 na mashauri mapya 25 yalifunguliwa katika mahakama hiyo. Hadi Machi, 2022 mashauri 20 yamehitimishwa na mashauri 26 yanaendelea kusikilizwa.

II. Kuchukua Hatua za Kupunguza Mlundikano wa Mashauri Mahakamani

65. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi kufikia Machi, 2022, Mlundikano wa mashauri umepungua kwa asilimia 26 kutoka mashauri 9,399 mwezi Machi 2021 hadi Mashauri 6,994 mwezi Machi, 2022. Hatua zilizochukuliwa ili kupunguza mlundikano wa mashauri ni pamoja na kufuta mashauri yasiyokuwa na ushahidi; kutumia mfumo wa kumaliza mashauri kwa njia ya makubaliano na majadiliano (plea bargaining); kuimarisha mfumo wa ufifishaji wa makosa; kutumia mahakama zinazotembea na mikutano mtandao (video conference) katika kuendesha mashauri; na kutekeleza mkakati wa kumaliza mashauri ya muda mrefu.

III. Kuhakikisha Huduma Bora za Sheria Zinapatikana Kwa Wakati na Gharama Nafuu kwa Kuongeza Wataalam, Miundombinu, Vitendea Kazi na Kusogeza Huduma Karibu na Wananchi

66. Mheshimiwa Spika, Jumla ya Mahakama za Mwanzo tatu (3) zilikamilika katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2021 hadi Machi, 2022 ambazo ni za matiri (Mbinga), Hydrom (Mbulu) na Kibaigwa (Kongwa). Vilevile, mahakama inaendelea na ujenzi wa mahakama za mwanzo katika maeneo ya Mlimba na Mang'ula (Morogoro) Chanika (Dar es Salaam), Kabanga (Ngara), Nyakibimbiri (Bukoba) na Kimbe (Kilindi). Mahakama inaendelea na Mpango wa ujenzi wa Mahakama za Mwanzo 60 katika Kata ambazo zipo Makao Makuu ya Tarafa ili kusogeza huduma ya utoaji haki karibu na Wananchi.

IV. Kuimarisha Mfumo wa Wasajili Wasaidizi Katika Halmashauri zote Ili Kuwezesha Uratibu na Utoaji wa Msaada wa Kisheria Kwa Wananchi, Ikiwemo Msaada Wa Huduma za Kisheria Katika Masuala ya Mirathi na Ndoa.

67. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 Wizara imezindua Kamati za Uratibu wa Wadau wa Msaada wa Kisheria katika mikoa ya Katavi, Mtwara, Dar es Salaam, Mara, Mbeya, Ruvuma, Lindi, Manyara, Mwanza na Mbeya na hivyo kufanya jumla ya mikoa 18 kuwa na kamati za uratibu wa masuala ya huduma za msaada wa kisheria. Kamati hizi zinarahisisha upatikanaji wa watoa huduma kwani wadau wote wa msaada wa kisheria wanakutana na hivyo kuimarisha ushirikiano katika kutekleza majukumu yao.

V. Kuimarisha Matumizi ya Lugha ya Kiswahili Katika Kutoa Huduma za Kimahakama na Kwenye Uandishi wa Nyaraka za Kisheria

68. Mheshimiwa Spika, Idadi ya Sheria kuu zilizokamilika kutafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza kuwa Kiswahili hadi kufikia Machi, 2022 ni 212 ambazo zilitafsiriwa kupata Rasimu ya Kwanza. Aidha, kupitia wasaidizi wa kisheria na watoa huduma za msaada wa kisheria, elimu kwa jamii kwa lugha ya Kiswahili na lugha za maeneo mahsusi imeendelea kutolewa kwa lengo la kujenga uelewa zaidi kwa jamii katika masuala mbalimbali ya kisheria. Lengo ni kuwezesha wananchi kusimamia na kulinda haki zao kwa kufahamu sheria.

VI. Kujenga Mifumo ya TEHAMA ya Kuendelea Kuhimiza Matumizi yake Katika Utoaji Haki

68. Mheshimiwa Spika, Wizara pamoja na taasisi sita (6) ambazo ni (Mahakama, Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu), Tume

ya Utumishi wa Mahakama, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali) kati ya Taasisi 10 vimeimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji haki ikiwemo wananchi kuweza kufungua na kufuatilia malalamiko; kuwasilisha maombi ya nyongeza ya muda, usajili wa waendesha maridhiano, majadiliano, usuluhishi na upatanishi; kuwezesha kufungua mashauri kwa njia ya kielektroniki; kusajili vizazi, vifo na bodi za wadhamini kielektroniki; kusajili, kutambua na kusimamia madalali wa Mahakama na kutoa mrejesho wa huduma zitolewazo na Mahakama kupitia simu janja.

F. MWENENDO WA BAJETI NA FEDHA ZILIZOPOKELEWA NA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

(i) Makusanyo ya Maduhuli

69. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara ilipanga kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 12,672,599,000.00** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato ambavyo ni pamoja na; ada za watoa huduma ya utatuzi wa migogoro kwa njia ya majadiliano, maridhiano, upatanishi na usuluhishi; ada za watoa huduma ya msaada wa kisheria; ada za kusajili mashauri, ada za mawakili na faini zinazotokana na mashauri mbalimbali pamoja na pango la ofisi. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 Wizara ilikusanya jumla ya **Shilingi 6,018,450,524.81** sawa na asilimia 47 ya lengo la makusanyo yaliyopangwa. Mchanganuo wa maduhuli kwa kila Fungu ni kama unavyoonekana kwenye Jedwali Na. 1.

JEDWALI Na. 1 Mchanganuo wa maduhuli yaliyokusanywa kwa kila Fungu kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

| Mafungu | KIASI KILICHODHINISHWA (SH) | KIASI KILICHOKUSANYWA JULAI 2021-MACHI 2022 (SH) |
|--------------|-----------------------------|--|
| Fungu 12 | - | - |
| Fungu 16 | - | - |
| Fungu 19 | - | - |
| Fungu 35 | 56,400,000.00 | 56,400,000.00 |
| Fungu 40 | 12,571,199,000.00 | 5,921,836,129.00 |
| Fungu 41 | 45,000,000.00 | 40,214,395.81 |
| Fungu 55 | - | - |
| Fungu 59 | - | - |
| JUMLA | 12,672,599,000.00 | 6,018,450,524.81 |

(ii) Bajeti Iliyoidhinishwa

71. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara ya Katiba na Sheria iliidhinishwa na Bunge jumla ya **Shilingi 231,693,745,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Miradi ya maendeleo. Kati ya hizo **Shilingi 79,599,030,000** ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi, **Shilingi 99,178,885,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi 52,915,830,000** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za Maendeleo jumla ya **Shilingi 44,100,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 8,815,830,000** fedha za nje.

(iii) Fedha zilizopokelewa na Wizara na Taasisi

72. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 194,115,559,872.30** sawa na asilimia 84 ya **Shilingi 231,693,745,000** zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2021/2022. Kati ya hizo **Shilingi 63,868,833,607.27** ni mishahara na **Shilingi 81,691,778,331.58** ni matumizi mengineyo. Fedha za maendeleo zilizopokelewa ni **Shilingi 49,616,082,804.44** ambazo zinajumuisha **Shilingi 22,135,756,234.90** fedha za ndani na **Shilingi 27,480,326,569.54** ni fedha za nje. Ongezeko la fedha za nje zilizopokelewa limetokana na Mfuko wa Mahakama kupokea kiasi cha **Shilingi 22,901,711,761.54** ambazo zilitokana na Mkataba wa Benki ya Dunia na Serikali ambapo kiasi hicho cha fedha kiliongezeka wakati wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22. Muhtasari wa mchanganuo wa Bajeti iliyoidhinishwa umeoneshwa kwenye Jedwali Na. 2 na kiasi cha fedha zilizopokelewa na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Wizara na Taasisi hadi Machi, 2022 zimeoneshwa kwenye **KIAMBATISHO H.**

JEDWALI: Na. 2: Muhtasari wa Bajeti na Fedha zilizopokelewa kwa Wizara na Taasis kwa Kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi 2022

| Na. | Matumizi | Bajeti iliyoidhinishwa | Kiasi kilichopokelewa Hadi Machi, 2022 | Asilimia ya kiasi kilichopokelewa hadi kufikia Machi, 2022 |
|-----|-----------------------------|------------------------|--|--|
| 1. | Mishahara ya watumishi | 79,599,030,000 | 63,129,965,237 | 79% |
| 2. | Matumizi mengineyo | 99,178,885,000 | 81,369,511,831 | 82% |
| 3. | Miradi ya Maendeleo (Ndani) | 44,100,000,000 | 22,135,756,235 | 50% |
| 4. | Miradi ya Maendeleo (Nje) | 8,815,830,000 | 27,480,326,570 | 312% |
| | JUMLA | 231,693,745,000 | 194,115,559,872 | 84% |

G. MAFANIKIO YALIYOPATIKANA

73. Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022 ulikuwa na mafanikio yafuatayo:-

i. Kuimarisha mfumo wa utoaji haki nchini kwa kuanza kutumia lugha ya Kiswahili katika uandishi wa sheria na shughuli za utoaji haki mahakamani;

ii. Kuongezeka kwa wigo wa mfumo wa utoaji haki kwa kuwawezesha Mawakili kuanza kutoa huduma za uwakili katika Mahakama za Mwanzo; Kuimarisha mfumo wa utatuzi wa migogoro nje ya mahakama kwa kutumia njia mbadala ambazo ni; majadiliano, maridhiano, upatanishi na usuluhishi;

iii. Uteuzi wa Majaji tisa (9) wa Mahakama ya Rufani na Majaji 21 wa Mahakama Kuu na kufanya jumla ya idadi ya Majaji wa Mahakama ya Rufani kufikia 24 na Majaji wa Mahakama Kuu kufikia 82 na Mahakimu 245;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

iv. Uteuzi wa Kabidhi Wasii Mkuu na Naibu Kabidhi Wasii Mkuu na hivyo kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu;

v. Kuendelea na matumizi ya lugha ya Kiswahili katika Shughuli za mahakama na uandishi wa nyaraka za Kisheria ambao umeongeza uelewa wa sheria kwa wananchi na hivyo kurahisisha upatikanaji wa haki kwa wakati na kwa gharama nafuu;

vii. Kuunganishwa kwa Mfumo wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udamini na Mahakama ambapo imerahisisha upatikanaji wa taarifa za talaka na watoto wa kuasili kwa njia ya mtandao;

viii. Tanzania kupitia Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu kuwa kinara wa Usajili wa matukio muhimu ya binadamu katika ukanda wa Afrika kupitia tangazo la Umoja wa Afrika mwaka 2021;

ix. Kuimarika na kuboreshwa kwa utoaji wa mafunzo ya uanasheria kwa vitendo nchini na mafunzo ya uongozi wa mahakama;

x. Kuendelea kuimarika kwa matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma;

xi. Kuiwakilisha Serikali katika mashauri ya madai na usuluhishi kulikowezesha kuokoa kiasi cha Shilingi bilioni 236.6; na

xii. Kutoa taarifa kwa nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa na Ulimwengu kwa ujumla kuhusu jitihada za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kukuza, kuheshimu na kulinda haki za kisiasa, kiraia, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii.

H. CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA

74. Mheshimiwa Spika, Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu, Wizara ilikabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo: -

- i. Kukosekana kwa ulinzi na usalama kwa watoa taarifa na mashahidi. Hali hii inasababisha watoa taarifa na mashahidi kusita au kutokutoa ushirikiano unaohitajika kwa vyombo vya haki jinai katika kutoa taarifa za uhalifu kwa kuhofia usalama wao;
- ii. Kuongezeka kwa uhitaji wa Wananchi kuelewa wajibu wao katika kudai haki zao za kijamii na kiraia ikilinganishwa na uwezo uliopo;
- iii. Mirathi kuchukua muda mrefu kufungwa kutokana na wanufaika kuendeleza migogoro hata baada ya Mahakama kumteua Kabidhi Wasii Mkuu kuwa msimamizi wa mirathi;
- iv. Kuwepo kwa migogoro ndani ya Bodi za Wadhamini za Taasisi zisizo za Serikali zilizosajiliwa na Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu inayotokana na kugombania madaraka, maslahi binafsi na ubadhillifu wa mali; na
- v. Kutofungamanishwa kwa mfumo wa utoaji haki kunakoathiri upatikanaji wa haki, uendeshaji na usimamizi wa vyombo vingine vya utoaji haki.

I. MIKAKATI YA KUTATUA CHANGAMOTO

75. Mheshimiwa Spika, ili kutatua changamoto zilizotajwa hapo juu Wizara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

- (i) Wizara inaratibu maandalizi ya kanuni za kutekeleza Sheria ya Kuwalinda mashahidi na Watoa taarifa za Uhalifu nchini;
- (ii) Kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu katiba na Sheria kupitia vyombo mbalimbali vya habari ikiwa ni pamoja kushirikisha Asasi za Kiraia ili kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu haki na wajibu wao katika kupata haki zao.
- (iii) Kutoa elimu kwa wanufaika kuhusu taratibu za usimamizi na ufungaji ili mirathi iweze kufungwa kwa wakati na warithi kupata haki zao.

(iv) Kuendelea kuhakikisha taasisi zilizosajiliwa zinaweka vipengele bayana katika katiba zake vitakavyotoa miongozo ya kuepusha migogoro katika Bodi za Wadhamini na kuendelea kutoa elimu kuhusu majukumu na wajibu wa Bodi za Wadhamini; na

(v) Kuendelea kuboresha na kufungamanisha mifumo ya utoaji haki kwa vyombo vya utoaji haki nchini.

76. Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana ni juhudi za pamoja kati ya Wizara, Idara, Taasisi na wadau wa Sekta ya Sheria wakiwemo washirika wa maendeleo. Hivyo, nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa ushirikiano mzuri uliopo kati yetu na Washirika wa Maendeleo ikiwa ni pamoja na Benki ya Dunia, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Shirika la Umoja wa Mataifa la Wanawake (UNWOMEN), Umoja wa Ulaya (EU), Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Uingereza (FCDO), Mahakama ya Uingereza, Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki. Wadau wengine walioshiriki katika kuleta mafanikio ya Wizara ni pamoja na; Kampuni ya Simu ya TIGO ambayo imeipatia Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu simu janja 1,046 kwa ajili ya usajili wa watoto chini ya umri wa miaka mitano (5) katika mikoa mitatu (3) ya Mwanza, Rukwa na Katavi na hivyo kufanya jumla ya mikoa iliyopokea simu janja kwa ajili ya shughuli za usajili kufikia 22. Ni matumaini yangu kuwa, Kampuni hiyo itaendelea kuipatia simu janja mikoa minne (4) iliyobaki ya Tabora, Kigoma, Kagera na Dar es Salaam kufanikisha usajili wa watoto. Wizara inatambua na kuthamini uhusiano mzuri uliopo kati ya Serikali na wadau hao, na tutahakikisha kuwa ushirikiano huo unaimarishwa kwa maendeleo ya sekta ya sheria na taifa kwa ujumla.

J. MPANGO NA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

77. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara na Taasisi zake itaendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa umma ili kuendana na Dhima yake. Ili kufikia

azma hiyo Wizara na Taasisi zake zimeainisha maeneo mahsusi ya kipaumbele na kuyawekea malengo na shabaha kwa ajili ya utekelezaji.

(a) Vipaumbele vya Wizara na Taasisi zake

78. Mheshimiwa Spika, Maeneo ya vipaumbele muhimu ambavyo Wizara na taasisi zake itakavyovitekeleza kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ni ifuatavyo: -

i. Kuendelea na kuanza kujenga vituo jumuishi vya Taasisi za Sheria Nchini;

ii. Kuendelea na kuanza kujenga majengo ya Makao Makuu ya Wizara na taasisi zake katika mji wa Dodoma;

iii. Kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala ya kikatiba na utawala wa sheria;

iv. Kuendelea kuhuisha sheria mbalimbali ili kuimarisha uhuru na wajibu wa wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo na kukuza demokrasia na utawala wa Sheria;

v. Kuimarisha mifumo ya uangalizi wa matumizi ya utajiri na maliasilia za nchi ili kuleta manufaa kwa wananchi na maendeleo ya Taifa kwa ujumla;

vi. Kuendelea kuhamasisha matumizi ya njia mbadala za utatuzi wa migogoro ambazo ni usuluhishi, upatanishi, maridhiano na majadiliano ili kurahisisha na kuharakisha upatikanaji wa haki nchini;

vii. Kuimarisha mifumo ya kuhamasisha, kuzingatia na kulinda haki za watu na haki za binadamu;

viii. Kuendelea kuimarisha mifumo ya utoaji Haki nchini na kuhimiza matumizi ya TEHAMA katika Sekta ya Sheria;

ix. Kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa Huduma ya Msaada wa Kisheria nchini;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

- x. Kutekeleza Programu ya Kutumia Lugha ya Kiswahili katika utoaji Haki Nchini;
- xi. Kuendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Pili wa Taifa wa Haki Mtoto 2020/2021-2024/2025;
- xii. Kuendelea kuimarisha Usajili wa matukio muhimu ya binadamu na takwimu pamoja na shughuli za ufilisi na udhamini;
- xiii. Kuharakisha utatuzi wa mashauri ya kawaida na mkakati wa kumaliza mashauri ya muda mrefu (Backlog);
- xiv. Kuimarisha uwezo katika ukaguzi na usimamizi wa shughuli za Mahakama;
- xv. Kuendelea kutekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa Majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali;
- xvi. Kuendelea na ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mahakama ya Tanzania ili kuhamia Dodoma;
- xvii. Kuimarisha maendeleo ya rasilimali watu, ikiwa ni pamoja na mafunzo, na nidhamu ya watumishi;
- xviii. Kuongeza ushirikiano na wadau wa haki jinai ili kuharakisha huduma ya utoaji haki;
- xix. Kuendesha vikao vya kisheria vya Tume na mchakato wa Ajira ya watumishi wa Mahakama;
- xx. Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu majukumu ya Tume na Kamati za Maadili ya Maafisa wa Mahakama ngazi ya Mikoa na Wilaya ;
- xxi. Kufanya Tafsiri, Uandishi na Urekebu wa sheria;
- xxii. Kutoa ushauri wa kisheria na kufanya Upekuzi na Marejeo ya Mikataba;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

xxiii. Kuimarisha uendeshaji mashtaka na usimamizi wa mashauri ya jinai;

xxiv. Kuimarisha uratibu na usimamizi wa upelelezi wa makosa ya jinai;

xxv. Kuimarisha mfumo wa utaifishaji mali, usimamizi na urejeshwaji wa mali zinazohusiana na uhalifu;

xxvi. Kuimarisha utekelezaji wa programu ya kutenganisha shughuli za Mashtaka na Upelelezi;

xxvii. Kuratibu, kusimamia na kuiwakilisha Serikali na Taasisi zake katika kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi yaliyofunguliwa na au dhidi ya Serikali katika mahakama na mabaraza mbalimbali ndani na nje ya nchi;

xxviii. Kufanya uchunguzi kuhusu masuala ya haki za binadamu na utawala bora;

xxix. Kutoa elimu kwa Umma kuhusu masuala ya haki za binadamu na utawala bora;

xxx. Kuimarisha mahusiano na Taasisi za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa;

xxxi. Kufanya tafiti kuhusu masuala ya haki za binadamu na utawala bora

xxxii. Kufanya Tathmini ya utekelezaji wa sheria za Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya; na Mfumo wa Sheria unaosimamia Usafiri Majini. xxxiii. Kufanya Mapitio ya mifumo ya sheria za Usimamizi wa haki katika Mahakama za Mwanzo; Makosa ya uhujumu uchumi; na Usajili wa wadhamini.

xxxiii. Kuimarisha maendeleo ya rasilimali watu na vitendea kazi.

(b) Makusanyo ya Maduhuli ya Serikali

79. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 12,676,201,000.00** ikiwa ni maduhuli ya Serikali, kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 3:-**

Jedwali Na. 3: Makadirio ya Maduhuli ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

| | | | |
|--------------|---|------------|--------------------------|
| Fungu 12 | - | Sh. | 0.00 |
| Fungu 16 | - | Sh. | 0.00 |
| Fungu 19 | - | Sh. | 0.00 |
| Fungu 35 | - | Sh. | 60,000,000.00 |
| Fungu 40 | - | Sh. | 12,571,199,000.00 |
| Fungu 41 | - | Sh. | 45,000,000.00 |
| Fungu 55 | - | Sh. | 2,000.00 |
| Fungu 59 | - | Sh. | 0.00 |
| JUMLA | | Sh. | 12,676,201,000.00 |

(c) Makadirio ya Fedha kwa ajili ya Kutekeleza Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

79. Mheshimiwa Spika, Ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 272,768,278,800.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kati ya Fedha hizo, **Shilingi 207,703,708,800.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 65,064,570,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo. Mchanganuo wa makadirio ya bajeti kwa mafungu nane (8) ya Wizara na taasisi zake ni kama ilivyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 4: -**

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Jedwali Na. 4: Mchanganuo wa Makadirio ya Bajeti kwa Wizara ya Katiba na Sheria na Mafungu yake kwa mwaka wa fedha, 2022/2023

| Na. | Fungu la Matumizi | Bajeti 2022/23 |
|--------------|--------------------------|---------------------------|
| 1. | Mishahara ya watumishi | 95,356,423,800.00 |
| 2. | Matumizi mengineyo | 112,347,285,000.00 |
| 3. | Miradi ya Maendeleo | 65,064,570,000.00 |
| JUMLA | | 272,768,278,800.00 |

81. Mheshimiwa Spika, Kiasi hicho cha fedha kinaombwa kupitia mafungu ya bajeti yaliyo chini ya Wizara yafuatavyo:-

(i) Fungu 12: Tume ya Utumishi wa Mahakama

Matumizi ya Mishahara - Sh. 461,127,800.00

Matumizi Mengineyo - Sh. 2,700,000,000.00

Matumizi ya Maendeleo (Ndani) - Sh. 0

Matumizi ya Maendeleo (Nje) - Sh. 0

Jumla - Sh. 3,161,127,800.00

(ii) Fungu 16: Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Matumizi ya Mishahara - Sh. 2,928,360,000.00

Matumizi Mengineyo - Sh. 6,942,981,000.00

Matumizi ya Maendeleo (Ndani) - Sh. 4,000,000,000.00

Matumizi ya Maendeleo (Nje) - Sh. 500,000,000.00

Jumla - Sh. 14,371,341,000.00

(iii) Fungu 19: Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

Matumizi ya Mishahara - Sh. 3,339,798,000.00

Matumizi Mengineyo - Sh. 9,473,018,000.00

Matumizi ya Maendeleo (Ndani) - Sh. 0

Matumizi ya Maendeleo (Nje) - Sh. 0

Jumla - Sh. 12,812,816,000.00

(iv) Fungu 35: Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

Matumizi ya Mishahara - Sh. 14,548,751,000.00

Matumizi Mengineyo - Sh. 22,068,944,000.00

Matumizi ya Maendeleo (Ndani) - Sh. 8,000,000,000.00

Matumizi ya Maendeleo (Nje) - Sh. 630,000,000.00

Jumla - Sh. 45,247,695,000.00

(v) Fungu 40: Mfuko wa Mahakama

Matumizi ya Mishahara - Sh. 63,408,443,000.00

Matumizi Mengineyo - Sh. 57,774,382,000.00

Matumizi ya Maendeleo (Ndani) - Sh. 36,002,000,000.00

Matumizi ya Maendeleo (Nje) - Sh. 3,091,000,000.00

Jumla - Sh. 160,275,825,000.00

(vi) Fungu 41: Wizara ya Katiba na Sheria

Matumizi ya Mishahara - Sh. 7,647,528,000.00

Matumizi Mengineyo - Sh. 6,865,271,000.00

Matumizi ya Maendeleo (Ndani) - Sh. 5,110,800,000.00

Matumizi ya Maendeleo (Nje) - Sh. 7,615,770,000.00

Jumla - Sh. 27,239,369,000.00

(vii) Fungu 55: Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

Matumizi ya Mishahara - Sh. 2,292,096,000.00

Matumizi Mengineyo - Sh. 4,098,680,000.00

Matumizi ya Maendeleo (Ndani) - Sh. 0

Matumizi ya Maendeleo (Nje) - Sh. 115,000,000.00

Jumla - Sh. 6,505,776,000.00

(viii) Fungu 59: Tume ya Kurekebisha Sheria

Matumizi ya Mishahara - Sh. 730,320,000.00

Matumizi Mengineyo - Sh. 2,424,009,000.00

Matumizi ya Maendeleo (Ndani) - Sh. 0

Matumizi ya Maendeleo (Nje) - Sh. 0

Jumla - Sh. 3,154,329,000.00

JUMLA KUU SH. 272,768,278,800.00

82. Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina na mchanganuo wa maombi ya fedha za bajeti ya kila Fungu umeainishwa kwenye vitabu vya Randama za mafungu husika ambavyo vimegawanywa kwa Waheshimiwa Wabunge kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Bunge.

83. Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru viongozi na watendaji wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya uwaziri. Hakika, ni kutokana na ushirikiano huo nimeweza kusimama leo hii mbele ya Bunge lako kueleza mafanikio, mipango na mikakati tuliyonayo katika kuwahudumia wananchi. Hivyo, kipekee nimshukuru Mhe. Geophrey Mizengo Pinda (Mb.) Naibu Waziri wa Katiba na Sheria; Bi. Mary Gasper Makondo, Katibu Mkuu; Dkt. Khatibu Malimi Kazungu, Naibu Katibu Mkuu; Mhe. Prof. Ibrahimu Hamisi Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Mahakama; Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi (Mb.), Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Mhe. Mustapher Mohamed Siyani, Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania; Prof. Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama; Mhe. Wilbert Martin Chuma, Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania; Bw. Sylvester Anthony Mwakitalu, Mkurugenzi wa Mashtaka; Bw. Gabriel Pascal Malata, Wakili Mkuu wa Serikali; Bi. Angela Kemanzi Anatory, Kabidhi Wasii Mkuu na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili Ufilisi na Udamini; Mhe. Jaji Mstaafu wa Mahakama ya Rufani January Henry Msoffe, Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria; Bw. Casmir Sumba Kyuki, Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania; Mhe. Jaji Mstaafu wa Mahakama Kuu ya Tanzania Mathew Mhina Mwaimu, Mwenyekiti Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Bw. Patience Kilanga Ntwina, Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Mhe. Jaji wa Mahakama ya Rufani Dkt. Paul Faustin Kihwelo, Mkuu wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto; Mhe. Jaji wa Mahakama Kuu Dkt. Benhaji Shaaban Masoud, Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania; Wakurugenzi na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake. Aidha,

nawashukuru familia yangu ikiwa ni pamoja na mke wangu Bibi. Flora Ndumbaro na watoto wangu kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia kwa kunivumilia na kunitia moyo wakati ninapokuwa natekeleza majukumu yangu ya kulumikika Taifa. Mwisho lakini sio mwisho kwa umuhimu, naomba nichukue fursa hii kwa namna ya kipekee kabisa kuwashukuru Wapiga kura wa Jimbo langu la Songea Mjini kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika shughuli za kuleta maendeleo ya jimbo letu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria. Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria. Kwa niaba yake Mheshimiwa Zainab A. Katimba.

MHE. ZAINAB A. KATIMBA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba taarifa yote ya Kamati iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa mezani.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria na kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako kwamba Kamati imefanya uchambuzi wa Bajeti ya Wizara

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zilizo chini yake katika Mafungu ya kibajeti yafuatayo: Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria; Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama; Fungu 19 – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali; Fungu 35 – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka; Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria pamoja na Fungu 40 - Mfuko wa Mahakama katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida; katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara ya Katiba na Sheria iliidhinishwa jumla ya Sh.65,739,056,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Februari, 2022 Wizara pamoja na taasisi zilizo chini yake zilikuwa zimepokea jumla ya Sh.51,769,680,705.92. Mchanganuo wa Mwenendo wa Fedha za Matumizi ya Kawaida umeainishwa katika Jedwali Na. 2.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi kuhusu mwenendo wa bajeti ya Matumizi ya Kawaida, Kamati imebaini masuala yafuatayo:

(a) Mapokezi ya jumla ya fedha za Matumizi ya Kawaida ni sawa na asilimia asilimia 78.75 ya makadirio. Kiwango hiki kimeongezeka ikilinganishwa na mapokezi katika kipindi kama hicho kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, ambapo mapokezi yalikuwa ni asilimia 65.53;

(b) Baadhi ya Mafungu yaliyo chini ya Wizara hiyo yamepokea fedha pungufu za Matumizi ya Kawaida ukilinganisha na Mafungu mengine. Mafungu hayo ni Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama na Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambapo walipokea asilimia 63.96 na asilimia 61.64 mtawalia.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kwamba, mapokezi ya fedha za Matumizi ya Kawaida yanapaswa kuwa na uwiano wenye ulinganifu kwa sababu katika fedha hizo imo mishahara ya watumishi, lakini pia zipo fedha za

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

matumizi mengineyo (O.C.) ambazo hutumika kwa ajili ya uendeshaji kila wa siku wa taasisi husika. Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara ya Katiba iliidhinishiwa jumla ya Sh.52,915,830,000 ambapo kati ya fedha hizo, Sh.44,100,000,000 ni Fedha za Ndani na Sh.8,815,330,000 ni Fedha za Nje. Hadi kufikia Februari, 2022, Wizara na taasisi zake zilikuwa zimepokea jumla ya Sh.45,059,412,966 sawa na wastani wa asilimia 85 ya makadirio. Mchanganuo wa bajeti ya maendeleo na mwenendo wa mapokezi ya fedha umefafanuliwa katika Jedwali Na.3.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini mambo mbalimbali kuhusu utekelezaji wa bajeti ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Naomba nitoe taarifa kuhusu baadhi ya mambo yaliyobainika kama ifuatavyo:-

(a) Pamoja na kwamba kwa ujumla mapokezi ya Fedha za Nje ni makubwa, Mafungu mengine ya kibajeti chini ya Wizara ya Katiba na Sheria yalipokea fedha pungufu. Kwa mfano, Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria ilipokea asilimia 24.74 ya Fedha za Nje zilizoidhinishwa wakati Fungu 35 – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilipokea asilimia 8.45 tu ya Fedha za Nje.

(b) Kamati pia imebaini kwamba mapokezi ya Fedha za Ndani yako chini ya kiwango kilichotarajiwa kwa Mafungu yote ambapo mapokezi ya juu kabisa ni katika Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama ambayo imepokea asilimia 44.53 ya Fedha iliyoidhinishwa, wakati mapokezi ya chini kabisa ni katika Fungu 35 – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ambayo ilipokea asilimia 7.14 tu ya Fedha za Ndani. Hali hii inaweza kukwamisha miradi ya maendeleo iliyopangwa endapo fedha za nje zitachelewa au kutofika kabisa kama ambavyo tumeona kwa baadhi ya Mafungu.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Katiba inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh.111,347,352,800. Jedwali Na.4 linatoa mchanganuo wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara pamoja na taasisi zilizo chini yake. Kwa ujumla, Bajeti ya Wizara ya Katiba

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

na Sheria na taasisi imeongezeka kwa asilimia 41.91 ukilinganisha na bajeti iliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha unaoisha.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Katiba na Sheria inaomba kuidhinishwa jumla ya Sh.85,375,782,840 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Makadirio haya ni sawa na ongezeko la asilimia 29.87 ukilinganisha na kiasi kilichotengwa katika Mwaka wa Fedha unaoisha.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake Kamati imebaini mambo mbalimbali ikiwemo yafuatayo:-

(a) Kwa ujumla bajeti ya Mishahara Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, imepanda kwa asilimia 30.69 ukilinganisha na Mwaka wa Fedha 2021/2022, wakati bajeti ya Matumizi Mengineyo imepanda kwa asilimia 29.38. Hata hivyo, ni Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora tu ambalo bajeti ya Mishahara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 imepungua.

(b) Mafungu manne ambayo ni Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria; Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria; Fungu 19 – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali; na Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama hayakupata ongezeko la bajeti ya Matumizi ya Kawaida (OC) katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, ukilinganisha na bajeti ya Mwaka 2021/2022. Hata hivyo, pamoja na kwamba Mafungu mengine matatu kati ya hayo yamepata ongezeko la bajeti ya Mishahara lisilozidi asilimia 26 kwa kila fungu katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria limepata ongezeko la asilimia 692.49.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Katiba na Sheria inaomba kuidhinishwa jumla ya Sh.25,971,570,000 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Makadirio haya ni sawa na ongezeko la asilimia 104.08 ukilinganisha na kiasi kilichotengwa katika Mwaka wa Fedha unaoisha. Jedwali Na. 6 linaoonesha

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ulinganifu wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kati ya Mwaka wa Fedha 2021/2022 na Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi huo, Kamati imebaini masuala yafuatayo:-

(a) Kwa ujumla, Bajeti ya Maendeleo kwa kutumia Fedha za Ndani katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 imepanda kwa asilimia 242.22 ukilinganisha na bajeti hiyo katika Mwaka wa Fedha 2021/2022. Kwa upande mwingine, Bajeti ya Maendeleo kwa kutumia Fedha za Nje imepanda kwa asilimia 14.69 tu.

(b) Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeongeza bajeti ya fedha za ndani za maendeleo kwa asilimia 300 katika Mwaka wa Fedha 2022/2023. Hata hivyo, Kamati ilibaini kwamba fedha zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 hazikupokelewa kufikia Februari, 2022.

(c) Bajeti ya Maendeleo katika Fungu 35 - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa fedha za nje umeshuka kwa asilimia 36.59. Aidha, pamoja na kwamba bajeti ya jumla ya Maendeleo imepanda kwa asilimia 166.66 bado kiwango hicho hakiridhishi ukilinganisha na mahitaji halisi ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka. Kwa mfano, Kamati imebaini kwamba Ofisi hii ina uhitaji wa majengo ili kuzifikia Wilaya 125 ambazo Ofisi za Mashtaka hazijafunguliwa.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Jumla. Kamati ina maoni na ushauri wa jumla kwa Serikali kama ifuatavyo:-

(a) Kamati imebaini kwamba, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida hususan Matumizi Mengineyo (*O.C*) imeongezeka kwa wastani wa asilimia 29.87. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zilizotengwa na Bunge zinafika kwa wakati ili kuwezesha Wizara na taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, Kamati inashauri Wizara na taasisi hizo kuwa wabunifu wa namna bora za utendaji wa majukumu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

yao kwa ufanisi na kasi zaidi ili fedha za Matumizi Mengineyo (O.C) zinazofika zitumike kwa weledi.

(b) Kamati ilibaini kwamba ni asilimia 45.37 tu ya fedha za ndani zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika Wizara ya Katiba na Sheria ndizo zilipatikana. Kamati inashauri Serikali ihakikishe kwamba inatoa kwa wakati Fedha za Maendeleo ili kuziwezesha Taasisi na Idara za Serikali kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, Serikali ijielekeze zaidi kwenye kutumia vyanzo vya ndani katika kutekeleza Miradi mbalimbali ya Maendeleo nchini.

(c) Kamati ilibaini kwamba, makusanyo ya maduhuli katika mwaka unaoisha yamevuka lengo ambapo hadi kufikia Februari, 2022 Wizara na taasisi zake zilikuwa zimekusanya zaidi ya asilimia 89. Pamoja na hali hiyo, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara imepanga kukusanya maduhuli kwa ongezeko la asilimia asilimia 3.55 tu ukilinganisha na Mwaka wa Fedha unaoisha. Kamati inashauri kwamba, Wizara itathmini upya vyanzo vya mapato pamoja na uwezo wa kukusanya mapato hayo. Kwa kufanya hivyo, Serikali itaweka makadirio ya makusanyo ya maduhuli ambayo ni halisi kulingana na uwezo wake wa kukusanya.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni yafuatayo katika Fungu hili. Maoni na Ushauri Mahsus; Wizara ifanye jitihada za makusudi na kuratibu zoezi la kuajiri Mwakili wa Serikali ili kupunguza uhaba wa wataalam hao katika idara na taasisi mbalimbali inazosisimamia. Zoezi hili liende sambamba na kutenga fedha za kutosha kuwapa mafunzo stahiki watumishi waliopo na watakaoajiriwa ili kuongeza ufanisi wa utendaji wao.

Mheshimiwa Spika, Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kamati ina maoni na ushauri ufuatao katika Fungu hili:-

(a) Kamati inapongeza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Seriali kwa kuanza kutunga sheria kwa lugha ya Kiswahili na kuendelea kutafsiri sheria zilizopo zililizoandikwa kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kiingereza. Kamati inaishauri Serikali kuweka kipaumbele cha kutafsiri Sheria kwa Kiswahili hususan sheria zinazotumika katika jamii mara kwa mara. Mfano wa makundi ya sheria hizo ni Sheria za Usalama Barabarani, Kanuni za Adhabu, Sheria za Kodi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Fungu 35 – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka; Kamati ina maoni na ushauri ufuatao:-

(a) Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ndicho chombo kikuu kinachoweza kuisaidia Serikali kupunguza mlundikano wa kesi Mahakamani na mahabusu katika magereza na hatimaye kupunguza malalamiko ya wananchi kuhusu mfumo mzima wa hakijina nchini.

Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba Bajeti ya Serikali haitoi kipaumbele kinachostahili kwa chombo hiki ukilinganisha na mahitaji halisi ya kibajeti. Kamati inashauri kwamba, Serikali itathmini mahitaji ya ofisi hii na kuipa kipaumbele cha kibajeti kulingana na mahitaji muhimu ya Ofisi hii ikiwemo Fedha za Matumizi Mengineyo na Fedha za Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Kamati inaishauri Tume hii mambo yafuatayo:-

(a) Kamati ilibaini kwamba kwa mwaka wa pili mfululizo Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora haijatenga kabisa Fedha za Ndani ili kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kamati inaishauri Tume hiyo kwa miradi ambayo inalenga kutoa elimu kwa umma, ni vyema Tume ikaanza utaratibu wa kutenga fedha za ndani ili kutekeleza miradi husika. Aidha, Tume imebuni mbinu za kutoa elimu kupitia majukwaa ambayo yana hadhira kubwa ikiwemo mitandao ya kijamii ili kuwafikia watu wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria. Kamati ina maoni na ushauri ufuatao:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(a) Tume ya Kurekebisha Sheria itoe elimu kwa umma kupitia vipindi vya redio, runinga, vipeperushi, na majarida mbalimbali kuhusu sheria zinazofanyiwa marekebisho kwa lengo la kuwapa uelewa wanachi.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Aidha, nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, kwa ushirikiano ambao wameupatia Kamati wakati wa uchambuzi wa bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake zote kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Mary Gabriel Makondo na akisaidiwa na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Khatibu M. Kazungu.

Aidha, namshukuru Mtendaji Mkuu wa Mahakama Profesa Elisante Ole-Gabriel na watendaji wote wa Mahakama ya Tanzania na Taasisi zilizo chini yake kwa ushirikiano ambao wameupatia Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kuwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Ndugu Nenelewa Mwihambi, *ndc*, Katibu wa Bunge kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA
SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA
KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022
PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA
HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 - KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI

*[Imetolewa kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za
Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020]*

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Maelezo ya Awali

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii imegawanyika katika Sehemu Kuu zifuatazo:-

a) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha muundo wa Taarifa na kuainisha namna Kamati ilivyofanya kazi.

b) Sehemu ya Pili ni uchambuzi na tathmini ya Kamati kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Aidha, Sehemu hii inatoa uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

c) Sehemu ya Tatu ni Maoni na Ushauri wa Kamati.

d) Sehemu ya Nne ni Hitimisho.

1.2 Namna Kamati Ilivyotekeleza Majukumu Yake

Mheshimiwa Spika, katika kufanyia kazi utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kamati ilifanya mambo yafuatayo: -

a) Kufanya ziara ya ukaguzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na kujadili taarifa za utekelezaji wa miradi hiyo kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

b) Kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

c) Kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

Mheshimiwa Spika, aidha Kamati ilitoa maoni na mapendekezo mbalimbali kwa Serikali na baadae kuwasilisha hoja mahsusi za kibajeti ili Kamati ya Bunge ya Bajeti iyazingatie wakati wa kuishauri Wizara ya Fedha na Mipango katika Bajeti ya Kuu ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

SEHEMU YA PILI

2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI

2.1 Msingi wa Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, msingi wa uchambuzi unatokana na **Kifungu cha 7 (1) (a)** kikisomwa pamoja na **Kifungu cha 6 (2) (b)** cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge ikisomwa pamoja na **Kanuni ya 118 (4)**. Kanuni hizi zimeipa Kamati ya Katiba na Sheria jukumu la kusimamia Shughuli za

Wizara ya Katiba na Sheria sambamba na Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo ili kukidhi matakwa ya **Ibara ya 63 (3) (b)** ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.

2.2 Mawanda ya Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Wizara kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Moja kati ya vigezo vinavyotumika katika uchambuzi huo ni, Kamati kufanya ulinganisho baina ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha unaoisha na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha unaofuata.

Aidha, Kamati iliangalia mwenendo wa makusanyo ya maduhuli, na upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida kwa Mwaka wa Fedha unaoisha. Aidha, kwa kuzingatia **Kanuni ya 117 (1)** Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi ili kujionea utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha unaoisha. Katika ukaguzi huo, Kamati iliangalia mambo mbalimbali ikiwemo ufanisi wa utekelezaji wa miradi husika.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako kwamba Kamati imefanya uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zilizo chini yake katika mafungu ya kibajeti yafuatayo:-

- a) **Fungu 41** – Wizara ya Katiba na Sheria
- b) **Fungu 16** – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali
- c) **Fungu 12** – Tume ya Utumishi wa Mahakama
- d) **Fungu 19** – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali
- e) **Fungu 35** – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

f) **Fungu 55** – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

g) **Fungu 59** – Tume ya Kurekebisha Sheria

Aidha, kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa kwa mujibu wa **Kifungu cha 9 (1) (c)** cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 bajeti ya **Fungu 40** – Mfuko wa Mahakama ilishughulikiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti. Hata hivyo, Kamati ya Katiba na Sheria ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Fungu hilo kwa niaba ya Bunge.

2.3 Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

2.3.1 Maelezo ya Awali

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara pamoja na taasisi zake iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 78,464,886,000** kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali. Fedha zilizotengwa zilitumika kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwemo yafuatayo:-

- a) Kusimamia mfumo wa haki na utoaji haki
- b) Kuendesha Mashtaka ya Jinai na kushughulikia Uendeshaji wa Mashauri ya Madai na Usuluhishi
- c) Kuratibu Masuala ya Haki za Binadamu na Utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria

2.3.2 Utekelezaji wa Maoni na Ushauri ya Kamati

Mheshimiwa Spika, wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hiyo. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, mfano wa ushauri uliozingatiwa kikamilifu ni pamoja na ushauri juu ya muundo wa bajeti ya matumizi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya kawaida ambapo Kamati ilishauri Wizara ya Katiba na Sheria kuandaa bajeti ya mwaka 2022/2023 yenye kuendana na uhalisia wa mahitaji ya utekelezaji wa vipaumbele na majukumu ya Ofisi hiyo. Kamati imebaini kwamba Wizara ya Katiba na Sheria imeongeza bajeti ya Matumizi ya Kawaida (OC) sawa na ushauri wa Kamati kama ambavyo ufafanuzi wake unatolewa katika Taarifa hii.

2.3.3 Ukusanyaji wa Maduhuli

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zilizo chini yake ziliweka malengo ya kukusanya maduhuli ya jumla ya **Sh. 101,400,000**. Maduhuli hayo ni kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato katika **Fungu 41** – Wizara ya Katiba na Sheria, na **Fungu 35** – Ofisi ya Taifa ya Mashataka. Hadi kufikia Februari, 2022 Wizara ya Katiba na Sheria ilikuwa imekusanya jumla ya **Sh. 38,894,315,212.36** sawa na **asilimia 38,357.31**. Mchanganuo wa makadirio na makusanyo ya taasisi hizo kufikia Februari, 2022 umeainishwa katika Jedwali Na. 1.

JEDWALI NA. 1 – Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka Fedha 2021/2022

| FUNGU | MADUHULI KWA MWAKA 2021/2022 (TZS) | MAKUSANYO KUFIKIA FEBRUARI, 2022 (TZS) | ASILIMIA YA MAKUSANYO |
|---------------------------------------|--|--|--------------------------|
| Fungu 35 - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 56,400,000 | 38,854,100,817.55 | 68,890.25% |
| Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria | 45,000,000 | 40,214,395.81 | 89.36% |
| JUMLA | 101,400,000 | 38,894,315,213.36 | 38,357.31% |

Chanzo: Randama za Wizara ya Katiba na Sheria

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini masuala yafuatayo katika makusanyo ya maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022:-

a) Makusanyo ya maduhuli yamevuka lengo kwa zaidi ya **Sh. 38,792,915,213.36**. Tofauti hiyo inatokana na makusanyo ya ziada jumla ya **Sh. 38,797,700,8170.55** yaliyokusanywa na **Fungu 35** – Ofisi ya Mashtaka kwa utaratibu wa washtakiwa kukiri makosa yao (*plea bargaining*). Kwa maelekezo ya Wizara ya Fedha, fedha hizi zilipokusanywa ziliwekwa kwenye akaunti maalum iliyoko Benki Kuu ya Tanzania (BOT) lakini zikahesabiwa kuwa maduhuli ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

b) **Fungu 41** – Wizara ya Katiba ilikusanya **Sh. 40,214,395.81** sawa na **asilimia 89** ya malengo waliyojiwekea ikilinganishwa na makusanyo ya **Sh. 15,267,873.78** zilizokusanywa katika kipindi kama hicho katika Mwaka wa Fedha 2020/2021. Kamati imebaini kwamba, moja kati ya sababu za kuvuka malengo hayo ni kuanza kutekelezwa masharti ya Sheria ya Usuluhishi, **Sura ya 15** ambayo pamoja na mambo mengine imeweka utaratibu wa kuwasajili Wasuluhishi, Wapatanishi, Waendesha Majadiliano na Maridhiano.

2.3.4 Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara ya Katiba na Sheria iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 65,739,056,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Februari, 2022 Wizara pamoja na taasisi zilizo chini yake zilikuwa zimepokea jumla ya **Sh. 51,769,680,705.92** sawa na wastani wa **asilimia 78.75** ya Bajeti iliyoidhinishwa. Mchanganuo wa Mwenendo wa Fedha za Matumizi ya Kawaida umeainishwa katika Jedwali Na.2.

Jedwali Na. 2 – Mapokezi ya Fedha za Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka 2021/2022

| FUNGU LA BAJETI | BAJETI YA MIRADI YYA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 (TZS) | | FEDHA ILIYOPOKELEWA KUFIKIA FEBRUARI, 2022 (TZS) | | ASILIMIA YA MAPOKEZI | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|----------------------|--|-----------------------|----------------------|----------------------|
| | FEDHA ZA NDANI | FEDHA ZA NJE | FEDHA ZA NDANI | FEDHA ZA NJE | FEDHA ZA NDANI | FEDHA ZA NJE |
| Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 1,000,000,000 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0% | 0% |
| Fungu 35 – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 3,000,000,000 | 993,616,000 | 214,155,912 | 84,000,000 | 7.14% | 8.45% |
| Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama | 39,100,000,000 | 1,090,000,000 | 19,365,123,301 | 23,133,893,262 | 49.53% | 2,122.37% |
| Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria | 1,000,000,000 | 6,358,598,000 | 429,125,000 | 1,573,036,400 | 42.91% | 24.74% |
| Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 0.00 | 373,616,000 | 0.00 | 260,079,091 | 0% | 69.61% |
| <i>Jumla Ndogo</i> | <i>44,100,000,000</i> | <i>8,815,830,000</i> | <i>20,008,404,213</i> | <i>25,051,008,753</i> | 45.37% | 284.16% |
| JUMLA KUU | 52,915,830,000 | | 45,059,412,966 | | 85.15% | |

Chanzo: Randama za Wizara ya Katiba

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi kuhusu mwenendo wa bajeti ya Matumizi ya Kawaida, Kamati imebaini masuala yafuatayo: -

a) Mapokezi ya jumla ya fedha za Matumizi ya Kawaida ni sawa na asilimia **asilimia 78.75** ya makadirio. Kiwango hiki kimeongezeka ikilinganishwa na mapokezi katika kipindi kama hicho katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 ambapo mapokezi walikuwa ni **asilimia 65.53**.

b) Baadhi ya mafungu yaliyo chini ya Wizara hiyo yamepokea fedha pungufu za Matumizi ya Kawaida ukilinganisha na mafungu mengine. Mafungu hayo ni **Fungu 12** – Tume ya Utumishi wa Mahakama na **Fungu 16** – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambapo walipokea **asilimia 63.96** na **asilimia 61.64** mtawalia.

c) **Fungu 35** – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imevuka matarajio ya mapokezi kwa sababu hadi kufikia Februari, 2022 limepokea **asilimia 102** ya Fedha za Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kwamba, mapokezi ya fedha za Matumizi ya Kawaida yanapaswa kuwa na uwiano wenye ulinganifu kwa sababu katika fedha hizo imo mishahara ya watumishi lakini pia zimo fedha za matumizi mengineyo (O.C.) ambazo hutumika kwa ajili ya uendeshaji kila siku wa taasisi husika.

2.3.5 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara ya Katiba iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 52,915,830,000** ambapo kati ya fedha hizo, **Sh. 44,100,000,000** ni Fedha za Ndani na **Sh. 8,815,830,000** ni Fedha za Nje. Fedha hiyo ilitengwa kutekeleza miradi ya maendeleo katika mafungu mbalimbali chini Wizara ya Katiba na Sheria ikiwemo **Fungu 40** – Mfuko wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari, 2022, Wizara na taasisi zake ilikuwa imepokea jumla ya **Sh. 45,059,412,966** sawa na wastani wa **asilimia 85** ya makadirio. Mchanganuo wa bajeti ya maendeleo na mwenendo wa mapokezi ya fedha umefafanuliwa katika Jedwali Na.3.

Jedwali Na. 3 – Mchanganuo wa Bajeti na Mapokezi ya Fedha za Maendeleo 2021/2022

| FUNGU LA KIBAJETI | FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA (TZS) | | FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO (TZS) | | JUMLA YA FEDHA KATIKA FUNGU (TZS) |
|---|------------------------------------|-----------------------|------------------------------------|----------------------|-----------------------------------|
| | MISHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | FEDHA ZA NDANI | FEDHA ZA NJE | |
| Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama | 461,127,800 | 2,700,000,000 | 0.00 | 0.00 | 3,161,127,800 |
| Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 2,928,360,000 | 6,942,981,000 | 4,000,000,000 | 500,000,000 | 14,371,341,000 |
| Fungu 19 – Ofisi ya Wakiili Mkuu wa Serikali | 3,339,798,000 | 9,473,018,000 | 0.00 | 0.00 | 12,812,816,000 |
| Fungu 35 – Ofisi ya Taifa ya Mashaka | 14,548,751,000 | 22,068,944,000 | 8,000,000,000 | 630,000,000 | 45,247,695,000 |
| Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria | 7,502,427,000 | 5,865,271,000 | 5,110,800,000 | 7,615,770,000 | 26,094,268,000 |
| Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 2,292,096,000 | 4,098,680,000 | 0.00 | 115,000,000 | 6,505,776,000 |
| Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria | 6,505,776,000 | 2,424,009,000 | 0.00 | 0.00 | 3,154,329,000 |
| JUMLA KUU | 31,802,879,840 | 53,572,903,000 | 17,110,800,000 | 8,860,770,000 | 111,347,352,800 |

Chanzo: Randama za Wizara na Usanifu wa Kamati

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi ambao imeufanya, Kamati imebaini mambo mbalimbali kuhusu utekelezaji wa bajeti ya maendeleo katika Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Naomba nitoe taarifa kuhusu baadhi ya mambo yaliyobainika kama ifuatavyo: -

a) Kwa ujumla mapokezi ya Fedha za Nje ni makubwa ambapo Wizara ilipokea **asilimia 284.15** ya makadirio ikilinganishwa na mapokezi ya **asilimia 45.37** ya Fedha za Ndani kutekeleza miradi iliyoidhinishiwa bajeti. Kamati ilibaini kwamba, mapokezi ya Fedha za Nje yalivuka malengo kwa sababu **Fungu 40** – Mfuko wa Mahakama lilipokea **Sh. 23,133,893,262** baada ya Serikali kuingia Mkataba na Benki ya Dunia (*World Bank*) kutekeleza miradi mbalimbali. Awali, Fungu hilo lilikuwa limeidhinishiwa **Sh. 1,090,000,000** ya Fedha za Nje kutekeleza miradi hiyo.

b) Pamoja na kwamba kwa ujumla mapokezi ya Fedha za Nje ni makubwa, mafungu mengine ya kibajeti chini ya Wizara ya Katiba na Sheria yalipokea fedha pungufu. Kwa mfano,

Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria lilipokea **asilimia 24.74** ya Fedha za Nje zilizoidhinishwa wakati **Fungu 35** – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilipokea **asilimia 8.45** tu ya Fedha za Nje.

c) Kamati pia imebaini kwamba mapokezi ya Fedha za Ndani yako chini ya kiwango kilichotarajiwa kwa mafungu yote ambapo mapokezi ya juu kabisa ni katika **Fungu 40** – Mfuko wa Mahakama ambayo imepokea **asilimia 49.53** ya Fedha iliyoidhinishwa, wakati mapokezi ya chini kabisa ni katika **Fungu 35** – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ambayo ilipokea **asilimia 7.14** tu ya Fedha za Ndani. Hali hii inaweza kukwamisha miradi ya maendeleo iliyopangwa endapo Fedha za Nje zitachelewa au kutofika kabisa kama ambavyo tumeona kwa baadhi ya mafungu.

d) Kamati imebaini kwamba, **Fungu 16** – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilitenga **Sh. 1,000,000,000** kwa Fedha za Ndani kutekeleza miradi ya maendeleo. Hata hivyo, hadi kufikia Februari, 2022, hakuna fedha yoyote iliyotolewa kwa Ofisi hiyo kutekeleza miradi husika. Kwa maoni ya Kamati, mwenendo huu wa mapokezi ya fedha hauleti tija na unaweza kuathiri utekelezaji wa vipaumbele vya maendeleo vya taasisi hizo.

e) Kamati imebaini kwamba, **Fungu 55** – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora halikutenga kabisa Fedha za Ndani kutekeleza miradi ya maendeleo. Fedha za Nje zilizotengwa, zililenga kutekeleza Mradi wa “Uimarishaji wa Upatikanaji Haki za Kisheria Ulinzi wa Haki za Binadamu Tanzania” wenye thamani ya **Sh. 373,616,000**. Hadi kufikia Februari, 2020 mapokezi yalikuwa **asilimia 69.61**. Ni vema Serikali ikatathmini mlinganyo wa bajeti ya maendeleo katika Fungu hilo na kuona iwapo kuendelea kutenga fedha za nje bila kutenga fedha za ndani kunaleta tija katika miradi husika.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba, Kamati pia ilifanya ziara katika Mkoa wa Tanga, Kilimanjaro na Arusha ili kukagua baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha unaoisha. Katika ziara hizo, Kamati ilifanya tathmini ya utekelezaji wa miradi husika ili kutimiza masharti ya **Kanuni**

ya **117 (1)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Miradi iliyokaguliwa na Kamati ni ifuatayo:-

a) Mradi Na. 6311 - Ujenzi wa Bweni la Wavulana Chuo cha Uongozi wa Mahakama (IJA), Lushoto

b) Mradi Na. 6312 – Ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Same

c) Mradi Na. 6312 – Ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Mwanga

d) Mradi Na. 6314 – Ujenzi na Ukarabati wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi

e) Mradi Na. 6389 - Ujenzi wa Kituo Jumuishi cha Kutoa Haki (JC) Arusha

Mheshimiwa Spika, kwa sehemu kubwa Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa miradi iliyokaguliwa kwa sababu imezingatia viwango. Hata hivyo, Kamati imebaini masuala kadhaa ambayo ingependa kuyatolea maelezo katika baadhi ya miradi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza hatua ya Mahakama kujenga na kukarabati majengo yake ambayo kwa muda mrefu yamekuwa katika hali ya uchakavu. Katika **Mradi Na. 6389 wa Ujenzi wa Kituo Jumuishi cha Kutoa Haki (JC) Arusha** lenye thamani ya **Sh. 9,297,560,024.73** Kamati imeridhishwa na ujenzi huo uliokamilika kwa **asilimia 100**. Jengo hilo ni la kisasa, lenye miundombinu rafiki kwa makundi ya watu wenye mahitaji maalum na ambalo kwa maoni ya Kamati, limezingatia viwango vilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, katika **Mradi Na. 6311 wa Ujenzi wa Bweni la Wavulana Chuo cha Uongozi wa Mahakama (IJA) Lushoto** Kamati ilijionea maendeleo mazuri ya utekelezaji wa mradi huo, ambapo kati ya **Sh. 2,628,314,367.76** zilizotengwa, tayari **Sh. 1,072,937,404.45** zilikuwa zimetolewa kutekeleza awamu mbili kati ya tatu za jengo hilo lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **320** kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Kamati ilibaini kwamba mradi huo ulikuwa umetelekezwa kwa kwa sababu chuo hicho kwa muda mrefu kimekuwa hakipati bajeti ya maendeleo mpaka Mahakama ilipoamua kusaidia kumaliza mradi huo. Kamati ina maoni kwamba, jengo hilo litapunguza adha kwa wanafunzi ambao wamekuwa wakilazimika kupanga vyumba nje ya chuo kwa kuongeza nafasi ya malazi chuoni.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Chuo kina takriban wanafunzi 1,100 ambapo zaidi ya wanafunzi 600 wanakaa nje ya chuo. Hivyo basi, hata jengo hilo litakapokamilika, bado kutakuwa na idadi kubwa ya wanafunzi wanaokaa nje ya chuo. Sambamba na hilo, ni vema Mahakama ikafanya pia ukarabati wa Bweni la wasichana ambalo liko pembeni ya bweni jipya la wavulana kwa sababu bweni hilo limechakaa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini pia kwamba chuo hicho kina eneo kubwa ambalo linaweza kutumika kujenga mabweni zaidi. Hivyo basi, Kamati inashauri Serikali kujenga mabweni mengine ili chuo kiweze kuwa na nafasi ya malazi kwa wanafunzi wote ili kuboresha mazingira ya kusoma. Hatua hii iende sambamba na ujenzi wa majengo mapya ya utawala kwa sababu yaliyopo ni chakavu kwa kuwa yalijengwa kipindi cha ukoloni.

2.4 Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

2.4.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Katiba inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 111,347,352,800**. Jedwali Na. 4 linatoa mchanganuo wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara pamoja na taasisi zilizo chini yake.

Jedwali Na. 4 – Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara Mwaka wa Fedha 2022/2023

| FUNGU LA KIBAJETI | MISHAHARA | | ONGEZEKO (%) MISHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | | ONGEZEKO (%) MENGINEYO |
|---|-----------------------|-----------------------|------------------------|-----------------------|-----------------------|------------------------|
| | 2021/2022 | 2022/2023 | | 2021/2022 | 2022/2023 | |
| Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama | 420,191,000 | 461,127,800 | +9.74 | 2,700,000,000 | 2,700,000,000 | 0 |
| Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 2,650,210,000 | 2,928,360,000 | +10.49 | 5,022,981,000 | 6,942,981,000 | +38.22 |
| Fungu 19 – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali | 2,658,329,000 | 3,339,798,000 | +25.63 | 9,473,018,000 | 9,473,018,000 | 0 |
| Fungu 35 – Ofisi ya Taifa ya Mashaka | 9,199,868,000 | 14,548,751,000 | +58.14 | 12,068,944,000 | 22,068,944,000 | +82.85 |
| Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria | 6,089,479,000 | 7,502,427,000 | +23.20 | 5,865,271,000 | 5,865,271,000 | 0 |
| Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 2,495,556,000 | 2,292,096,000 | -8.15 | 3,850,280,000 | 4,098,680,000 | +6.45 |
| Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria | 820,920,000 | 6,505,776,000 | +692.49 | 2,424,009,000 | 2,424,009,000 | 0 |
| JUMLA | 24,334,553,000 | 31,802,879,840 | +30.69 | 41,404,503,000 | 53,572,903,000 | +29.38 |

Chanzo: Randama za Wizara ya Katiba na Sheria

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria na taasisi imeongezeka kwa **asilimia 41.91** ukilinganisha bajeti iliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha unaoisha. Ongezeko hili linaakisi maoni ya Kamati kwamba Serikali iongezeke fedha kwa taasisi mbalimbali za Wizara ili kuboresha ufanisi wa utendaji wake.

2.4.2 Makusanyo ya Maduhuli

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara pamoja na taasisi zake inaomba kuidhinishwa kukusanya **Sh. 105,002,000**. Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la **asilimia 3.55** ukilinganisha na Makadirio ya Makusanyo katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 ambayo yalikuwa **Sh. 101,400,000** (Tazama Jedwali Na. 1).

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kwa maoni ya Kamati, ongezeko hili la makusanyo ni dogo na linaweza kutafsiriwa kwamba, Wizara ya Katiba na Sheria hususan taasisi ambazo zimeidhinishiwa kukusanya maduhuli zimeshindwa kutathmini uwezo wa vyanzo vyake. Maoni haya yamejengwa katika msingi kwamba, katika Mwaka wa Fedha unaoisha kufikia Februari, 2022 taasisi hizo zilikusanya maduhuli zaidi ya makisio yaliyowekwa (Tazama Jedwali Na. 1).

2.4.3 Uchambuzi Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Kawaida

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara ya Katiba na Sheria inaomba kudhinishiwa jumla ya **Sh. 85,375,782,840** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Makadirio haya ni sawa na ongezeko la **asilimia 29.87** ukilinganisha na kiasi cha **Sh. 65,739,056,000** kilichotengwa katika Mwaka wa Fedha unaoisha. Jedwali Na. 5 linaonesha ulinganifu wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kati ya Mwaka wa Fedha 2021/2022 na Mwaka wa Fedha 2022/2023.

| FUNGU LA KIBAJETI | FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO KWA VYANZO VYA NDANI | | ONGEZEKO (%) FEDHA ZA NDANI | FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO KWA FEDHA KUTOKA NJE YA NCHI | | ONGEZEKO (%) FEDHA ZA NJE |
|---|---|-----------------------|-----------------------------|---|----------------------|---------------------------|
| | 2021/2022 | 2022/2023 | | 2021/2022 | 2022/2023 | |
| Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama | 0.00 | 0.00 | 0 | 0.00 | 0.00 | 0 |
| Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 1,000,000,000 | 4,000,000,000 | 300 | 0.00 | 500,000,000 | 0 |
| Fungu 19 – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali | 0.00 | 0.00 | 0 | 0.00 | 0.00 | 0 |
| Fungu 35 – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 3,000,000,000 | 8,000,000,000 | 166.66 | 993,616,000 | 630,000,000 | -36.59 |
| Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria | 1,000,000,000 | 5,110,800,000 | 411.08 | 6,358,598,000 | 7,615,770,000 | 19.77 |
| Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 0.00 | 0.00 | 0 | 373,616,000 | 115,000,000 | 69.22 |
| Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria | 0.00 | 0.00 | 0 | 0.00 | 0.00 | 0 |
| JUMLA | 5,000,000,000 | 17,110,800,000 | 242.22 | 7,725,830,000 | 8,860,770,000 | 14.69 |

Jedwali Na. 5 – Mchanganuo wa Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida 2021/2022 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2022/2023

| FUNGU LA BAJETI | BAJETI YA MATUMIZI YA KAWAIDA 2021/2022 (TZS) | FEDHA ILIYOPOKELEWA KUFIKIA FEBRUARI, 2022 (TZS) | ASILIMIA YA MAPOKEZI KUFIKIA FEBRUARI, 2022 |
|---|---|--|---|
| Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama | 3,120,191,000 | 1,995,622,410.26 | 63.96% |
| Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 7,673,191,000 | 4,730,074,308.28 | 61.64% |
| Fungu 19 – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali | 12,131,347,000 | 8,726,999,644 | 71.94% |
| Fungu 35 – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 21,268,812,000 | 21,757,718,762.48 | 102.30% |
| Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria | 11,954,750,000 | 8,086,936,337.88 | 67.65% |
| Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 6,345,836,000 | 4,216,726,106.23 | 66.45% |
| Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria | 3,244,929,000 | 2,255,603,136.79 | 69.51% |
| JUMLA | 65,739,056,000 | 51,769,680,705.92 | 78.75% |

Chanzo: Randama za Wizara ya Katiba na Sheria

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi huo Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

a) Kwa ujumla bajeti ya Mishahara Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 imepanda kwa **asilimia 30.69** ukilinganisha na Mwaka wa Fedha 2021/2022 wakati bajeti ya Matumizi Mengineyo imepanda kwa **asimilia 29.38**. Hata hivyo, ni **Fungu 55** – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora tu ambalo bajeti ya Mishahara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 imepungua.

b) Mafungu manne ambayo ni **Fungu 59** – Tume ya Kurekebisha Sheria, **Fungu 41** – Wizara ya Katiba na Sheria, **Fungu 19** – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, na **Fungu 12** – Tume ya Utumishi wa Mahakama hayakupata ongezeko la bajeti ya Matumizi ya Kawaida (OC) katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 ukilinganisha na bajeti ya Mwaka 2021/2022. Hata hivyo, pamoja na kwamba mafungu mengine matatu kati ya hayo yamepata ongezeko la bajeti ya Mishahara lisilozidi **asilimia 26** kwa kila fungu katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, **Fungu 59** – Tume ya Kurekebisha Sheria limepata ongezeko la **asilimia 692.49**.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza Fedha za Matumizi ya Kawaida hususan katika Matumizi Mengineyo, ambayo itawezesha taasisi chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kutekeleza majukumu yake na vipaumbele walivyojiwekea.

2.4.4 Uchambuzi Kuhusu Mpango wa Maendeleo

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara ya Katiba na Sheria inaomba kudhinishiwa jumla ya **Sh. 25,971,570,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Makadirio haya ni sawa na ongezeko la **asilimia 104.08** ukilinganisha na kiasi cha **Sh. 12,725,830,000** kilichotengwa katika Mwaka wa Fedha unaoisha. Jedwali Na. 6 linaonesha ulinganifu wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kati ya Mwaka wa Fedha 2021/2022 na Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Jedwali Na. 6 – Mchanganuo wa Makadirio ya Bajeti ya Miradi ya Maendeleo 2021/2022 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2022/2023

| FUNGU LA KIBAJETI | FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO KWA VYANZO VYA NDANI | | ONGEZECO (%) FEDHA ZA NDANI | FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO KWA FEDHA KUTOKA NJE YA NCHI | | ONGEZECO (%) FEDHA ZA NDE |
|--|---|----------------|-----------------------------|---|---------------|---------------------------|
| | 2021/2022 | 2022/2023 | | 2021/2022 | 2022/2023 | |
| Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama | 0.00 | 0.00 | 0 | 0.00 | 0.00 | 0 |
| Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 1,000,000,000 | 4,000,000,000 | 300 | 0.00 | 500,000,000 | 0 |
| Fungu 19 – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali | 0.00 | 0.00 | 0 | 0.00 | 0.00 | 0 |
| Fungu 35 – Ofisi ya Taifa ya Mashitaka | 3,000,000,000 | 8,000,000,000 | 166.66 | 993,616,000 | 630,000,000 | -36.59 |
| Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria | 1,000,000,000 | 5,110,800,000 | 411.08 | 6,358,598,000 | 7,615,770,000 | 19.77 |
| Fungu 55 – Tume ya Haki za Binaadamu na Utawala Bora | 0.00 | 0.00 | 0 | 373,616,000 | 115,000,000 | 69.22 |
| Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria | 0.00 | 0.00 | 0 | 0.00 | 0.00 | 0 |
| JUMLA | 5,000,000,000 | 17,110,800,000 | 242.22 | 7,725,630,000 | 8,860,770,000 | 14.69 |

Chanzo: Randama za Wizara ya Katiba na Sheria

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi huo, Kamati imebaini masuala yafuatayo katika Mpango wa Maendeleo:-

a) Kwa ujumla, Bajeti ya Maendeleo kwa kutumia Fedha za Ndani katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 imepanda kwa **asilimia 242.22** ukilinganisha na bajeti hiyo katika Mwaka wa Fedha 2021/2022. Kwa upande mwingine, Bajeti ya Maendeleo kwa kutumia Fedha za Nje imepanda kwa **asilimia 14.69** tu.

b) **Fungu 16** – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeongeza bajeti ya fedha za ndani za maendeleo kwa asilimia 300. Hata hivyo, Kamati ilibaini kwamba fedha

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 hazikutolewa kikamilifu kwa sababu hadi kufikia Februari, 2022 Ofisi hiyo haikupokea fedha yoyote.

c) Kamati imebaini kwamba, kwa mwaka wa pili mfululuzo, **Fungu 19** – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali halijatengewa kabisa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo. Kutokuwa na bajeti ya maendeleo ni changamoto kwa Ofisi hiyo kwa sababu inashindwa kuendeleza ujenzi wa ofisi zake.

d) Kamati imebaini kwamba, **Fungu 59** – Tume ya Kurekebisha Sheria haijapangiwa kabisa fedha miradi ya maendeleo kwa mwaka wa pili mfululizo pamoja na kwamba Tume hiyo haina jengo la ofisi. Kamati inashauri Serikali kutenga fedha za maendeleo katika Fungu hili Kuiwezesha ianze ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu katika jiji la Dodoma ambapo tayari ina kiwanja katika Mji wa Serikali.

e) Kwa mwaka wa pili mfululizo, **Fungu 55** – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora halijatenga kabisa Fedha za Ndani ili kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Tume hiyo imekuwa kitekeleza miradi ya maendeleo kwa kutumia Fedha za Nje.

f) Bajeti ya maendeleo katika **Fungu 35** – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kwa Fedha za Nje, imeshuka kwa **asilimia 36.59**. Aidha, pamoja na kwamba Bajeti ya Maendeleo imepanda kwa asilimia **166.66**, bado kiwango hicho hakiridhishi ukilinganisha na mahitaji halisi ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka. Kwa mfano, Kamati imebaini kwamba Ofisi hii ina uhitaji wa majengo ili kuzifikia Wilaya 125 ambazo Ofisi za Mashtaka hazijafunguliwa. Hivyo basi, kwa kutopatikana fedha za kutosha kutekeleza miradi ya maendeleo, kunakwamisha utendaji wa Ofisi na hatimaye kupunguza kasi ya uendeshaji wa mashtaka nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kusikiliza maoni ya Bunge na kuongeza Bajeti ya Fedha za Ndani ili kutekeleza miradi ya maendeleo. Kwa uzoefu kama ambavyo Bunge limekuwa likishauri, utegemezi wa Fedha za Nje katika Miradi ya Maendeleo unapaswa

kupungua na ikiwezekana kuondokana kabisa na utegemezi huo.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

3.1 Maoni na Ushauri wa Jumla

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria imepewa dhamana ya kutekeleza majukumu ya Serikali yanayohusu masuala ya Katiba na Sheria za nchi. Dira ya Wizara hii ni Katiba na Sheria wezeshi kwa maendeleo ya Taifa na dira hiyo imelenga kuweka mazingira rafiki ya kisera na ya kisheria ya kuwezesha utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Taifa, kudumisha hali ya amani, utulivu na utangamano wa kitaifa ambazo ni nguzo muhimu kwa mstakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mwelekeo huo, Kamati ina maoni na ushauri wa jumla kwa Serikali kama ifuatavyo:

-

a) Kamati imebaini kwamba, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Bajeti ya Matumizi ya Kawaida hususan Matumizi Mengineyo (O.C) imeongezeka kwa wastani wa **asilimia 29.87**. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zilizotengwa na Bunge zinafika kwa wakati ili kuwezesha Wizara na taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, Kamati inashauri Wizara na taasisi hizo kuwa wabunifu wa namna bora za utendaji wa majukumu yao kwa ufanisi na kasi zaidi ili fedha za Matumizi Mengineyo (O.C) zinafika zinatumika kwa weledi.

b) Kamati ilibaini kwamba ni **asilimia 45.37** tu ya fedha za ndani zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika Wizara ya Katiba na Sheria ndizo zilipatikana. Kamati inashauri Serikali ihakikishe kwamba inatoa kwa wakati Fedha za Maendeleo ili kuziwezesha taasisi na idara za Serikali kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, Serikali

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ijielekeze zaidi kwenye kutumia vyanzo vya ndani katika kutekeleza Miradi mbalimbali ya Maendeleo nchini.

c) Kwa kuwa Kamati imebaini kwamba baadhi ya taasisi zilizo chini yake kutotengewa kabisa fedha za maendeleo, Kamati inashauri Serikali kutenga fedha ili taasisi hizo zipate fedha za utekelezaji wa miradi.

d) Serikali iweke mkakati wa muda mrefu na muda mfupi kuhusu namna bora ya kutekeleza miradi yake yote ya maendeleo ili kuhakikisha miradi iliyopo katika hatua za utekelezaji inakamilika kwa wakati. Aidha, katika mkakati huo, Serikali iainishe namna ambavyo miradi iliyokamilika itatunzwa na kufanyiwa ukarabati wa mara kwa mara (*routine maintenance*).

e) Kamati inashauri Wizara kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) katika utendaji wake ili kupunguza gharama za matumizi yasiyo ya lazima.

f) Fedha zinazotengwa kwa ajili ya mafunzo ya watumishi zinaweza kusaidia kukuza weledi, kuongeza ufanisi na motisha kwa watumishi iwapo fedha hizo zitatolewa na kutumika inavyostahili. Serikali itumie fedha za mafunzo na matumizi mengineyo kuwapatia watumishi mafunzo ya ndani na nje ya nchi ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

g) Kamati ilibaini kwamba, makusanyo ya maduhuli katika mwaka unaoisha yamevuka lengo ambapo hadi kufikia Februari, 2022 Wizara na taasisi zake zilikuwa zimekusanya zaidi ya **asilimia 89**. Pamoja na hali hiyo, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara imepanga kukusanya maduhuli kwa ongezeko la asilimia **asilimia 3.55** tu ukilinganisha na Mwaka wa Fedha unaoisha. Kamati inashauri kwamba, Wizara itathmini upya vyanzo vya mapato pamoja na uwezo wa kukusanya mapato hayo. Kwa kufanya hivyo, Serikali itaweka

makadirio ya makusanyo ya maduhuli ambayo yako halisi kulingana na uwezo wake wa kukusanya.

3.2 Maoni na Ushauri Mahsusi

3.2.1 Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni yafuatayo katika fungu hili:-

a) Serikali iendelee kuimarisha mfumo wa utoaji haki nchini kwa kuendelea kutumia lugha ya Kiswahili katika uandishi wa sheria na shughuli za utoaji haki mahakamani.

b) Kamati imebaini kwamba kiwango kidogo cha ufaulu wa wanafunzi wanaohitimu katika Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo (*Law School of Tanzania*) ambapo tangu kuanzishwa kwa chuo hicho, ufaulu haujawahi kufika **asilimia 35**. Kamati imebaini pia kwamba, Serikali ilifanya tathmini kujua sababu za changamoto hiyo ambapo moja kati ya sababu kubwa ilikuwa ni uwezo mdogo wa wanafunzi wanaodahiliwa katika taasisi hiyo. Kamati inashauri kwamba, Serikali ifanye mapitio (*review*) ya mitaala, pamoja na vigezo vya wanafunzi kusoma taaluma ya sheria ili Taasisi hiyo iwe inadahili wanafunzi wenye sifa. Hata hivyo, mapitio haya yaende sambamba na nia ya Kamati kuona kwamba, idadi ya mawakili nchini inaongezeka ili kusaidia wananchi walio wengi kupata haki ya msaada wa kisheria (*the right to legal representation*).

c) Wizara ifanye jitihada za makusudi na kuratibu zoezi la kuajiri Mawakili wa Serikali ili kupunguza uhaba wa wataalamu hao katika idara na taasisi mbalimbali inazosisimamia. Zoezi hili liende sambamba na kutenga fedha za kutosha kuwapa mafunzo stahiki watumishi waliopo na watakaoajiriwa ili kuongeza ufanisi wa utendaji wao.

d) Kamati imebaini kwamba hakuna uelewa wa kutosha kwa watekelezaji wa sheria na jamii kwa ujumla kuhusiana na sheria mpya zinazotungwa. Hivyo basi, Kamati inashauri

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Serikali kutoa kipaumbele katika eneo hili kwa kutoa mafunzo ya kutosha kwenye eneo la sheria mpya zinazotungwa kwa wanasheria wake na jamii kwa ujumla ili kuboresha utekelezaji wa sheria hizo.

e) Kwa kuwa Kamati imebaini kwamba Serikali imechukua hatua muhimu na zenye tija katika kuboresha utendaji wa Mahakama kwa kujenga majengo mapya ya Mahakama. Kamati inapongeza hatua hiyo kwa sababu kwa muda mrefu Mahakama ilikuwa na majengo chakavu. Hata hivyo, Kamati inaishauri Wizara ya Katiba na Sheria kufanya uratibu kwa kushirikiana na Wizara nyingine husika ili taasisi zote ambazo zinahusika katika mnyororo wa utoaji haki zinapata fedha ili kuboresha miundombinu yake ikiwemo magereza, mahabusu na dawati la jinsia.

3.2.2 Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama

Mheshimiwa Spika, Kamati ina ushauri ufuatao katika fungu hili:-

a) Serikali itenge fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili Tume ya Utumishi wa Mahakama ijenge Ofisi katika Makao Makuu ya Nchi, Dodoma.

b) Kamati imebaini kwamba kuna uelewa mdogo katika jamii kuhusu kuwepo kwa Kamati za Maadili ya Maafisa wa Mahakama katika ngazi za mikoa na Wilaya. Hali hii inasababisha wananchi kushindwa kuwasilisha taarifa au malalamiko yao dhidi ya ukiukwaji wa maadili kwa Maafisa wa Mahakama. Hivyo basi, Kamati inashauri Tume ya Utumishi wa Mahakama kutenga fedha na kububni mbinu za kutoa elimu kwa umma kuhusu afua hizo.

c) Kamati imebaini kwamba, baadhi ya Kamati za Maadili za Mikoa na Wilaya hazitekelezi majukumu yake kwa ufanisi na weledi. Changamoto hii inatokana na baadhi ya Kamati hizo kuwa na Wajumbe wapya. Kamati inashauri Tume ya Utumishi wa Mahakama iandae na kutekeleza mpango

maalum wa kutoa elimu ya mara kwa mara kwa Kamati za Maadili za Mikoa na Wilaya.

3.2.3 Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao katika Fungu hili:-

a) Kamati ilibaini kwamba, hadi kufikia Februari, 2022, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilikuwa haijapokea fedha za miradi ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha unaoisha. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba inatoa fedha hizo, na kwamba katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Ofisi hiyo inapokea fedha za maendeleo kwa ukamilifu na kwa wakati.

b) Kamati inapongeza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Seriali kwa kuanza kutunga Sheria kwa lugha ya Kiswahili na kuendelea kutafsiri Sheria zilizopo zililizoandikwa kwa Kiingereza kwa Kiswahili. Kamati inashauri Serikali kuweka kipaumbele cha kutafsiri Sheria kwa Kiswahili hususan sheria zinazotumika katika jamii mara kwa mara. Mfano wa makundi ya sheria hizo ni sheria za usalama barabarani, kanuni za adhabu, sheria za kodi n.k.

3.2.4 Fungu 35 – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao:-

a) Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ndicho chombo kikuu kinachoweza kuisaidia Serikali kupunguza mlundikano wa kesi Mahakamani na mahabusu katika magereza na hatimaye kupunguza malalamiko ya wananchi kuhusu mfumo mzima wa hakijina nchini. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba Bajeti ya Serikali haitoi kipaumbele kinachostahili kwa chombo hiki ukilinganisha na mahitaji halisi ya kibajeti. Kamati inashauri kwamba, Serikali itathmini mahitaji ya ofisi hii na kuipa kipaumbele cha kibajeti kulingana na mahitaji muhimu ya Ofisi hii ikiwemo Fedha za Matumizi Mengineyo, na Fedha za Miradi ya Maendeleo.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

b) Kamati imebaini ukosefu wa vitendea kazi, upungufu wa watumishi, mazingira yasiyo rafiki na kukosekana kwa maslahi muhimu kwa watumishi wa ofisi hii ambavyo kwa pamoja vinachangia katika kucheleweshwaji wa haki nchini. Kamati inashauri Serikali itenge bajeti ya kutosha ili kuiwezesha ofisi hii kuboresha vitendea kazi, mazingira ya kazi pamoja na maslahi kwa watumishi kwa lengo la kuleta tija na ufanisi.

c) Kamati imebaini kuwepo kwa ucheleweshwaji wa mashitaka unaotokana na upelelezi wa mashitaka hayo kuchukua muda mrefu na kupelekea upelelezi kutokamilika kwa wakati. Kamati inashauri ofisi hii kuongeza nguvu katika kusimamia na kuratibu shughuli za upelelezi kwa ufanisi zaidi ili upelelezi uwe inakamilika kwa wakati

d) Kamati inapongeza Ofisi ya Mashtaka kwa kuongeza idadi ya Magereza na vituo vya polisi vilivyokaguliwa pamoja na kuwa na changamoto ya Covid 19. Hata hivyo, Kamati inashauri Ofisi hiyo kuendelea kutekeleza jukumu hili kwa ufanisi ili kuainisha changamoto zinazotokana na shughuli za upelelezi na kuweza kuzitatua kwa wakati.

e) Kamati imebaini kwamba Ofisi hii ina upungufu wa rasilimali watu. Hivyo basi, Kamati inashauri Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Ofisi hii waombe kibali cha ajira ili kuongeza watumishi wenye sifa za kuwa mawakili wa Serikali waweze kuendesha mashtaka.

3.2.5 Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora mambo yafuatayo:-

a) Kamati ilibaini kwamba kwa mwaka wa pili mfululizo Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora haijatangia kabisa Fedha za Ndani ili kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kamati inaishauri kwamba, kwa miradi ambayo inalenga kutoa elimu kwa umma, ni vyema Tume ikaanza utaratibu wa kutenga fedha za ndani ili kutekeleza miradi husika. Aidha, Tume ibuni mbinu za kutoa elimu kupitia majukwaa

ambayo yana hadhira kubwa ikiwemo mitandao ya kijamii ili kuwafikia watu wengi zaidi.

b) Kamati imebaini kuwa wananchi wengi hawana uelewa wa kutosha kuhusu haki za binadamu na haki zao za msingi kwa mujibu wa sheria za nchi. Kamati inashauri Serikali kutoa elimu kwa wananchi kuhusu haki hizo na misingi ya Utawala Bora ili kuwawezesha wananchi kuzijua na kuziadai haki hizo kwa mujibu wa sheria za nchi yetu.

c) Kamati imebaini kutokuwepo kwa uchunguzi wa kutosha wa mambo yanayohusu uvunjwaji wa haki za binadamu. Aidha, kukosekana kwa mrejesho wa ripoti za kiuchunguzi kunapelekea kuongezeka kwa matendo ya ukiukwaji wa haki za binadamu. Kamati inashauri Serikali iongeze jitihada za uchunguzi kuhusu wa mambo yanayohusu ukiukwaji wa haki za binadamu na itoe mrejesho wa ripoti za kiuchunguzi pale inapostahili ili kukemea vitendo viovu na kuboresha misingi ya utawala bora nchini.

d) Kamati inashauri Serikali iongeze juhudi katika kushirikiana na Mashirika ya Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, pamoja na Jumuiya ya Madola yenye uzoefu wa kutosha katika masuala ya ukuzaji na uteteaji wa haki za binadamu kwa lengo la kukuza misingi ya haki za binadamu na utawala bora hapa nchini.

e) Kamati inashauri tume ya haki za Binadamu kushirikiana na Tume ya Kurekebisha sheria kufanya mapitio ya sheria na kuainisha sheria zinazokinzana na sheria zinazotoa haki za binadamu na kuzifanyia marekebisho.

3.2.6 Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao:-

a) Tume itoe elimu kwa umma kupitia vipindi vya redio, runinga, vipeperushi, na majarida mbalimbali kuhusu sheria zinazofanyiwa marekebisho kwa lengo la kuwapa uelewa wanachi

b) Tume kwa awamu mbalimbali ifanye uchunguzi wa sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuainisha sheria zote zilizopitwa na wakati na kuzifanyia marekebisho ili ziendane na mazingira ya sasa ya Tanzania

c) Tume ifanye mapitio ya sheria inayoanzisha mabaraza ya Ardhi ya kata na ya Wilaya na kuona iwapo kuna ulazima kuyapeleka mabaraza haya chini ya Mahakama na sio chini ya Wizara ya Ardhi kama ilivyo sasa kwa lengo la kuwezesha usimamizi wa mabaraza haya. kuhakikisha utendaji kazi wake ni wa ufanisi kwa lengo la kupunguza migogoro ya ardhi hapa nchini

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Kwa umuhimu wao katika utendaji wa Kamati hii naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb. – Mwenyekiti
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb. – Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb.
4. Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mb.
5. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb.
6. Mhe. Joseph Anania Tadayo, Mb.
7. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb.
8. Mhe. Zainabu Athumani Katimba, Mb.
9. Mhe. Ng'wasi Damas Kamani, Mb.
10. Mhe. Lemburis Saputu Mollel Noah, Mb.
11. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb.
12. Mhe. Elibariki Immanuel Kingu, Mb.
13. Mhe. Omar Ali Omar, Mb.

14. Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb.
15. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb.
16. Mhe. Ahmed Juma Ngwali Dedi, Mb.
17. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb.
18. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb.
19. Mhe. Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mb.
20. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb.
21. Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb.
22. Mhe. Agnes Elias Hokororo, Mb.
23. Mhe. Luhaga Joelson Mpina, Mb.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Aidha, nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Geophrey Mizengo Pinda (Mb.), Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, kwa ushirikiano ambao ameupatia Kamati wakati wa uchambuzi wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndg. Mary Gabriel Makondo na akisaidiwa na Naibu Katibu Mkuu Ndg. Khatibu M. Kazungu. Aidha, namshukuru Mtendaji Mkuu wa Mahakama Prof. Elisante Ole Gabriel na watendaji wote wa Mahakama ya Tanzania na taasisi zilizo chini yake kwa ushirikiano ambao wameupatia Kamati.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nanelwa Mwiambi, *ndc* kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Shughuli za Bunge. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, *ndc*, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Yona Kirumbi na Ndg. Elihaika Mtui wakisaidiwa na Bi. Theresia Jacob kwa kuratibu Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi

ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb.

MWENYEKITI

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria

28 Aprili, 2022

SPIKA: Ahsante sana. Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, kwa niaba yake Mheshimiwa Issa Mtemvu. *(Makofi)*

MHE. ISSA J. MTEMVU K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kutoa pole kwako, kwa familia ya marehemu pamoja na wananchi wa Mkoa wa Rukwa kwa kuondokewa na mpendwa wetu, Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Irene Alex Ndiyamkama; na baada ya pole hizo kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama Fungu 40 kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022; na Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Naomba taarifa yote iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa Mujibu wa Kifungu cha 9(1)(c) cha Sheria ya Bajeti Na.11 ya mwaka 2015 pamoja na Kifungu cha 59 cha Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama Na.4 ya mwaka 2011, Kamati ya Bunge ya Bajeti ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mtendaji Mkuu wa Mahakama ili kujadiliana na kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kuwa majukumu ya Mahakama ya Tanzania yameainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama chombo kikuu cha kusimamia utolewaji wa haki nchini. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Ibara ya 107(a) fasili ya (1): *“Mahakama ndiyo chombo pekee chenye mamlaka ya mwisho katika kutoa haki kwenye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.”* Hivyo, ni wazi kwamba chombo hiki ni muhimu sana katika ustawi wa jamii na maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti ilifanya uchambuzi kuhusu utekelezaji wa bajeti na majukumu ya Mfuko wa Mahakama kuanzia mwezi Julai, 2021 hadi Mwezi Februari, 2022, pamoja na vipaumbele na masuala muhimu yanayopendekezwa katika Mpango wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha, 2021/2022: Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Mfuko wa Mahakama – Fungu 40 uliidhinishiwa na Bunge jumla ya Shilingi 153,228,859,000 . Kati ya fedha hizo Shilingi 53,066,756,000 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Mahakama; Shilingi 2,197,721,000 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, Shilingi 57,774,382,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC); na Shilingi 40,190,000,000 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Katika fedha za Maendeleo, Shilingi 39,100,000,000 ni fedha za ndani na Shilingi 1,090,000,000 ni fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Februari, 2022, Mahakama ilipokea jumla ya Shilingi 96,599,464,820.52/= ambazo ni sawa na asilimia 63 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha, 2021/2022. Kati ya fedha hizo, Shilingi 37,071,895,116.64/= kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC); Shilingi 38,891,112,902.56/= kwa ajili ya Mishahara ya Mahakama; Shilingi 1,039,152,000 kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

na Shilingi 19,597,304,801.32/= ni fedha za maendeleo, ambapo kati ya fedha hizo Shilingi 19,365,123,301.32/= ni fedha za ndani na Shilingi 232,181,500 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mahakama katika mwaka wa fedha, 2021/2022 ulipanga kukusanya maduhuli ya Shilingi 12,571,199,000 ambapo hadi kufikia mwezi Februari, 2022 kiasi kilichokuwa kimekusanywa ni Shilingi 5,136,157,946/= ikiwa sawa na asilimia 40.9 ya lengo la mwaka mzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kutoa fedha za Mfuko wa Mahakama kama zilizopitishwa na Bunge. Aidha, mwenendo wa utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama hadi kufikia mwezi Februari, 2022 ulikuwa ni asilimia 63, ambapo kwa kufanya hivyo kunaiwezesha Mahakama kutekeleza majukumu yake. Mwenendo huu unaonesha hadi kufikia mwezi Juni, 2022 Fungu hili linaweza kuwa limepokea fedha kwa zaidi ya asilimia 90 ya bajeti yake. Vile vile, pamoja na mwenendo huu bado jitihada kubwa zinahitajika za rasilimali fedha ili kuhakikisha kuwa Mahakama inafikia malengo yake ya utoaji wa huduma pamoja na ujenzi wa miundombinu yake. Hivyo, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuhakikisha kuwa Mahakama inaendelea kupewa fedha za Bajeti ili kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Mafanikio na Changamoto katika Utekelezaji wa Majukumu ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha, 2021/2022: Moja ya vipaumbele vya Mahakama katika mwaka wa fedha 2021/2022; moja, ilikuwa ni kuharakisha utatuzi wa mashauri ya kawaida na mkakati wa kumaliza mashauri ya muda mrefu; pili, kuboresha mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kama nyenzo muhimu ya kuboresha utoaji wa huduma; tatu, kuimarisha maendeleo ya rasilimali watu, ikiwa ni pamoja na mafunzo na nidhamu ya watumishi; nne, kuongeza ushirikiano na wadau wa haki jinai ili kuharakisha huduma ya utoaji haki; na tano, kuendelea kutekeleza mpango wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza vipaumbele hivyo, mafanikio yaliyofikiwa na Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ni kama ifuatavyo:-

(a) Utatuzi wa mashauri ya kawaida na mkakati wa kumaliza mashauri ya muda mrefu 186,442 yaliyokuwa yamesajiliwa mwanzoni mwa mwezi Julai, 2021 hadi Februari, 2022;

(b) Kuboresha mfumo wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kama nyenzo muhimu ya kuboresha utoaji wa huduma. Mifumo iliyoboreshwa ni pamoja na mifumo ya kielektroniki ya usimamizi na uendeshaji wa mashauri unaofanya kazi (*Comprehensive Case Management System*), Mfumo wa kuratibu na kuhifadhi taarifa za mali na vitendea kazi Mahakamani (*Asset Management System*), e-Wakili, na mifumo ya *video conference*;

(c) Kuimairisha uwezo katika ukaguzi na usimamizi wa shughuli katika ngazi zote za Mahakama, ambapo ukaguzi katika kanda 18 ulifanyika kwa asilimia 97; na

(d) Kuendelea kutekeleza Mpango (2021/2022 – 2025/2026) wa ujenzi na ukarabati wa Mahakama katika ngazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa miradi 37 katika ngazi mbalimbali za Mahakama.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka 2021/2022, Mahakama inaendelea kukabiliwa na changamoto zifuatazo:-

Moja, Uhaba na uchakavu wa Majengo ya ofisi na makazi; pili, ufinyu wa bajeti unaotokana na ukomo mdogo usiokidhi mahitaji ya Mfuko wa Mahakama; tatu, uhaba wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

watumishi wa kada mbalimbali; na nne, uhaba wa vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya mfuko wa mahakama kwa mwaka wa fedha, 2022/2023: Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Mfuko wa Mahakama umepanga kutekeleza majukumu yake ya kikatiba na malengo ya mpango mkakati na ya Kitaifa. Aidha, maeneo ambayo yamepewa kipaumbele ni yafuatayo: -

(a) Kuharakisha utatuzi wa mashauri ya kawaida na mkakati wa kumaliza mashauri ya muda mrefu (*backlog*);

(b) Kuboresha mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kama nyenzo muhimu ya kuboresha utoaji huduma;

(c) Kuimarisha uwezo katika ukaguzi na usimamizi wa shughuli za Mahakama;

(d) Kuendelea kutekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali;

e) Kuendelea na ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mahakama ya Tanzania ili kuhamia Dodoma; na

f) Kuongeza ushirikiano na wadau wa haki jinai na madai ili kuharakisha huduma ya utoaji haki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu makadirio ya bajeti ya mwaka 2022/2023. Katika Mwaka wa Fedha, 2022/2023 Mfuko wa Mahakama umepewa ukomo wa jumla ya Shilingi 160,275,825,000 . Kati ya fedha hizo Shilingi 61,017,018,000 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Mahakama; Shilingi 2,391,425,000 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA); na Shilingi 57,774,382,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Mengineyo (OC) na Shilingi 39,093,000,000 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ambapo kati ya fedha hizo Shilingi 36,091,000,000 ni fedha za ndani na Shilingi 1,091,000,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Fungu hili imeongezeka kwa shilingi 7,046,966,000 sawa na asilimia 4.6 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2021/2022 kutokana na ongezeko la mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapato katika mwaka wa fedha 2022/2023 Mahakama imepanga kukusanya maduhuli ya kiasi cha Shilingi 12,571,199,000 .

Mheshimiwa Spika, maoni na Mapendekezo ya Kamati; Utekelezaji wa Mpango wa (2021/2022 – 2025/2026) wa ujenzi na ukarabati wa Mahakama katika ngazi mbalimbali. Moja ya changamoto inazozikabili Mahakama ni pamoja na uhaba wa majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali, ili kutekeleza Mpango huo, Mahakama inahitaji kiasi cha Shilingi bilioni 15 kila mwaka kwa miaka mitano ili kukamilisha Mpango huo.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inatenga fedha za maendeleo kiasi cha Shilingi bilioni 15 kila mwaka ili Mahakama iweze kujenga Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Wilaya, Mahakama Kuu pamoja na nyumba za Majaji ili kusogeza huduma hii muhimu kwa wananchi.

Mheshiwa Spika, ili kuongeza tija na ufanisi kwa kuruhusu haki kutendeka katika Mahakama, Kamati inaishauri Serikali kupitia Mahakama kutekeleza Mpango wa kuwahamisha Majaji waliokaa katika vituo vyao kwa muda mrefu. Utaratibu unataka kuwahamisha Majaji na Mahakimu walau kila baada ya miaka 2 au miaka 3 ili kuondoa uwezekano wa kutoa haki kwa upendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni Mahakama kukaa kwenye majengo ya Taasisi nyingine. Utakumbuka kuwa moja ya shughuli kubwa ya Mahakama ni kutoa haki kwa raia na kwa usawa. Hata hivyo, bado kwa baadhi ya maeneo nchini Mahakama imepanga katika majengo ya taasisi nyingine.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Hali hiyo inaweza kuathiri uhuru wa utoaji haki kwani inaweza kusababisha kuwa na mgongano wa kimaslahi. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha kifedha Mahakama ili ijenge majengo yake yenyewe. Kwa kufanya hivyo itakuwa huru na haki itatolewa bila upendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uboreshwaji wa Mabaraza ya Kata: Mabaraza ya Usuluhishi yalianzishwa kwa Sheria Na. 5 Sura 216 ya mwaka 1985 kwa nia njema ya kusaidia utoaji haki katika maeneo ambayo hayajafikiwa na Mahakama, lakini mabaraza haya badala yake yamekuwa yakiongoza katika kuwanyima wananchi haki kutokana na baadhi yake kutawala kwa rushwa na kushughulikia kesi ambazo hawana mamlaka ya kisheria ya kuzishughulikia.

Aidha, ili kuongeza ufanisi na tija ya utendaji wa mabaraza haya, ni vyema Serikali ikayaunganisha na Mahakama ili kuruhusu utoaji haki.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza kuwa ni vyema Serikali ikarejea upya viwango vya posho za Wazee wa Mabaraza ambao wanalipwa shilingi 5,000 tu kwa kesi. Kiasi hiki ni kidogo sana ukizingatia muda unaotumika hadi kumaliza kesi.

Mheshimiwa Spika, aidha, kiwango hiki ukilinganisha na mfumuko wa bei pamoja na kuwa ni cha miaka mingi sana, kutokufanya marejeo ya viwango, hivyo kunaweza kusababisha mwanya wa rushwa na hivyo kuathiri utolewaji wa haki. Aidha, hatua ya kufanya marejeo itaongeza motisha, tija na ufanisi katika kazi za Mabaraza haya muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utolewaji wa haki unahusisha ofisi mbalimbali kama Vile Ofisi ya Mwendesha Mashtaka, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Tume ya Haki za Binadamu. Hivyo ni wazi kwamba endapo Mahakama pekee itaendelea kupiga hatua zaidi katika kufanya maamuzi ya mashauri yanayofika mbele ya Mahakama bila kuangalia kule ambapo ushahidi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

unakusanywa au utetezi unafanyika, ni wazi kwamba lazima kutakuwa na ucheleweshwaji. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuangalia mfumo mzima wa utolewaji haki kwa kutenga Bajeti ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuongoza vyema mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali; Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango; Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango; kwa ushirikiano wao kwa Kamati.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inamshukuru pia Prof. Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano ya Bajeti ya Mfuko Mkuu.

Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini na uweledi wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama. Naomba majina ya Wajumbe wa Kamati yaingie kwenye *Hansard* kama yanavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge, Bi. Nanelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo, pamoja na Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndg. Michael Kadebe kwa kuipatia ushauri wa kitaalamu Kamati hadi kukamilika kwa Taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama – Fungu 40, kwa Mwaka wa Fedha, 2022/2023 jumla ya Shilingi 160,275,825,000 kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA MAHAKAMA (FUNGU 40) KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Awali ya yote naomba kutoa pole kwako Mhe. Spika, Kwa Familia ya Marehemu pamoja na Wananchi wa Mkoa wa Rukwa kwa kuondokewa na mpendwa wetu Mbunge mwenzetu Mhe. Irene Ndyamkama. Baada ya pole hizo kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bajeti, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama (Fungu 40) kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/23.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 9 (1)(c) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015 pamoja na Kifungu cha 59 cha Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama Na. 4 ya mwaka 2011, Kamati ya Bunge ya Bajeti ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mtendaji Mkuu wa Mahakama ili kujadiliana na kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/23.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kuwa majukumu ya Mahakama ya Tanzania yameanishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama chombo kikuu cha kusimamia utolewaji wa Haki nchini. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Ibara 107(A)(1) Mahakama ndio chombo pekee chenye mamlaka ya mwisho katika kutoa haki kwenye Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania. Hivyo, ni wazi kwamba chombo hiki ni muhimu sana katika ustawi wa jamii na maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti ilifanya uchambuzi kuhusu Utekelezaji wa Bajeti na Majukumu ya Mfuko wa Mahakama kuanzia Mwezi Julai, 2021 hadi 3 Mwezi Februari, 2022, pamoja na vipaumbele na masuala muhimu yanayopendekezwa katika Mpango wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2022/23.

2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA MAHAKAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2021/22 Mfuko wa Mahakama – Fungu 40 uliidhinishiwa na Bunge jumla ya **Shilingi 153,228,859,000.00**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 53,066,756,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Mahakama, **Shilingi 2,197,721,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, **Shilingi 57,774,382,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), na **Shilingi 40,190,000,000.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Katika fedha za Maendeleo, **Shilingi 39,100,000,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 1,090,000,000.00** ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Februari, 2022, Mahakama ilipokea jumla ya **Sh. 96,599,464,820.52** ambazo ni sawa na **asilimia 63** ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2021/22. Kati ya fedha hizo, **Sh. 37,071,895,116.64** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), **Sh. 38,891,112,902.56** kwa ajili ya Mishahara ya Mahakama, **Shilingi 1,039,152,000.00** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto na **Shilingi 19,597,304,801.32** ni fedha za maendeleo, ambapo kati ya fedha hizo **Shilingi 19,365,123,301.32** ni fedha za ndani na **Shilingi 232,181,500** ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mahakama katika mwaka wa fedha 2021/22 ulipanga kukusanya maduhuli ya **Shilingi 12,571,199,000** ambapo hadi kufikia mwezi Februari, 2022 kiasi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kilichokuwa kimekusanywa ni **Shilingi 5,136,157,946** ikiwa sawa na **asilimia 40.9** ya lengo la mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kutoa fedha za Mfuko wa Mahakama kama zilizopitishwa na Bunge. Aidha, mwenendo wa utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama hadi kufikia mwezi Februari, 2022 ulikuwa ni **asilimia 63**, ambapo kwa kufanya hivyo kunaiwezesha Mahakama kutekeleza majukumu yake. Mwenendo huu unaonyesha hadi kufikia mwezi Juni, 2022 Fungu hili linaweza kuwa limepokea fedha kwa zaidi ya **asilimia 90** ya bajeti yake. Vilevile, pamoja na mwenendo huu bado jitihada kubwa zinahitajika za rasilimali fedha ili kuhakikisha kuwa Mahakama inafikia malengo yake ya utoaji wa huduma pamoja na ujenzi wa miundombinu yake. Hivyo, Kamati inaendelea kuisitiza Serikali kuhakikisha kuwa Mahakama inaendelea kupewa fedha za Bajeti ili kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Jedwali Na. 1. Mwenendo wa Bajeti wa Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2021/22

| Matumizi | Bajeti | Fedha zilizotolewa Hadi Februari | Asilimia ya Bajeti |
|--------------------------|------------------------|----------------------------------|--------------------|
| Mishahara Mahakama | 53,066,756,000 | 38,891,112,902.56 | 73.3 |
| Mishahara (JA) | 2,197,721,000 | 1,039,152,000 | 47.3 |
| Matumizi Mengineyo | 57,774,382,000 | 37,071,895,116.64 | 64.2 |
| Maendeleo Fedha za Ndani | 39,100,000,000 | 19,365,123,301.32 | 49.5 |
| Maendeleo Fedha za Nje | 1,090,000,000 | 232,181,500 | 21.3 |
| Jumla Kuu | 153,228,859,000 | 96,599,464,820.52 | 63.0 |

3.0. MAFANIKIO NA CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MFUKO WA MAHAKAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22

Mheshimiwa Spika, moja ya vipaumbele vya Mahakama katika mwaka wa fedha 2021/22, ilikuwa ni

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

- i. kuharakisha utatuzi wa mashauri ya kawaida na mkakati wa kumaliza mashauri ya muda mrefu;
- ii. kuboresha mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kama nyenzo muhimu ya kuboresha utoaji wa huduma;
- iii. kuimarisha maendeleo ya rasilimali watu, ikiwa ni pamoja na mafunzo na nidhamu ya watumishi;
- iii. kuongeza ushirikiano na wadau wa haki jinai ili kuharakisha huduma ya utoaji haki; na
- v. kuendelea kutekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya mahakama katika ngazi mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza vipaumbele hivyo, mafanikio yaliyofikiwa na Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2021/22 ni kama ifuatavyo:-

- a) Utatuzi wa mashauri ya Kawaida na mkakati wa kumaliza mashauri ya muda mrefu 186,442 yaliyokuwa yamesajiliwa mwanzoni mwa mwezi Julai, 2021 hadi Februari, 2022;
- b) Kuboresha mfumo wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kama nyenzo muhimu ya kuboresha utoaji wa huduma. Mifumo iliyoboreshwa ni pamoja na mifumo ya kielektroniki ya usimamizi na uendeshaji wa mashauri unaofanya kazi (Comprehensive Case Management System), Mfumo wa kuratibu na kuhifadhi taarifa za mali na vitendea kazi mahakamani (Asset Management System), e-Wakili, na mifumo ya video conference;
- c) Kuimarisha uwezo katika ukaguzi na usimamizi wa shughuli katika ngazi zote za mahakama, ambapo ukaguzi katika kanda 18 ulifanyika kwa asilimia 97; na
- d) Kuendelea kutekeleza mpango (2021/22 – 2025/26) wa ujenzi na ukarabati wa mahakama katika ngazi mbalimbali

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa miradi 37 katika ngazi mbalimbali za mahakama.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka 2021/22, Mahakama inaendelea kukabiliwa na changamoto zifuatazo: -

- i. Uhaba na uchakavu wa Majengo ya ofisi na makazi
- ii. Ufinyu wa bajeti unaotokana na ukomo mdogo usiokidhi mahitaji ya Mfuko wa Mahakama; iii. Uhaba wa watumishi wa kada mbalimbali; na
- iv. Uhaba wa vitendea kazi.

4.0. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MFUKO WA MAHAKAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa Fedha 2022/23, Mfuko wa Mahakama umepanga kutekeleza majukumu yake ya kikatiba na malengo ya mpango mkakati na ya kitaifa. Aidha, maeneo ambayo yamepewa kipaumbele ni yafuatayo: -

- a) Kuharakisha utatuzi wa mashauri ya kawaida na mkakati wa kumaliza mashauri ya muda mrefu (backlog);
- b) Kuboresha mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kama nyenzo muhimu ya kuboresha utoaji huduma;
- c) Kuimarisha uwezo katika ukaguzi na usimamizi wa shughuli za Mahakama; d) Kuendelea kutekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa Majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali;
- e) Kuendelea na ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mahakama ya Tanzania ili kuhamia Dodoma; na

f) Kuongeza ushirikiano na wadau wa haki jinai na madai ili kuharakisha huduma ya utoaji haki.

4.1 Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2022/23

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2022/23 Mfuko wa Mahakama umepewa ukomo wa jumla ya **Shilingi 160,275,825,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 61,017,018,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya 7 Watumishi wa Mahakama, **Shilingi 2,391,425,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA), **Shilingi 57,774,382,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Mengineyo (OC) na **Shilingi 39,093,000,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, ambapo kati ya fedha hizo **Shilingi 36,091,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 1,091,000,000** ni fedha za nje. Bajeti ya fungu hili imeongezeka kwa **shilingi 7,046,966,000** sawa na **asilimia 4.6** ukilinganisha na mwaka wa fedha 2021/22 kutokana na ongezeko la mishahara ya watumishi.

4.2 Maduhuli

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapato katika mwaka wa fedha 2022/23 Mahakama imepanga kukusanya maduhuli ya kiasi cha **Shilingi 12,571,199,000**.

5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

5.1. Utekelezaji wa mpango (2021/22 – 2025/26) wa ujenzi na ukarabati wa mahakama katika ngazi mbalimbali

Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto inazozikabili Mahakama ni pamoja na uhaba wa majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali. Ili kutekeleza mpango huo Mahakama inahitaji kiasi cha Shilingi. Bilioni 15 kila mwaka kwa miaka mitano (5) ili kukamilisha Mpango huo. Hivyo basi, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inatenga fedha za maendeleo kiasi cha Shilingi bilioni 15 kila mwaka ili Mahakama iweze kujenga mahakama za mwanzo,

mahakama za Wilaya, Mahakama kuu pamoja na Nyumba za Majaji ili kusogeza huduma hii muhimu kwa wananchi.

5.2. Kubadilisha vituo vya kazi kwa Majaji na Mahakimu

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza tija na ufanisi kwa kuruhusu haki kutendeka katika Mahakama. Kamati inaishauri Serikali kupitia Mahakama kutekeleza mpango wa kuwahamisha majaji waliokaa katika vituo vyao kwa muda mrefu. Utaratibu unataka kuwahamisha Majaji na Mahakimu walau kila baada ya miaka 2 au 3 ili kuondoa uwezekano wa kutoa haki kwa upendeleo.

5.3. Mahakama kukaa kwenye majengo ya Taasisi nyingine

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kuwa moja ya shughuli kubwa ya Mahakama ni kutoa haki kwa raia na kwa usawa. Hata hivyo, bado kwa baadhi ya maeneo nchini Mahakama imepanga katika majengo ya taasisi nyingine. Hali hiyo inaweza kuathiri uhuru wa utoaji haki kwani inaweza kupelekea kuwa na mgongano wa kimaslahi. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha kifedha Mahakama ili ijenge majengo yake yenyewe kwa kufanya hivyo itakuwa huru na haki itatolewa bila upendeleo.

5.4. Uboreshwaji wa Mabaraza ya Kata

Mheshimiwa Spika, Mabaraza ya usuluhishi yalianzishwa kwa Sheria namba 5 Sura 216 ya mwaka 1985 kwa nia njema ya kusaidia utoaji haki katika maeneo ambayo hayajafikiwa na mahakama, lakini mabaraza haya badala yake yamekuwa yakiongoza katika kuwanyima wananchi haki kutokana na baadhi yake kutawala kwa rushwa na kushughulikia kesi ambazo hawana mamlaka ya kisheria ya kuzishughulikia. Aidha, ili kuongeza ufanisi na tija ya utendaji wa mabaraza haya, ni vyema Serikali ikayaunganisha na Mahakama ili kuruhusu utoaji haki.

5.5. Posho za Wazee wa Mahakama

Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza kuwa ni vyema Serikali ikarejea upya viwango vya posho za wazee wa mabaraza ambao wanalipwa **shilingi 5,000** tu kwa kesi, kiasi hiki ni kidogo sana ukizingatia muda unaotumika hadi kumaliza kesi. Aidha, kiwango hiki ukilinganisha na mfumuko wa bei pamoja na kuwa ni cha miaka mingi sana. Kutokufanya marejeo ya viwango hivyo kunaweza kusababisha mwanya wa rushwa na hivyo kuathiri utolewaji wa haki. Aidha, hatua ya kufanya marejeo itaongeza motisha, tija na ufanisi katika kazi za Mabaraza haya muhimu.

5.6. Uimarishaji wa Mfumo mzima wa Utolewaji wa Haki

Mheshimiwa Spika, Utolewaji wa haki unahusisha ofisi mbalimbali kama Vile Ofisi ya Muendesha mashtaka, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Tume ya Haki za Binadamu. Hivyo ni wazi kwamba endapo Mahakama pekee itaendelea kupiga hatua zaidi katika kufanya maamuzi ya mashauri yanayofika mbele ya mahakama bila kuangalia kule ambapo ushahidi unakusanywa au utetezi unafanyika ni wazi kwamba lazima kutakuwa na ucheleweshaji. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuangalia mfumo mzima wa utolewaji haki kwa kutenga Bajeti ya kutosha.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuongoza vema mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, Kamati inamshukuru pia Prof. Elisante Ole Gabriel Mtendaji Mkuu wa Mahakama kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano ya Bajeti ya Mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati hii kwa umakini na uweledi wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama. Naomba kuwatambua wajumbe hao kama ifuatavyo;

1. Mhe. Daniel Baran Sillo, Mb Mwenyekiti
2. Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb M/Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Hassan Omar King, Mb Mjumbe
4. Mhe. Issa Jumanne Mtemvu, Mb Mjumbe
5. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb Mjumbe
6. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb Mjumbe
7. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb Mjumbe
8. Mhe. Joseph George Kakunda, Mb Mjumbe
9. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb Mjumbe
10. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb Mjumbe
11. Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb Mjumbe
12. Mhe. Jonas William Mbunda, Mb Mjumbe
13. Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb Mjumbe
14. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb Mjumbe
15. Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb Mjumbe
16. Mhe. Tarimba Gulam Abbas, Mb Mjumbe
17. Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mb Mjumbe
18. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb Mjumbe
19. Mhe. Halima James Mdee, Mb Mjumbe
20. Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb Mjumbe
21. Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb Mjumbe
22. Mhe. Mariam Nassoro Kisangi, Mb Mjumbe
23. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb Mjumbe

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii, pia kumshukuru Katibu wa Bunge Bi. Nanelwa Mwihambi, ndc kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo, pamoja na Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndg. Michael Kadebe kwa kuipatia ushauri wa kitaalamu Kamati hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato

na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama – Fungu 40, kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 jumla ya **sh. 160,275,825,000** kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Daniel Baran Sillo (Mb)

MWENYEKITI

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI

28 Aprili, 2022

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Issa Mtemvu.

Waheshimiwa Wabunge, nimeona wageni wengine wameingia hapo, lakini tangazo lao halijafika bado. Litakapofika, nitawatangaza.

Sasa tutaendelea na uchangiaji. Ninayo majina hapa ya Waheshimiwa Wabunge ambao wameomba kuchangia hoja hii. Tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama, atafuatiwa na Mheshimiwa Asha Juma Abdallah, na Mheshimiwa Joseph Tadayo, ajiandae.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria. Mchango wangu utajikita kwenye Fungu Na. 35 la Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa maana ya *DPP*.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeeleza nini imebaini kwenye Ofisi hii. Moja katika mambo makubwa ambayo imebaini ni kwamba Ofisi ya *DPP* ni Ofisi muhimu sana katika masuala ya utoaji haki, lakini bajeti ambayo imetengwa kwa ajili ya ofisi hii ni ndogo sana katika kukidhi mahitaji ya upatikanaji haki kwa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili hoja yangu ieleweke, naomba Watanzania wafungamanishe Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na dhana au Dira ya Tanzania ya kujenga uchumi kwa kupitia

viwanda na biashara. Utakubaliana nami kwamba moja ya vivutio vikubwa vya uwekezaji na biashara nchini ni utawala wa sheria. Kama hakuna utawala wa sheria, hatutaweza kuvutia uwekezaji wa aina yoyote nchini.

Mheshimiwa Spika, wataalam wanasema, hatuwekezi biashara pale ambapo pana utawala wa viongozi, bali pale ambapo pana utawala wa sheria. Hapa ni mkazo juu ya utawala wa sheria dhidi ya utawala wa viongozi. Tanzania tumepiga hatua kubwa sana kwenye eneo hilo. Awamu hadi Awamu Tanzania imefanya *transformation* kubwa kutoka kwenye utawala wa viongozi kwenda kwenye utawala wa sheria. Hilo limejdhahirisha sana katika utawala wa Awamu ya Sita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Awamu hii ya Sita, tumeona namna Mheshimiwa Rais ameendelea kuweka mkazo wa *ku-transform* mfumo wetu wa utawala ili tuwe na utawala wa sheria ambao utatoa haki kwa Watanzania wengi, lakini pia itafungua fursa za kukua kibiashara. Miongoni mwa mambo ambayo tumefanikiwa sana katika kipindi hiki kifupi; moja, ni zaidi ya Watanzania milioni moja na nusu wamepata huduma ya ushauri wa sheria katika Wiki ya Sheria. Haya ni mafanikio makubwa. Lingine ni uteuzi wa Majaji. Ili kutoa huduma, ni Majaji katika Mahakama ya Rufani tisa na kufanya jumla ya Majaji wote katika Mahakama ya Rufani kufikia 21. Ni hatua kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia kumekuwa na uteuzi wa Majaji katika Mahakama Kuu Majaji 21 wameteuliwa na hivyo Majaji katika Mahakama Kuu kufikia 82. Hii ni hatua kubwa sana katika utoaji wa haki nchini. Sasa tuna Mahakimu 245, hayo ni mafanikio makubwa sana katika Awamu hii. Siyo hayo tu, unaona kwamba Mahakama imepanua wigo wa utoaji haki na imewapeleka Mawakili sasa waweze kutoa huduma kwenye Mahakama za Mwanzo ili kuwafikia Watanzania walio wengi ambao wanategemea sana Mahakama hizi za Mwanzo ili kupata huduma ya upatikanaji wa sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye Mahakama zetu ni hatua kubwa sana ambayo ni

lazima tuiweke kwenye kumbukumbu za Taifa letu katika Awamu hizi zinazofuatana. Tumeona kuna mafanikio makubwa kwenye ujenzi wa majengo ya Mahakama, lakini pia Ofisi ya *DPP* imezidi kupanua huduma na sasa ina ofisi karibu katika Mikoa 26 za Kimahakama, lakini Wilaya 14. Hayo yote ni mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, nilitamani kabla sijatoa ushauri na mapendekezo yangu niwapongeze sana, kwanza Mheshimiwa Rais, Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan; Waziri wetu, Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbo, Naibu Waziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na timu nzima ya Wizara hii kwa kazi kubwa ambazo wamezifanya na mafanikio ni makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio haya makubwa ambayo nimeyaeleza bado tuna changamoto kubwa sana ya kuwafikia Watanzania walio wengi huko chini kwenye Mahakama za Mwanzo, ikiwemo Madaba, maeneo yote ya Songea Vijijini, hatuna huduma za uhakika zitakazompunguzia Mtanzania gharama ya kwenda kutafuta haki. Leo Ofisi ya *DPP* ina ofisi katika wilaya 14 tu, maana yake nini?

Mheshimiwa Spika, maana yake ni kwamba, katika wilaya nyingine za Tanzania zinazobaki mashitaka mengi yanaendeshwa na watu ambao hawana sifa ya kuendesha mashitaka. Askari Polisi ndio wanaokamata, Askari Polisi ndio wanaopeleleza, lakini ndio wanaoshitaki, haki ya Mtanzania itapatikana vipi kama utaratibu huu utaendelea hivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, rai yangu ni kuiomba Serikali iiongezee fedha Ofisi ya *DPP* ili iweze kufika katika maeneo yote ya Tanzania, ili iweze kuwafikia Watanzania wanyonge ambao uchumi wao unategemea kulinda haki zao za ardhi na maeneo ya biashara. Watu wananyimwa haki za kufanya biashara katika maeneo mbalimbali, lakini hawana namna ya kutafuta haki hizo kwa sababu wanaotakiwa kulisimamia hilo hawana uwezo wa kufika maeneo hayo.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, ninasema haya kwa Ushahidi. Mpaka mwezi Februari, 2022 kesi za jinai zilizosimamiwa na Ofisi ya *DPP* ni 42,138 katika hizo ni asilimia 28 tu ya kesi zote zimepatiwa ufumbuzi, hizo nyingine zote zimebaki. Tunawasaidiaje Watanzania kumaliza changamoto hizo kama Serikali haipo tayari kuongeza fedha kwenye Ofisi ya *DPP*? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, lakini naiomba Serikali iingalie ofisi hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Asha Juma Abdallah, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Thadayo. Mheshimiwa Neema Lugangira ajiandae.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Namshukuru Mungu kutujalia sote tukawa wazima hapa ili kujadili bajeti hii ya Katiba na Sheria kwa mwaka huu wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, napenda sana nianze kwa kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika pamoja na wasaidizi wako kwa jinsi mnavyoliendesha Bunge letu hili la Bajeti kwa ustadi na umahiri na uhodari.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea na mchango wangu kwa ruksa yako nichukue nafasi hii kumpongeza Mama yetu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa jinsi anavyopambana kuhakikisha kwamba Tanzania yetu hii inashamiri kiuchumi, uhusiano wa kimataifa na ustawi wa Tanzania yetu. Vilevile kusimamia utawala wa sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Katiba na Sheria na Msaidizi Waziri, pamoja na watendaji na taasisi zote zilizo chini ya Wizara hii. Na kwa dhati kabisa nampongeza *AG*, Dkt. Feleshi kwa jinsi anavyokuwa makini na kushirikiana na sisi muda wote, *he is never missed* kwa kweli, *AG* ni kiboko yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kuzungumzia kuhusu utendaji na maboresho kwenye Mahakama. Pongezi za Serikali kwa hatua ya kuboresha Mahakama. Kusema kweli Mahakama za kileo. zimejengwa, Mahakama za kwa mfano Mahakama Kuu Shirikishi Arusha ni Mahakama ya kupigiwa mfano, *facilities* zote za kisasa, za ki-*digital*, za kimaendeleo yote. Maana hata kama utataka kwenda *washroom* basi utatamani usitoke kwa jinsi ya hali ilivyokuwa nzuri pale Arusha.

Mheshimiwa Spika, na vilevile tumeweza kuona kwamba, nchi yetu inakwenda kama vile *supreme courts* za Marekani. Jengo letu la *supreme court* litakapokamilika hapa Dodoma litakuwa ni jengo la mfano kabisa. Nashukuru sana, kwa kuwa kazi nzuri inafanywa pia chini ya usimamizi wa Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Prof. Elisante, anafanya kazi nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna maendeleo makubwa sana. Bado kama wilaya 19 tu ndizo hazijapata majengo ya kileo. Sisi wenyewe na kamati yetu tumeshuhudia majengo ya kisasa kabisa ambapo hata mtu ukipelekwa huko hukumu itakayotoka unaweza ukaridhikanayo. Ukitizama siku za nyuma Mahakama zilivyokuwa utafikiri vijumba vya ndege, lakini sasahivi wilaya zote zimepata Mahakama nzuri na *furniture* za kileo. Unakwenda unapambana na ki-*dock* kile anachowekwa mtumiwa, mninga safi kabisa, ni kazi nzuri sana imefanyika. Samani za kileo na nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, lakini maboresho kwenye Mahakama yameweza kustawi zaidi kwa vile imetolewa huduma nyingine inayosema, *Sema Na Mahakama Saa 24*, ambapo watu wataweza kupeleka malalamiko yao na kujua *status* ya kesi zao na mambo yao mbalimbali. Kwa hivyo haya nasema ni maendeleo makubwa kwa sekta ya Mahakama ambapo mtu atapiga simu saa 24 na ataweza kupata maelezo.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kwa upande huu wa uboreshaji masuala ya Mahakama ni kweli fedha iliyotumika, wanasema wazungu ni *value for money*, tumeweza kuona sasa fedha iliyotumika ni kweli. Kwa sababu, kwa mfano Mahakama ile ya Mwanga ni ya kileo kabisa; kwa hivyo, tunapongeza jitihada hizi zinazofanywa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, nataka sasahivi niizungumzie Ofisi ya Mashitaka ambayo ni kilio kikubwa kwa kuwa imekuwa inapata fedha kidogo za kufanyia kazi zake. Kama tulivyosikia kwenye ripoti, kwenye ofisi hii kuna upungufu wa ofisi 125 ambazo haziko. Na tunaona jinsi watu wanavyopata malalamiko ya kucheleweshewa uchambuzi katika kesi zao na hivyo kubaki mahabusu kwa siku nyingi. Kwa hivyo, Serikali haina budi kuongeza fedha na kuongeza watendaji ili waweze kufanya shughuli hizi za ofisi ya mashitaka ziende kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ambayo ninataka kuzungumzia ni Chuo Cha Uongozi wa Mahakama (JA) kilichopo Lushoto. Chuo hiki kina mchango mkubwa kwa sekta ya sheria nchini, tumeona. Na mpaka sasahivi ni chuo ambacho hata majaji wapya wakiapishwa wanakwenda kule kupigwa msasa. Hata hivyo, chuo hiki kina majengo machakavu sana, miundombinu yake si mizuri na si *friendly* hasa kwa wale watu wenye mahitaji maalum. Kwa hivyo, tungependa Serikali ifikirie kuongeza fungu pale kukiboresha hiki kiwe cha kileo zaidi, ikiwezekana cha namna yake kwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, mabweni yamechoka sana. Tunayahitaji, tungependekeza kwa sababu, wanafunzi pale ni wengi na hivyo wanalazimika kwenda kupanga mitaani. Kwa hivyo, ni bora pakafikiriwa kuongezwa *hostels* mpya ili wanafunzi wapate malazi. Pamoja na hayo tunapongeza tumeweza kushuhudia jingo la *hostel* ya wavulana zuri sana ambalo linakidhi hata hawa watu wenye mahitaji maalum. Kwa hivyo, napongeza jitihada hizi zinazofanywa, na nalazimika tena kumpongeza sana mtendaji mkuu wa Mahakama, Prof. Elisante, anafanya kazi nzuri. Prof. Elisante

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

yeye ni mtendaji, yeye ni mhamasishaji, yeye vilevile ni kila kitu. *Thank you very much Professor. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa kwa ujumla wake Serikali iongeze mafungu kwenye mambo hayo mawili. Chuo hiki cha usimamizi huku Lushoto na Mkurugenzi wa Mashitaka.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi hayo ndio yangu. Ahsante kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Thadayo, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Lugangira. Mheshimiwa Luhaga Mpina ajiandae.

MHE. JOSEPH A. THADAYO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii ya kuchangia Wizara hii nyeti ya Katiba na Sheria. Awali ya yote niipongeze sana Serikali na Wizara, hasa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya kazi nzuri ambayo wamefanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria; kwa hiyo chini ya Kanuni ya 117 ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2020 nilipata fursa ya kutembea pamoja na kamati kuangalia miradi mbalimbali ya maendeleo ya Mahakama, iliyoko chini ya Wizara hii. Na kwa kweli, lazima nikiri kwamba, tumeona maendeleo makubwa sana katika uboreshaji wa sekta ya utoaji haki. Tumeona majengo ya kisasa kama ambavyo wenzangu wameeleza, tumeona uboreshaji mkubwa sana wa mifumo ya TEHAMA, pamoja na vitu vya kisasa kama hii *Call Centre* ambayo inawasaidia wananchi kupeleka kero zao.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumeona ushirikishwaji wa wadau wengine. Kwa mfano kitendo cha kuwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kupewa ofisi ndani ya Jengo la Mahakama, ili watu wote wanaohitaji msaada wa kisheria waweze kuupata palepale, hayo ni mapinduzi makubwa sana yanayodhihirisha kwamba Serikali ya Awamu ya Sita haifanyi maigizo kwenye suala zima la utoaji haki. Wako

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

serious kwamba, tunataka nchi iende kwa mujibu wa sheria.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na nadhani ni jambo ambalo linaeleweka tu kwamba, umuhimu wa sekta ya utoaji haji katika kukua kwa uchumi na utulivu wa nchi. Pamoja na kwamba, Mahakama haiuzi na kununua, lakini wanaouza na kununua hawataweza kuuza na kununua kama Mahakama na sekta ya utoaji haki kwa ujumla haifanyi kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo hayo mazuri tunaendelea kushauri tu kwamba, Serikali iendeele kuwekeza katika sekta ya utoaji haki. Kwa mfano, tumekwenda vizuri katika hivi vituo jumuishi ambavyo ni Mahakama Kuu na Mahakama za Wilaya, lakini bado hatujafika vizuri kwenye Mahakama za mwanzo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, katika Jimbo langu la Mwangi tumepata jingo la Mahakama la kisasa ambalo liko katika hatua za mwisho kabisa za umaliziaji, lakini kwenye kata 20 ambazo tunazo tuna Mahakama za mwanzo tano tu. Sasa wananchi wengi ni wanufaika zaidi wa Mahakama za mwanzo kuliko hizi Mahakama nyingine huku. Na bahati mbaya kwa utaratibu wa sheria ni kwamba, hata kama Mahakama ya Wilaya au Mahakama Kuu iko ukumbini mwako, lakini kama shauri lako inabidi lianze Mahakama ya Mwanzo lazima ukaanze kule. Kwa hiyo, pamoja na kuwa na hizi Mahakama nzuri za katika ngazi ya wilaya na Mahakama Kuu, lakini kuna umuhimu sana wa kuwekeza katika Mahakama za Mwanzo ambako ndiko wengi waliko.

Mheshimiwa Spika, na huku kwenye Mahakama za Mwanzo, au tuseme mahitaji ya watu wengi zaidi yanayoleta kero kubwa yako zaidi kwenye masuala ya ardhi na haya masuala ya familia, kama vile ndoa, talaka, mirathi, n.k.

Mheshimiwa Spika, sasa yako mambo mawili hapa ambayo ningependa kusema. La kwanza ni kwamba, hata tunapokwenda kuwekeza kwenye Mahakama za Mwanzo

tuangalie pia kuwajengea uwezo mahakimu walio kwenye Mahakama za Mwanzo juu ya suala zima la sheria za ardhi pamoja na hizi sheria zinazohusiana na mambo ya mirathi na ndoa, n.k. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na suala la sheria zinazohusiana na mambo ya mirathi na (*family law*), tatizo kubwa kwa kweli, liko kwenye sheria za kimila ambazo hasa ndizo ambazo zinasumbua watu wengi kule chini. Na bahati mbaya ni kwamba, utaratibu wa marekebisho wa zile sheria haupo kupitia Bunge, ila uko kupitia kwenye Halmashauri za wilaya kwa kupitia ile sheria inayoitwa *Judicature and Application of Laws ACT*, Kifungu cha 12. Ni vizuri hilo eneo likafanyiwa kazi kwa sababu, tunaweza tukawa na miundombinu mizuri sana ya Mahakama, n.k., lakini watu wanatumia sheria za kimila kufanya mambo yao huko na kwa hiyo mateso yataendelea huko chini wakati sisi huku tunabakia na *facilities* zetu ambazo ni nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili ni kuhusu suala hili la Mahakama za Ardhi. Tunaweza kuwa na Mahakama za Wilaya nzuri sana, lakini bahati mbaya ni kwamba, katika *level* ile ya chini ya wilaya ukiwa na shauri la ardhi lazima uende Mahakama ya ardhi kwanza. Sasa Mahakama za ardhi ziko chache sana, mimi nashukuru Napata Mahakama nzuri ya Wilaya, lakini bado ukiwa na tatizo la ardhi lazima uende Same kwa sababu Mahakama ya ardhi pale haipo. Ni vizuri ikafanyika kama ilivyofanyika kwenye Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Spika, hapo awali ilikuwa hata ukiwa kwenye Mahakama Kuu ilikuwa lazima uende kwenye Mahakama Kuu, Kitengo cha Ardhi, lakini nafikiri mwaka 2010 Mheshimiwa Jaji Mkuu alipitisha *circular*, tena namshukuru sana kwa hilo, kuzipa Mahakama Kuu mamlaka ya kusikiliza mashauri ya ardhi, Mahakama kuu zote, Kitengo cha Ardhi pamoja nah ii Mahakama Kuu ya kawaida. Kwa hiyo, nadhani tunahitaji kulifanya hilo katika ngazi ya wilaya pia, ili wananchi waweze kutumia huu uboreshaji ambao unafanyika. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la muhimu ni kwamba, tunaweza tukaboresha Mahakama sana lakini tusipoboresha wale washiriki na wadau wa hii sekta ya utoaji wa sheria kama magereza na polisi, bado matatizo yatakuwa palepale. Na kwa bahati mbaya sana lawama huwa zinaenda kwa Mahakama tu wakati ambapo Mahakama mwisho wa siku naweza nikasema ni kama *computer* kwa hiyo, lazima ulete *ui-feed*, iweze ku-*process* na kutoa matokeo. Sasa hayo yanafanyika kwa hawa wadau wengine kama polisi, n.k. Kwa hiyo, ni vizuri maboresho haya yanapofanyika kwenye Mahakama yaende pia kwenye maeneo mengine.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. JOSEPH A. THADAYO: Mheshimiwa Spika, hivi ni kengele ya kwanza au ya pili? Ya kwanza, ahsante.

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa nasisitiza hilo kwamba, ni vizuri maboresho haya yanapokwenda kwenye Mahakama yaende pia kwa hawa wadau wengine. Ukienda kwenye baadhi ya magereza, kama Gereza la Kirumi lililoko katika jimbo langu kwa kweli hali ni ya kusikitisha. Jengo lenyewe ni dogo na ardhi ni ndogo pia, hawana hata mahali pa kupanuka au hata pa kuendesha shughuli kilimo, lakini pia hawana magari na vitu vingine. Kwa hiyo tusipoboresha hawa wadau ni kwamba hata Mahakama zenyewe zitakuwa haziwezi kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, la mwisho nizungumzie kuhusu suala la utoaji wa elimu kwa wananchi juu ya matumizi ya haki zao kwenye Katiba na Sheria nyingine.

Mheshimiwa Spika, naona kengele imelia; niombe tu kuunga mkono hoja pamoja na kwamba, nilikuwa na hoja ya muhimu kidogo kwenye eneo hilo. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Neema Lugangira, atafuatiwa na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina. Mheshimiwa Reuben Kwagilwa ajiandae.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii. Napenda kuanza kwa kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan, kwa dhamira yake ya dhiti ya kuhakikisha anaweka mazingira wezeshi yatakatayosababisha kufikia usawa wa kijinsia katika siasa hapa nchini kwetu Tanzania. Nasema hivi kwa sababu, ndani ya mwaka mmoja wa uongozi wake Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan, ameunda Kikosi Kazi cha Taifa ambacho kimepewa jukumu la kupokea maoni na kutoa ushauri juu ya hali halisi ya demokrasia ya vyama vya siasa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, na ninakumbuka kati ya vitu ambavyo amekuwa akisisitiza kwa kikosi kazi hiki ni kuhakikisha kwamba, wanaangalia pia kwa jicho la kipekee suala zima la usawa wa kijinsia kwenye siasa kuanzia kwenye vyama vya siasa vyenyewe. Nami nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan juu ya umuhimu wa kufanya hivi kwa sababu, kwa mujibu wa Ripoti ya Uchaguzi Mkuu Tanzania ya Tume ya Uchaguzi *NEC* kati ya wagombea 11,933 waliogombea nafasi mbalimbali kuanzia Urais, Ubunge, Udiwani, katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015 ni asilimia 7.5 tu ndio walikuwa wanawake ilhali idadi ya wanawake waliojiandikisha kupiga kura ni asilimia 53 ya wapiga kura wote.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili. Takwimu za Tume ya Taifa ya Uchaguzi (*NEC*) zinaonesha pia asilimia kubwa ya wanawake waliojitishwa na vyama vyao kugombea nafasi mbalimbali za uchaguzi huwa wana fursa kubwa zaidi ya kushinda.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, mwaka 1995 CCM ilikuwa na wagombea wanawake saba kwenye majimbo na wanawake saba wote walishinda. Mwaka 2000 wanawake wa CCM ambao waligombea kwenye majimbo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

walikuwa 13 na kati ya hao 12 walishinda. Mwaka 2005 kulikuwa na wagombea wanawake 19 na kati ya hao 17 walishinda. Mwaka 2010 kulikuwa na wagombea 24 na kati ya hao wagombea 19 walishinda. Mwaka 2015 kulikuwa na wagombea 24 na kati ya hao 18 walishinda kwa upande wa CCM na kwa upande wa CHADEMA kulikuwa kuna wagombea 13 na sita walishinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii inadhihirisha kuwa wanawake wana uwezo mkubwa sana wa kushinda kwenye chaguzi endapo watateuliwa. Hivyo, dhamira ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ya kufikia usawa wa kijinsia inawezekana kabisa endapo tutaweka mikakati thabiti ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaeleza wazi kabisa kuwa binadamu wote ni sawa mbele ya sheria na kila mwananchi anayo haki ya kushiriki katika masuala ya umma, yakiwemo ya uongozi wa Taifa. Aidha, Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019 imegusia umuhimu wa vyama vya siasa kuzingatia masuala ya usawa wa kijinsia wanapotunga na kutekeleza sera zao, wanapoteua wagombea kwa ajili ya uchaguzi na uchaguzi wa viongozi ndani ya vyama.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na kwamba, sheria ya vyama vya siasa imeweka mazingira haya wezeshi, bado matakwa haya yanakuwa ni magumu kutekelezeka kwa sababu, yanamfanya Msajili wa Vyama vya Siasa anakosa meno ya kuvilazimisha vyama vya siasa vitekeleze usawa wa kijinsia. Kwa hiyo, ili tuweze kufikia dhamira ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ya kuwa na usawa wa kijinsia kwenye siasa, yapo mambo ya msingi ambayo lazima yafanyike. Kwa hiyo ningependa kuishauri Serikali yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza Sheria ya Vyama vya Siasa liwekwe takwa la kisheria kwamba kila chama cha siasa kiwe kina sera ya usawa wa kijinsia. Jambo la pili, kama ambavyo kwenye Katiba na kama ambavyo kwenye Sheria ya Serikali

za Mitaa pia kwenye Vyama vya Siasa viweke kiwango ambacho aidha kati ya asilimia fulani ya wagombea ambao watateuliwa na Vyama vya Siasa wawe wanawake. Vilevile katika mapato ambayo Vyama vya Siasa wanapata kupitia ruzuku, Vyama vya Siasa viweze kutenga kiwango fulani cha fedha ambacho kitakwenda kuwainua na kuwajengea uwezo na kuwasaidia wagombea wanawake.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni katika Sheria ya Uchaguzi huwa kunatokea matendo mengi ya ukatili wa kijinsia wa aina mbalimbali ikiwemo ukatili wa kimtandao pamoja na matusi na kufedheheshwa wakati wa kipindi cha kampeni wakati wa uchaguzi na hasa baada ya uchaguzi. Kwa hiyo, Sheria ile pia ya uchaguzi iweke wazi adhabu ambazo zitatolewa pale ambapo kutakuwa kuna udhalilishaji na ukatili wa kijinsia wa aina yoyote ile kwa wagombea wanawake. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Neema Lugangira kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Salome Makamba.

T A A R I F A

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa mzungumzaji Mheshimiwa Neema Lugangira kwamba, Sheria ya Uchaguzi inataka uchapofanyiwa makosa yoyote ya kimaadili upeleke kama ni kosa la jinai kwa sababu udhalilishaji wa kijinsia ni kosa la kijinai, unatakiwa upeleke kwenye mfumo wa kijinai ambao kiuhalisia inaweza ikachukua mpaka uchaguzi unaisha bado kosa lile halijafikiwa hatma. Kwa hiyo, nakubaliana naye kabisa kwamba Sheria ya Vyama vya Siasa na Sheria ya Uchaguzi iseme *clear* kama kumetokea kosa la jinai, basi mtu aliyemfanyia mwenzie kosa la unyanyasaji wa kijinsia apewe adhabu kupitia Kamati ya Maadili ambayo inasimamia uchaguzi na moja kati ya adhabu hizo ziwe *strict* iwe ni mtu huyo kuenguliwa katika kugombea.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana nae kabisa. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Neema Lugangira.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwa kumalizia naomba kusisitiza na kuishauri, nashukuru sana naipokea taarifa hiyo kwa mikono miwili.

SPIKA: Ngoja. Mheshimiwa Neema mimi ndiyo naongoza kikao usiwasikilize hao wanakupoteza, kwa sababu mimi sijakuuliza kwa sababu yeye alichofanya hapo amechangia hajakupa wewe taarifa. Mheshimiwa Neema Lugangira malizia mchango wako.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwa kumalizia napenda kusisitiza na kuishauri Serikali kwamba ilete ile Sheria ya Vyama vya Siasa na iifanyie maboresho ili Msajili wa Vyama vya Siasa aweze kuwa na meno ya kuvismamia Vyama vya Siasa vyenyewe kutekeleza na kuimarisha na kufikisha usawa wa kijinsia kwenye siasa. Hii ni pamoja na kuhakikisha kwamba wanaweka angalau asilimia fulani ya wagombea katika nafasi zote za uchaguzi kuwa wanawake, pia Vyama vya Siasa viwe vina sera ya usawa wa kijinsia na vilevile katika Sheria ya Uchaguzi iweke wazi adhabu ambazo zitachukuliwa pale ambapo mgombea yeyote mwanamke iwe katika mchakato wa kampeni, uchaguzi na hata baadaye anapofanyiwa aina yoyote ya ukatili wa kijinsia, ikiwemo wa kimtandao ni hatua gani zitachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina atafuatiwa na Mheshimiwa Reuben Kwagilwa Nhamanilo, Mheshimiwa Agnesta Lambat Kaiza ajiandae.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii ambayo umenipa na kwa sababu ya changamoto ya muda pia mchango wangu nitaupeleka kwa maandishi

Mheshimiwa Spika, kwa dakika hizi chache nilizopata niseme kwamba tuko leo kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya sekta muhimu sana ya Wizara nyeti ya Katiba na Sheria ambako tunaenda kuwahakikishia wananchi wetu kwamba haki itaendelea kutolewa pia haki itaendelea kupatikana kwa wakati na rasilimali zao za umma zitaendelea kulindwa.

Mheshimiwa Spika, bado tuna changamoto nyingi sana kufikia haki hizi kutolewa sawasawa.

Moja, kuna baadhi ya Watendaji wa Serikali ambao wanavunja Katiba na wanavunja na Sheria wakati wa kutekeleza majukumu yao.

Pili, bado kumekuwepo na usiri mkubwa sana kwa mikataba inayoingiwa na Serikali kwa niaba ya wananchi.

Tatu, bado kuna ucheleweshaji mkubwa wa maamuzi ya Mahakama na taasisi zingine ambazo zimepewa jukumu la kutoa haki.

Nne, maeneo mengi muhimu ya kiuchumi na kijamii hayajatungiwa sheria na hivyo kutumia matamko ya Viongozi katika kutoa uelekeo wa nini kifanyike katika eneo husika.

Tano, ni upendeleo na kukosekana kwa uwiano wa utoaji wa adhabu zinazotolewa katika baadhi maeneo ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, haya yasipofanyiwa tathmini vizuri tutaendelea kupiga *mark time* kwa sababu yana madhara makubwa sana katika uchumi wetu tunaousimamia. Tunasema tu kirahisi kwamba Mahakama imechelewesha maamuzi au Taasisi iliyopewa dhamana ya kutoa haki imechelewesha maamuzi, lakini madhara yake ya maamuzi hayo kwenye Taifa ni yapi, madhara hayo ya kuchelewa kwa maamuzi kwa mtu aliyetakiwa kuipata hiyo haki ni yapi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, tunasema tu kiurahisi kwamba mikataba inaungiwa kwa usiri na inatunzwa kwa usiri, lakini madhara ya kutunza mikataba kwa usiri kama Taifa ni ipi. Tunakuwa kwenye changamoto kubwa za namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, niweze tu kutoa mfano wa madhara makubwa sana ambayo tunayapata kutokana na ucheleweshaji wa maamuzi wa kesi katika Mahakama. Hapa tunakumbuka kwamba tulikuwa na tatizo la pingamizi za kikodi la Shilingi Trilioni 360, hili jambo lililalamikiwa na Bunge hili, hili jambo lililalamikiwa na mimi mwenyewe binafsi hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa ya CAG ya mwaka 2020/2021 inasema kwamba Mahakama hizi zimehitimisha haya mashauri na katika hitimisho Trilioni 5.65 jumla ya kesi 54 zenye thamani ya Shilingi Trilioni 5.65 zimeamuliwa na Mahakama, Serikali pamoja na wadau wa makampuni ya madini wamekabidhiwa kwenda kufanya mjadala wa namna ya kuhitimisha hili suala. Kesi zenye thamani ya Shilingi Trilioni 343.5 zenyewe zimerudishwa TRA kwa majadiliano, na kesi zenye thamani ya Shilingi Trilioni 5.19 zenyewe bado zinaendelea katika Bodi na Baraza la Rufani za Kodi.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa zilizopo hivi sasa ni kwamba tayari Serikali imehitimisha mjadala huu na imekubaliana kupokea Dola za Kimarekani Milioni 300 ambayo badala yake ukibadilisha nadhani ni kama Bilioni 692.61.

Mheshimiwa Spika, hiki kidogo kilichopatikana ni cha kupongeza, nami kabisa nataka nipongeze na Bunge lako hili Tukufu kwa kulisimamia hili jambo, tumeweza kupata hizo Bilioni 692.61 jambo ambalo hapa tuliambiwa hizi fedha ni za mchongo, haya makampuni ya madini madeni ya nyuma hatuwezi kulipwa kwa hiyo tunapoteza muda. Fedha hizi tumezipata leo Bilioni 692.61 ni suala la kujivunia sana.

Mheshimiwa Spika, hapa namkumbuka tingatinga Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alivyosimama kidete kuhakikisha kwamba hizi fedha za Watanzania zinapatikana,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

watu wakasema haziwezi kupatikana lakini dunia nzima aliambia na akaihakikishia na leo Taifa limepata Bilioni 692.61.

Mheshimiwa Spika, nakubali kabisa kwamba ndiyo maana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alimteua Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuwa Makamu wa Rais Awamu ya Kwanza na Awamu ya Pili, alimuona uwezo wake na ndiyo maana leo hii amekuja kulisimamia hili kwa kauli yake aliyoisema kazi iendelee.

Mheshimiwa Spika, jambo moja lingine pamoja na mafanikio haya tuliyoyapata lakini suala la kujuliza hawa wenzetu walioenda kwenye *negotiation* Mahakama zilisema Trilioni 5.65 zinaweza kupatikana na Serikali iende ikajadiliane walikubaliye kupokea Milioni 300 ambayo ni Bilioni 692 tu wakati Mahakama hizi za Bodi ya Rufaa za Kodi, Bodi pamoja na Baraza zilisema kwamba Trilioni 5.65 zinaweza kupatikana kama kodi, kwa nini tupate Bilioni 692.65.

Mheshimiwa Spika, ninaomba eneo hili lina changamoto kubwa na ninashauri na kulishawishi Bunge lako likubali tuunde Tume Teule ya Bunge ikachunguze suala hili, kwanza *negotiation* timu hiyo ilifikiaje maamuzi ya kupokea Bilioni 692.61, pia ikaangalie uhalali wa majadiliano hayo na kile ambacho kilichopatikana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni hapo ambapo bado ukiondoa sasa hivi kesi za makinikia kwa sababu ni karibu zote zimeondolewa mahakamani. Ukiondoa hizo, bado tunabakiza kesi zenye thamani ya Shilingi Trilioni 5.19 za makosa tu mbalimbali, sasa hivi ukataji wa rufaa kwenye bodi hizi na Mabaraza ya Kodi za Rufaa yamefikia wastani wa Trilioni Mbili kwa mwaka, tukiruhusu hili likaeendelea na tukaendelea kuchelewesha hizi kesi? Tutajikuta watu wote watatufungulia kesi au watatukatia rufaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa kama leo imefikia Trilioni Mbili inakatiwa rufaa Mahakamani na wadau hawa wa kodi, ni lazima tuhakikishe kwamba kesi zinamalizika kwa wakati,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

sababu za kuchelewesha kesi eti Mabaraza hayana pesa, sababu za kuchelewesha kesi eti kwa sababu mabaraza haya hayana watumishi! Hili ni jambo ambalo halingii akilini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, eneo ambalo unaweza kwenda kukusanya mapato siku hiyo hiyo kesi zikiamuliwa, haki za wale waliokata rufaa zikasikilizwa, pia haki ya Serikali kupata kodi yake na yenyewe ikaweza kupatikana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho kutokana na changamoto hii ya muda ni usiri mkubwa wa mikataba ambayo Serikali inaingia. Mfano mmoja wa usiri wa mikataba unavyoliathiri Taifa letu ni utekelezaji wa bwawa la Mwalimu Nyerere, utekelezaji wa bwawa la kufua umeme la Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Spika, nizungumze hapa kwa kusema kabisa kwamba maeneo haya ya kimkataba yana changamoto nyingi na ndiyo maana taasisi zetu za kiuchunguzi *CAG*, *PPRA* pamoja na *PCCB* wote wamekuwa wakilalamikia maeneo haya ya kimkataba kuwa na changamoto nyingi sana za ubadhirifu wa fedha za umma, changamoto za wizi wa fedha za umma, changamoto za ufisadi wa fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa Bwawa la Mwalimu Nyerere na mkataba wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, hivi majuzi hapa tumetangaziwa kwamba mkataba huu utamalizika baada ya miaka miwili ijayo, lakini ndani ya mkataba iko *clear* kwamba kuna Billioni 260 ambazo ni *CSR* lakini Mkandarasi akichelewesha mkataba wetu anapaswa kulipa asilimia Kumi. Kwa hiyo, kama amechelewesha Mkandarasi kwa miaka miwili anapaswa kutulipa shilingi trilioni 1.3.

Mheshimiwa Spika, kwa nini haya mambo hayajawekwa wazi katika hili jambo? Tunamdai bilioni 260 za *CSR*, tunamdai ucheleweshaji wa miaka miwili ambayo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ni Trilioni 1.3. Kwa nini haya mambo yana usiri gani? Siri hizo zinawekwa kwa ajili ya kumlinda nani?

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

SPIKA: Haya ahsante sana. Mheshimiwa Reuben Kwagilwa Nhamanilo atafuatiwa na Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, Mheshimiwa Dkt. Felesh Mbugi - Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ajiandae.

MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia kwenye Wizara hii ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, moja kati ya maeneo ambayo yanahitaji sana kusaidiwa ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwenye maelezo yao kwenye Kamati mbalimbali ambazo wamefika na kwa mujibu wa taarifa ya Kamati yetu ya Bunge inayosimamia Wizara hii ya Katiba na Sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inahitaji ipewe fedha kwa ajili ya kwanza, mafunzo maalum kwenye maeneo ya Uandishi wa Sheria; Pili, kwenye eneo la masuala ya utawala; na Tatu, ni katika eneo la mikataba. Kwamba wanahitaji wapewe fedha kwa ajili ya mafunzo maalum kwenye hayo maeneo matatu niliyoyataja.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nisizungumzie hili la Uandishi wa Sheria na naomba pia nisizungumzie hili la masuala ya utawala, nataka nizungumzie hili la eneo la mikataba.

Mheshimiwa Spika, kutoiwezesha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kutoipatia fedha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili wataalam wake wakapate mafunzo kwenye eneo hili la mkataba ni gharama kubwa sana kwa nchi yetu. Fedha ambazo walikuwa wameomba Milioni 300, kutokuwapa Milioni 300 ni gharama kubwa sana kwa nchi yetu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, wakati naendelea kuelezea nitatoa mfano kwa nini ni gharama sana kwa nchi yetu, kwa maana hiyo nimesimama hapa siyo tu kuchangia, lakini kulishawishi Bunge kwamba ni lazima tusimame kidete kuhakikisha kwamba Serikali inapeleka fedha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuwapeleka Wataalam wetu wajifunze mambo ya mikataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusipo-*train* watu wetu kwenye eneo hili la mikataba nchi yetu itashindwa kunufaika na rasilimali tulizonazo. Hivi sasa kama Taifa tunajielekeza kwenda kuwekeza kwenye *LNG*, tunajielekeza kwenda kuwekeza kwenye Uchumi wa *Blue* ambao ni Uchumi wa Bahari. Kote huku tutatakiwa kuingia mikataba mbalimbali, tusipoiwezesha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Sheria, tutaishia kuwa watazamaji na rasilimali zetu hatutanufaika nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano mmoja tu ili niijenge hoja yangu vizuri na Bunge hili liweze kunielewa kwa nini nasisitiza tupeleke fedha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Milioni 300 iliyokuwa imeombwa na majibu ya Serikali yamekuwa tu ni mepesi, eti ukomo wa bajeti umefikia hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano ninaotaka kuutoa ni kwamba, majuzi Serikali yetu iliingia mkataba na kampuni ya *Baker Botts* ya Uingereza kwa ajili ya kutusaidia ile *Government Negotiation Team* itakayopatikana, kwenye hili nimshukuru sana Mheshimiwa Rais na nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kumteua Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi kuwa Mkuu wa *Government Negotiation Teams* ambazo zitakuwa zinatengenezwa. Sasa kampuni hii ya *Baker Botts* ikitufanyia kazi kwa miaka miwili tunailipa Dola Milioni Tatu na Nusu hiyo ni takriban Bilioni Nane ya kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunafanya hivyo kwa gharama tu ya kushindwa ku-*train* watu wetu! Umeombwa Milioni 300 unashindwa ku-*allocate*, halafu uko *willing* kulipa Bilioni Nane

kwa kampuni moja kwa mkataba mmoja, *this is ridiculous.*
(Makofi)

Mheshimiwa Spika, tunaingia mkataba wa aina hiyo tukiwa na *facts* hizi zifuatazo: Nchi yetu ina Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali toka mwaka 1961 miaka 60 sasa; Nchi yetu imeshakuwa na *Geology Department* kwenye University of Dar es Salaam toka mwaka 1974 *which means* tuna wataalam wa *geology*, tuna wataalam wa mambo ya *Oil and Gas* na ambao pengine hawapo nchini kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, nilibahatika wakati mmoja kwenda *Texas* - Marekani nikakutana na Watanzania wengi sana wenye utaalam wa mambo ya *Gas and Oil*, sasa tunapoingia mikataba hii halafu kwa kisingizio tu cha kusema eti hatuna wataalam! Tusiwe tunajiangalia kwenye Wizara za Serikali kwamba kama hatuna mtaalam ndiyo tuna-*assume* nchi nzima haina wataalam. Tujengeni utamaduni wa kuwatumia watanzania wenzetu ambao wana ujuzi hata kama wako nje ya nchi, *we can access them!* (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naongea haya tumeingia mkataba huu tukiwa na *TPDC*, Shirika ambalo lina wataalam wa *Oil and Gas*, Shirika lipo toka mwaka 1969, lina miaka 53 tunaongelea jambo hili tukiwa tunayo *Faculty of Law* ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambayo ilianza hata chuo chenyewe kabla hakijaanza mwaka 1961, ina miaka 61.

Mheshimiwa Spika, wataalam wote hawa tunao wamefika mpaka *level* ya PhD, eti leo kwenye mkataba Watanzania hatuwezi kusimama kusema mpaka tutafute mtu atusemee, atufundishe cha kusema, atufundishe ku-*negotiate*, ilihali tuna wataalam wa kwetu! Tunalipa fedha halafu tumeacha kupeleka halafu tumeacha kupeleka bajeti kwa wataalam wetu kuwa-*enhance what is this?* Tumuungeni mkono Mheshimiwa Rais yeye ameshaonyesha njia nasi wasaidizi wake twendeni tumuunge mkono.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapa, nakushukuru sana kwa nafasi. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Agneta Lambert Kaiza atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria ajjandae.

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili namimi niweze kuchangia machache katika Wizara hii ya Katiba na Sheria. Kabla sijaenda katika mchango wangu wa leo, naomba nitumie nafasi hii kwanza kabisa kumpongeza Waziri wa Katiba na Sheria, Naibu Waziri Mheshimiwa AG pamoja na Mtendaji Mkuu wa Mahakama kwa kazi nzuri kwa kweli ambayo wanaifanya. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria, nimeshiriki katika ziara kwenda kukagua miradi ya maendeleo iliyopo chini ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba kwa macho yangu nimeona *value of money* na nichukue nafasi hii kuwapongeza kwamba fedha ambazo zimetengwa, hakika Mahakama wamezitendea haki na *value for money* inaonekana kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo sasa, niende kwenye mchango wangu ambao utakijita kwenye Fungu namba 55 kwa maana ya Tume ya Haki za Binadamu. Tume ya Haki za Binadamu ndicho chombo pekee ambacho kimeundwa na Serikali ili kuhakikisha kinalinda, kinasimamia haki zote za binadamu nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa lugha nyingine ikiwa kuna namna yoyote ya haki za binadamu kutokufuatwa au kuvunjwa, nchi haiwezi kuwa katika hali ya usalama. Nayasema haya ili kuonesha namna gani ambavyo chombo hiki au Tume hii ya Haki za Binadamu ni chombo muhimu sana, lakini kwa masikitiko makubwa sana niseme Tume hii imekuwa ni Tume mfu. Nayasema haya na niliyasema hata ndani ya Kamati yangu ya Katiba na Sheria, nikasema Tume

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hii ni Tume ambayo imekuwa ikionekana au naweza nikasema imekuwa ikifufuka wakati wa bajeti kama hizi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Tume hii haisikiki kabisa huko kwa wananchi ambapo inapaswa kusikika. Tume hii imeshindwa kutekeleza wajibu wake wa msingi ambao umeidhinishwa au ni jukumu lake la kimsingi kikatiba kuhakikisha wanasimamia na wanalinda haki za binadamu zisivunjwe. Pamoja na majukumu mengine Tume hii ina wajibu wa kutembelea katika magereza, kutembea shuleni, kutembea katika vituo vya Polisi kuhakikisha wanalinda na wakati wanalinda wanaangalia, je, haki za Watanzania zinalindwa? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba Tume hii haifanyi kazi na naweza kusema kwamba haifanyi kazi kabisa kwa sababu hatuisikii. Nayasema hayo kwamba ni mfu, ukiangalia bajeti ya mwaka wa fedha ya maendeleo ya mwaka 2021/2022, bajeti ya maendeleo ilitengwa Sh.373,000,000 tu na fedha hizi hazitokani na mapato ya ndani, ni fedha ambazo zinatoka kwa *donors*. Sasa inasikitisha kwamba haki za watu wetu zinalindwa na watu wa kutoka nje, yaani Serikali haioni kama ina wajibu wa kutenga bajeti tena bajeti ya kutosha kuhakikisha Tume hii sasa inakwenda kufanya kazi yake kwa uaminifu, kwa uadilifu, lakini pasipokuwa na kikwazo cha bajeti. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi natokea Mkoa wa Dar es Salaam, Mkoa wa Dar es Salaam tukihesabu kuna shule ngapi, tukihesabu kuna vituo vya Polisi vingapi, tukayahesabu na magereza ukiangalia hii bajeti ya Sh.373,000,000 haiwezi kutosha hata kwa mkoa mmoja! Kama kweli Tume inafanya kazi fedha hizi sio tu kwamba hazitoshi nchi nzima hata mkoa mmoja hazitoshi. Hata hivyo, kuonesha kwamba Tume hii ni mfu mwaka huu wa bajeti imetengwa Sh.260,000,000 tu na hizi fedha ni kutoka nje, hakuna mpango mkakati wa Serikali kuona umuhimu wa kulinda haki za watu wake au wananchi wake ni mpaka tusaidiwe na *donors* kutoka nje. (Makofi)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, sasa najiuliza inawezekana kweli umezaa mtoto, mtoto wako unampenda sana, unalala naye nyumba moja mlango haufungi, unategemea jirani aje kumfungia mlango mtoto wako na bado unaamini mtoto wako yupo salama, ni jambo ambalo haliwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea kuonesha namna gani ambavyo Tume hii ya Haki za Binadamu ni mfu na huwa inafufuka wakati wa bajeti kama hii, tunafahamu, tunatambua kwamba yamekuwepo matukio mbalimbali ya watu kutekwa, watu kuuawa na wengine mpaka leo hawajawahi kuonekana, mfano wa Azory Gwanda, Mfano Benny Saa Nane, alitekwa mpaka leo hajaonekana, hatukuwahi kusikia Tume hii ikisimama kutekeleza wajibu wake wa kukemea, wa kulaani na hata kushtaki angalau taasisi au watu wanaosadikiwa kwamba walishiriki katika uvunjaji wa haki za binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sio tu hilo lakini wapo Watanzania wenzetu ambao walitekwa lakini wakapatikana, yaani mtu anatekwa halafu anarudi, ana uwezo wa kuelezea wapi alikuwepo nani alimkamata, kilikwenda kilirudi, watu hao wakaonekana, mfano Mo Dewji, lakini tunaye mwingine Roma Mkatoliki, walitekwa wakarudi wakapatikana, Tume hii haijawahi kusikika inalaani, haijawahi kusikika angalau inatoa tamko au basi angalau kufuatilia hata kwenda kufungua kesi, kwa sababu ni wajibu wa Tume hii inapobidi kufungua kesi *against* taasisi au mtu ambaye inasemekana amefanya uvunjifu wa haki za binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine kuonesha kwamba hii ni Tume mfu, hivi karibuni yametokea matukio makubwa katika Mkoa wa Mtwara na Mkoa wa Tanga, Jeshi la Polisi linatuhumiwa kuua Watanzania. Ni kiongozi wa nchi Mheshimiwa Rais Mama yetu Samia Suluhu Hassan ambaye alisimama juu ya mlima akapiga kelele, kwanza akalaani, akakemea na akatoa maelekezo nini kifanyike kwa ajili ya uvunjwaji wa haki za binadamu, lakini Tume hii ambayo leo hii ipo hapa inahitaji tupitisha bajeti iko kimya imekufa...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana, muda wako umekwisha.

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Spika, naomba ni *wind up* kidogo.

SPIKA: Ahsante sana.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana Waziri wa Katiba na Sheria Dkt. Damas Ndumbo na Naibu wake Mheshimiwa Godfrey Pinda na wataalamu wa Wizara kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Spika, mimi nitachangia kuhusu uwepo wa sheria iliyo kwenye *GN. 269* ya Aprili, 2020. Sheria ilitoa kipindi cha mpito cha miaka miwili kuitekeleza na sasa iko kwenye hatua za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, sheria hii inayokataza uwepo wa maduka ya dawa mita 500 kuzunguka Hospitali za Serikali kwa hisia kwamba baadhi ya wataalamu wa Wizara ya Afya wanaijumu Serikali kwa kuiba dawa na kuziua maduka ya karibu au kuwa na maduka karibu na hospitali za Serikali na huishia kuyakuza maduka yao.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Waziri wa Afya Mheshimiwa Umy Mwalimu alitoa agizo la kuondolewa kwa maduka yote ya dawa ambayo yapo mita 500 ndani ya eneo la hospitali za Serikali kwa kile kinachodaiwa kuhujumu upatikanaji wa dawa katika hospitali hizo. Tangazo hili lilisababisha taharuki kubwa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa mawazo yangu, sheria hii ilipotungwa haikuzingatia maslahi ya wagonjwa wa Kitanzania na wamiliki wa maduka binafsi ya dawa yaliyo karibu na hospitali. Maduka haya yapo kusaidia upatikanaji

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wa dawa kwani Serikali yenyewe bado haina uwezo wa kusambaza dawa zote na vifaa tiba kwa wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, hii sheria ina mapungufu makubwa sana. Mimi naona hakuna mwananchi anayependa kwenda nje ya hospitali kutafuta dawa au vifaa tiba bali changamoto za uhaba wa madawa na vifaa tiba zilizopo ndani ya hizo hospitali ndio zinafanya waende nje.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya kuanzisha sheria hii yanakinzana kabisa na uhalisia uliopo. Tatizo kubwa lililopo Wizara ya Afya ni katika mfumo mzima wa ugavi, usambazaji na usimamizi wa dawa, na si uwepo wa maduka ya watu binafsi ya dawa karibu na hospitali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, watumishi wasio waaminifu wakiiba na kutoa dawa nje ya hospitali, dawa inaweza kwenda popote nje ya hospitali na hata mikoa ya mbali kwa haraka kwa kutumia mbinu mbalimbali zikiwemo bodaboda.

Mheshimiwa Spika, ninachokiona, si kweli kwamba maduka yaliyo karibu na hospitali ndio wateja wa wizi wa dawa kutoka hospitali za Serikali. Kutokana na ukweli huu napendekeza kwa Waziri wa Katiba na Sheria kwa kushauriana na Waziri wa Afya sheria hii ifutwe kwani kwa kufanya hivyo tutawapunguzia wananchi adha ya kutafuta dawa na vifaa tiba wanazoandikiwa kwenda kununua nje ya hospitali za Serikali; Wizara ya ya Katiba na Sheria itambue kwamba Wizara ya Afya ilitoa vibali mbalimbali vya kuanzisha maduka ya dawa. Kufunga biashara zao kutasababisha hasara kubwa kwa hawa wawekezaji wazalendo na kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na kodi wanazolipa; maduka ya watu binafsi ya dawa hasa yale yaliyo karibu na hospitali husaidia upatikanaji wa dawa kirahisi kwani Serikali yetu yenyewe bado haina uwezo wa kutoa dawa zote na vifaa tiba ana kufuta hii sheria kutaonesha hawajali wafanyabiashara na wawekezaji wa biashara ya dawa na vifaa tiba hapa nchini.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nampongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli naipongeza sana Seikali kwa kujenga Mahakama ya Temeke. Nilikuwa Mbunge wa vipindi vilivyopita nilikuwa nataka ikamilike sana kuhusu Mahakama ya Temeke, sasa tumepata Mahakama Maalum yenye kila kitu mpaka chumba cha kunyonyeshea Watoto, hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo Mahakama za Wilaya zote za Mkoa Dar es Salaam zimejengwa na ziko vizuri sana. Ombi langu naomba Serikali iangalie Mahakama ya Mwanzo Mbagala; hali ni mbaya Mbagala. Idadi ya watu Mbagala ni kubwa na mahitaji ni makubwa sana. Naomba Serikali iangalie sana Mbagala.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono na tumekuwa na *mobile* mahakama maeneo ya Chanika na zile za pembezoni, shukrani sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii muhimu kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kujaalia neema na baraka Watanzania. Aidha naungana na Watanzania kuipongeza sana Serikali yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wetu mpendwa kwa jinsi inavyotekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025 na kutatua kero ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nitoe mchango wangu kupitia hotuba ya Wizara na Kamati ya Katiba na Sheria; kwanza Serikali iangalie matumizi sahihi ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

maadhimisho ya siku ya sheria kwa ajili ya kupata picha ya upande wa wapokea huduma ili kutathmini kwani kwa sasa jamii na wapokea huduma hawajafahamu kikamilifu maudhui ya maadhimisho hayo, hivyo basi kutafutwe muundo mzuri wa siku hiyo kuwa na tija nzuri zaidi ili kuleta ufanisi wa utendaji kazi na jamii kuwa na imani kwa mahakama kama mhimili wa kutoa haki kwa wapokea huduma za jamii na matumizi sahihi ya *media*, redio na mitandao ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu itoe fedha za kujenga na kukarabati mahakama zote kongwe zilizojengwa toka enzi za kikoloni kwani kwa sasa hazifai kwa matumizi, mfano huo ni Mahakama ya Wilaya ya Mbulu, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri atembelee na maeneo mengine nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali ijitahidi kutoa fedha zinazoombwa kwenye bajeti kwani hadi mwezi Februari, 2022 ni kiasi cha asilimia 29.87 kilichotolewa ya maombi ya matumizi, kiasi hiki ni kidogo sana kulingana na malengo yaliyotarajiwa katika kutekeleza majukumu yake muhimu na katika maombi ya miradi ya maendeleo hadi Februari, 2022 ni asilimia 45.37; hali hii itaathiri mpango wa bajeti ya maendeleo ya mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, Serikali iandae kalenda ya vikao vya Kamati ya Maadili za Wilaya na Mkoa na kuwepo kwa wajumbe kutoka upande wa wapokea huduma ili kupata taswira ya upande huu. Aidha, ni muhimu sana kuangalia hadidu za ajenda Kamati ya Maadili za Mahakama.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa uchangiaji, sasa tunaingia upande wa Serikali. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, mtoa hoja ajiandae.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuendelea kuhudumu kwa nafasi ambazo amependa tuendeleo kuwemo humu kuwahudumia Watanzania. Nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mahsusi kwa leo kwa jinsi ambavyo anasimamia utawala wa sheria na utawala bora. Pia nikushukuru sana wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti na uongozi wote wa Bunge kwa kuhakikisha kwamba Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linatimiza wajibu wake kwa Katiba na kwa mujibu wa kanuni ambazo zipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Naibu Waziri, Mawaziri wengine waliopo hapa pamoja na watendaji wote Serikalini. Nimshukuru Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania na viongozi wote ambao kwa upande wa Serikali wanahakikisha kwamba haki inatendeka kwa mujibu wa Katiba. Aidha, niishukuru Kamati ya Katiba na Sheria ya Bunge pamoja na Kamati ya Bajeti ambazo nimekuwa nikifanya nazo kazi kwa jinsi ambavyo zimekuwa zikichakata mambo mbalimbali na kuhakikisha kwamba Bunge lako pamoja na Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, Ofisi yangu na wengine, zinatekeleza wajibu wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sitatenda haki nisipoishukuru sana Ofisi yangu kwa kuanza na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Watumishi wote kwa jinsi ambavyo wao kama sehemu ya Wizara ambayo inaratibu mashauri yote kwa mujibu wa *instrument* ya Wizara wanasaidia kuhakikisha kwamba shughuli hizi zinaendelea na kwa shukrani niwashukuru sana Wabunge wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, utakumbuka nilitoa dakika 15 za mwanzo kabla ya Bunge kuanza na dakika 15 baada ya Bunge kuahirishwa, kuingia Bungeni kusikiliza Wabunge walio na kero zao ambao huenda wanahitaji kuongea na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama mwakilishi wa Ofisi kuu ya Utumishi wa Umma upande wa Sheria. Niwashukuru wengi wamekuwa wakiniona na nimeendelea kutimiza wajibu wangu kwa kufanya nao kazi kwa karibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hoja na michango iliyowasilishwa katika Bunge hili na Wabunge wachangiaji ambao wote tunawashukuru sana, labda kiasi nichangie hili, kuna hoja imetolewa na Mheshimiwa Luhaga Mpina kuhusiana na usiri wa mikataba.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mpina ameeleza kwamba ana maelezo mengi zaidi ya yale ambayo ameyasema hapa na nashawishika na kumwomba hata Waziri wangu wa Katiba na Sheria, yawezekana tunahitaji kukaa naye na kujifunza mambo mengi sana ambayo huenda hayapati fursa ya kushughulikiwa kwenye michakato ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapoongelea masuala ya mikataba, mikataba yote inayofuata sheria inaongozwa na sheria na kwa ushiriki wa Bunge hili Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, wote mnajua kabisa kwamba Bunge hili kwa Mujibu wa Ibara 63(2) na (3) ninao wajibu mahsusi kwa mambo yanayohusu mikataba. Wajibu wa kwanza ni ule wa mikataba ambayo inatakiwa kuridhiwa na Bunge hili ambayo ni kwa mujibu wa Ibara 63(3)(e). Sijaona kama kuna lalamiko kwamba kuna mikataba ya kuletwa hapa haijaletwa. Kwa hiyo mchango wangu ni kwamba Ofisi yangu itaendelea kuhakikisha kwa wajibu wake kwamba Mikataba ya kuletwa kuwasilishwa Bungeni hapa kuridhiwa na Bunge hili itaridhiwa na Bunge kwa kufuata matakwa ya Katiba na Sheria zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa wajibu wa Bunge kusimamia Serikali niamini kwamba Kamati za Bunge hili Tukufu ambazo zipo zinasimamia Wizara na kila Sekta ya Serikali na zinao wajibu kutembelea maeneo miradi iliko ambapo naamini kazi zinazoendelea kule ni pamoja na kufuata matakwa ya mikataba iliko. Kwa hiyo niamini kwamba Bunge hili na Kamati zake vile vile itaendelea kuhakikisha kwamba zile Kamati zinapewa fursa ya kuwianisha miradi iliyopo na mikataba inayohusika na naelewa katika mwaka wa kazi kuna kikao mahsusi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ambacho kama sikosei ni kikao cha mwezi wa Tisa ambapo Serikali huwa inakuja na shughuli za Serikali Bungeni, lakini kikao kinachofuata ambacho ni cha mwezi wa Kumi na Moja ni Kamati za Bunge kuja kufanya mawasilisho ya shughuli ambazo zimeangalia utendaji wa kazi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hilo naamini kwamba kama zile Kamati za Bunge zinazosimamia maeneo ya utendaji wa Serikali kuliko na mikataba hiyo zimenyimwa fursa ya kujua mikataba hiyo ina nini, ukiachilia ile ya kuleta hapa Bungeni, basi tupo tayari kama Serikali kupokea hoja kama kuna ukiukwaji huo kuushughulikia, lakini kwa mapendekezo ya Mikataba, ni wajibu wetu kuendelea kujenga uwezo kama Serikali kuhakikisha kwamba tunao uwezo wa kufanya majadiliano na kama mnavyofahamu ile Kamati ya Serikali inayoshughulika na mradi wa *LNG* jana ilikuwa kwenye ziara mojawapo. Serikali haipo tupu sana kwa maana ya wataalam, lakini wajibu wetu ni kuendelea kuhakikisha kwamba Serikali yetu inao uwezo wa kutosha kuhakikisha kwamba kadri kunapokuwa na uwekezaji mkubwa basi wataalam wetu wote kutoka sekta mbalimbali wanahusishwa pamoja na kushughulika kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, lakini faraja yangu mara nyingi wanapenda kudadisi, Bungeni humu kuna Wanasheria zaidi ya 30 na hawa wote nimeshawakaribisha kuwa sehemu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mambo yote ambayo wataona wanahitaji maboresho, wote tunaijua tasnia ya sheria sio maneno matupu. Tasnia ya sheria inaongozwa na uhalisia na baadaye uhalisia kutokana na mambo yanayoibuka, basi wote tunakuwa na ile *collective responsibility* hata kuona maeneo yapi ambayo yanahitaji kuboresha sheria zetu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa muda ulionipatia na naunga mkono hoja ya Waziri wa Katiba na Sheria. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, nami nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kupata uhai na leo hii kupata nafasi ya kuwasilisha bajeti ya Wizara kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali yaliyopangwa katika mwaka wa fedha ujao. Nitakuwa na eneo dogo la kuzungumzia, ni maboresho mbalimbali ambayo tunaendelea kuyafanya kama Wizara kwenye maeneo mbalimbali hasa ujenzi wa miundombinu kama Mahakama, kuimarisha ofisi za watendaji wetu kama ofisi ya *DPP* na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kimsingi kwanza niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge kwa sababu kwanza wametoa kama *appreciation* kwa Wizara katika kutekeleza wajibu wake na wamekiri kabisa kwamba wanaona kazi zinazofanywa na Wizara yetu. Nawashukuru sana sana kwa eneo hili na kadri uwezo wa kifedha utakavyoendelea tutaendelea kujenga uwezo mkubwa zaidi wa kuboresha miundombinu ambayo kimsingi maboresho yoyote ya miundombinu yanasababisha utoaji wa haki usiokuwa na mashaka.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mahakama, tunao mkakati wa mpaka ifikapo mwaka 2025 kwa nchi nzima, tutakuwa tumeweka miundombinu mizuri sana. Mahakama zile ambazo ni mahakama jumuishi ambazo zipo kwenye *level* kuanzia Mahakama ya Mwanzo mpaka Mahakama ya Rufaa kwa sasa zipo sita, lakini mpango ujao tunategemea kuweka karibu mahakama tisa nyingine zenye sura ile.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika ngazi za Wilaya hadi kufikia mwaka 2025, tunategemea Wilaya zote nchini zitakuwa na majengo mapya kwa zile wilaya ambazo hazina majengo kabisa tutakuwa tumekamilisha kabisa uwekaji wa miundombinu ya mahakama.

Kwa upande wa Mahakama zile za Mwanzo mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba mpaka ifikapo mwaka

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

2025, Makao Makuu yote ya Tarafa kwa nchi nzima, tutakwenda kuweka mahakama mahali ambapo huduma hii haijafika. Kwa hiyo haya ni makubwa ambayo tunakwenda nayo.

Mheshimiwa Spika, vile vile upande wa *DPP* kweli kuna uhaba mkubwa kama Waheshimiwa Wabunge walivyoliona na kwa kadri fedha zitakapopatikana tunataka kukimbiza ujenzi wa ofisi kwa sababu ofisi hii itakapoi marika, ni uhakika wa kutosha kwamba na Mahakama ule ufanisi utaonekana kwa uwazi mkubwa zaidi kuliko ilivyo sasa, kwa sababu Mahakama haiwezi kukamilisha shughuli bila ushirikiano na *DPP* na vyombo vingine.

Mheshimiwa Spika, vile vile upande wa Wakili Mkuu wa Serikali naye kumuimarishia ofisi ili aweze kutekeleza wajibu wake ipasavyo. Kwa hiyo jambo la kuimarisha miundombinu ni jambo muhimu sana na sisi tunapokea mawazo ya Waheshimiwa Wabunge wote na maboresho yataendelea kulingana na jinsi ambavyo tunaendelea kupata fedha au vitendea kazi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, lipo eneo lingine ambalo limeguswa na Waheshimiwa Wabunge hapa ni marekebisho ya sheria mbalimbali. Kuna Mheshimiwa ameeleza kwamba tupitie sheria mbalimbali hasa za vyama hivi kuangalia jinsi ambavyo wanaweka usawa wa kijinsia haya yote tunayapokea kwa sababu ni lazima yachakatwe.

Mheshimiwa Spika, ni wito tu kwa vyama na vyenyewe kwa sababu sheria yenyewe imetoa uhuru mkubwa sana, ni utekelezaji tu na usimamizi wa vyama vyenyewe binafsi kwenye utekelezaji wao, kwa sababu ukiangalia Chama cha Mapinduzi hakina uhaba wa akinamama katika ngazi mbalimbali za uongozi. Kwa hiyo unaweza ukaona labda ni mapungufu tu katika baadhi ya vyama ambavyo vinatakiwa vifungue milango kwa akinamama kupata ile haki sawa, hakuna mahali ambapo sheria imewanyima haki ya kugawana madaraka katika maeneo yao.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, hivyo niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na tumepokea maelekezo yao na tutakwenda kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Haya, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, aje ahitimishe hoja yake.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kwa mara nyingine kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi ambavyo anatuongoza hususan katika Wizara hii ya Katiba na Sheria. Namshukuru Makamu wa Rais na Waziri Mkuu kwa kazi nzuri ambayo wanawafanyia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee nikushukuru tena wewe kwa namna ambavyo unaliendesha Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, tumepokea maoni ya kamati mbili; Kamati ya Katiba na Sheria pia Kamati ya Bajeti ikieleza mambo mengi mbalimbali ambayo Wizara tunapaswa kuyatilia maanani ili kuhakikisha kwamba haki siyo tu inatendeka lakini pia inaonekana ikitendeka.

Mheshimiwa Spika, kwa moyo wa dhati kabisa nazishukuru Kamati zote mbili na hasa Wenyeviti wake; Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama na Mheshimiwa Sillo, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, kwa maoni yao. Nawaahidi kwamba tumeyapokea na tutakwenda kuyatekeleza.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia wanakamati wote wa Kamati zote hizo mbili na Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa michango yao kwa Wizara ya Katiba na Sheria siku hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja chache zilizotolewa. Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria imejipanga kumfanya kila Mtanzania aweze kuzielewa sheria, aweze kuzitekeleza na kuzitii ili lile suala la kutokujua sheria isiwe utetezi, liweze kuondoka kabisa. Kwa kufanya hivyo, tumejikita katika kutafsiri sheria kutoka kwenye lugha za Kiingereza kwenda kwenye lugha ya Kiswahili. Mpaka hivi sasa katika sheria 466 tulizonazo katika nchi hii, sheria 212 zimeshatafsiriwa. Kila sheria mpya ambayo inatungwa, itakuja kwa lugha ya Kiswahili ili mwananchi aliyeko Kijijini, aliyeko kule Songea na Mbeya, aweze kuzifahamu sheria hizi, kuzitii na kuzitekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maboresho ya Mahakama yameongelewa vizuri sana Mheshimiwa Naibu Waziri, niongeze jambo la muhimu. Pamoja na miundombinu ambayo imewekwa na inaendelea kuwekwa, Mahakama imeleta mfumo wa kuwasiliana na mwananchi wa kawaida, kupitia namba ya simu ambayo ni huduma ya bure, kila mwananchi anaweza akapiga na kutuma meseji bure. Tumeitaja namba hiyo ni 0752 500 400; na mpango huo umepewa jina unaitwa "Sema na Mahakama," kwa saa 24 ndani ya siku saba katika wiki.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa mtu yoyote anaweza akatumia mfumo huo kutoa kero zake, kutoa hoja zake, hata pale ambapo anahisi kwamba kuna kesi imeendeshwa kinyume cha maadili, kuna viashilia vya rushwa, basi atumie mfumo huo. Tahadhari tu ni kwamba mfumo huo siyo rufani; mfumo huo ni kuelezea kero za kiutawala zilizopo, na wala hutaweza kutangua maamuzi yaliyotolewa kihalali kabisa.

Mheshimiwa Spika, pia kumetolewa hoja na Waheshimiwa Wabunge kuelezea mfumo wa jinai na kwa jinsi gani umekuwa ukichelewesha mashauri za kesi za jinai. Niwaeleze Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote, sasa hivi tuna mkakati wa kuuchukua mfumo mzima wa jinai na kuingiza maabara ili kuweza kujua changamoto hasa ni nini? Baada ya hapo, tuufanyie mabadiliko makubwa sana

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mfumo wote wa jinai. Tukifanya hivyo tutaondoa kero za kucheleweshwa kesi.

Mheshimiwa Spika, katika hilo, tunaangalia maeneo matatu; eneo la kwanza, tunaangalia Ofisi ya Mwendesha Mashitaka Mkuu wa Serikali, wengi hupenda kumwita *DPP*. Ili tuweze kufanya kazi vizuri, mmesema hapa Waheshimiwa wabunge, lazima tuitendee haki ofisi hiyo. Lazima tupe vitendea kazi na mambo mengine ili kesi ziweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, pia tunaangalia Mahakama na Mfumo wa Jinai, wapi kuna vikwazo? Tunaenda kuangalia pia Magereza na mfumo wa jinai tunaamini tukifanya hivi ndani ya mwaka huu wa fedha na kuendelea tutakuwa tumetatua matazo makubwa yanayoikabili mfumo wa jinai.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Neema Lugangira amesimama na kutoa hoja ambazo zinagusa sheria mbili; moja ni sheria ya vyama vya siasa; na ya pili ni sheria ya uchaguzi. Mahususi ameongelea kwa jinsi gani sheria hizi hazimtendei haki mwanamke katika uwanja huu wa siasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Neema tumepokea maoni yako kwa uzito mkubwa kabisa. Naomba nichukue fursa hii kuiagiza Tume ya Kurekebisha Sheria kuanzia kesho waanze kuzifanyia kazi sheria hizi mbili; na wawashirikishe wadau wote wakiwemo Waheshimiwa Wabunge wanawake, Waheshimiwa wanasiasa wanawake na wadau wengine ili kujua wapi panawakwaza na tuweze kubadilisha sheria hizi.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Chama cha Mapinduzi kinasema, sheria hizi zinapaswa kuwatumikia watu, na sio watu kuzitumikia sheria hizi. Ni muda sasa wa kuzirekebisha ili kuweza kutenda haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Agneta ameongelea sana kuhusiana na Tume ya Haki za Binadamu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Tunapokea maoni yake na tuko tayari kuboresha tume hizo. Niseme tu kitu kimoja, katika bajeti ya mwaka huu, Tume za Haki za Binadamu - Fungu la 55, fedha ambayo inapendekezwa endapo Bunge hili Tukufu litapitisha ni shilingi bilioni 6.5. Hiyo ndiyo fedha ambayo tunapendekeza. Kwa hiyo, Mheshimiwa Agnesta, hebu tupitishie hii ili Tume iweze kupata fedha hiyo. Katika fedha hiyo, fedha za nje ni shilingi milioni 155 tu. Kwa hiyo, tunataka kwenda kubadilisha utendaji wa Tume ili Fungu hili la 55 likaibadilishe Tume, Tume itende haki, pia Tume iwafikie wananchi na kutatua kero zote zinazowagusa.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena nakushukuru wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Tunaendelea na utaratibu wetu, Katibu.

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

KITABU CHA PILI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources*

Management Division.....Sh.

7,479,959,000

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki kina mshahara wa Waziri na naona kuna Mbunge hapa anataka kupata ufafanuzi. Mheshimiwa Neema Mwandabila.

MHE. NEEMA G. MWANDABILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Tumeona katika maelezo ya Waziri, ametueleza kabisa kwamba kuna kesi ambazo zinachukua muda mrefu na baadaye zinaisha. Unakuta katika kwisha huenda zinaondolewa bila kupatiwa maelezo ya kina, lakini pia ziko zinazoisha kwa mtuhumiwa kukosa hatia; na wakati mwingine unakuta kesi hizi zinawagusa Watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba, inapokuwa kesi inaondolewa, au mtu anashinda hiyo kesi: Ni nini utaratibu ambao Wizara imeweka ya kumfidia huyu mtu kutokana na madhara anayokuwa ameyapata kwa kipindi hicho ambacho anakuwa aliwekwa rumande au wakati anafuatilia hiyo kesi? Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, ufafanuzi.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Namshukuru Mheshimiwa Neema kwa kuuliza swali hilo ambalo lina maslahi mapana kwa Watanzania wengi ambao yeye anawawakilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wetu wa jinai uko bayana kabisa kwamba endapo mtu anashitakiwa na baadaye akashinda hiyo kesi, lakini akaona kuna viashiria na chembe chembe za uonevu, anaweza akafungua kesi ya madai kudai fidia kwa kadhia ambayo amefanyiwa kinyume cha sheria. Mahakama zetu zipo, wapo watu ambao wamefanya hivyo na wametendewa haki. Kwa sababu huo ndiyo mfumo wa sheria waliyojiwekea.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, endapo mtu ameshitakiwa kwenye kesi ya jinai au kesi nyingine, ameona kwamba amemaliza kesi yake lakini hakukuwa na ukweli, anaweza akafungua kudai madai. Hiyo inaitwa *malicious prosecution* kwamba alishitakiwa pasipokuwa na sababu ya msingi ya kushitakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Neema nikuhakikishie kwamba mfumo upo, unatenda haki hiyo na Mtanzania yeyote anaweza akaipata haki yake.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

| | |
|--|-------------------|
| Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts Unit</i> | Sh.470,107,000 |
| Kifungu 1003 - <i>Policy and Planning Division</i> | Sh. 1,043,925,000 |
| Kifungu 1004 - <i>Internal Audit Unit</i> | Sh. 368,329,000 |
| Kifungu 1005 - <i>Government Communication Unit</i> | Sh. 188,715,000 |
| Kifungu 1006 - <i>Procurement Management</i> | Sh. 292,071,000 |
| Kifungu 1007 - <i>Information and Communication Technology Unit</i> | Sh. 384,285,000 |
| Kifungu 2001 - <i>Human Rights Division</i> | Sh. 886,085,000 |
| Kifungu 2002 - <i>Legal and Services Unit</i> | Sh. 713,461,000 |
| Kifungu 2004 - <i>Public Legal Services Division</i> ... | Sh. 1,049,316,000 |
| Kifungu 2005 - <i>Natural Wealth and Resource Abservatory unit</i> | Sh. 608,127,000 |
| Kifungu 4001 - <i>Constitutional and Justice Monitoring Division</i> | Sh. 1,028,418,000 |

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama

| | |
|---|-----------------|
| Kifungu 1001 – <i>Administration and Human Resources Management.....</i> | Sh. |
| 1,434,190,000 | |
| Kifungu 1002 – <i>Finance and Account Unit.....</i> | Sh. 89,440,000 |
| Kifungu 1003 – <i>Procurement Management Unit...Sh.</i> | 59,105,000 |
| Kifungu 1004 – <i>Internal Audit Unit.....</i> | Sh. 48,865,000 |
| Kifungu 1005 – <i>Recruitment, Appointment and Confirmation Unit.....</i> | Sh. |
| 492,010,000 | |
| Kifungu 1006 – <i>Ethics and Discipline Section.....</i> | Sh. 741,580,000 |
| Kifungu 1007 – <i>Planning, Monitoring and Evaluation Unit.....</i> | Sh. |
| 59,580,000 | |
| Kifungu 1008 – <i>Information and Communication Technology Unit.....</i> | Sh. |
| 213,758,000 | |
| Kifungu 1009 – <i>Legal Service Unit.....</i> | Sh. 22,600,000 |

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

| | |
|--|-----------------|
| Kifungu 1001 – <i>Administration and Human Resources Management.....</i> | Sh. |
| 2,847,348,000 | |
| Kifungu 1002 – <i>Finance and Account Unit.....</i> | Sh. 428,200,000 |
| Kifungu 1003 – <i>Planning Division.....</i> | Sh. 588,560,000 |
| Kifungu 1004 – <i>Internal Audit Unit.....</i> | Sh. 185,610,000 |
| Kifungu 1005 – <i>Government Communication Unit</i> | Sh. |
| 166,490,000 | |
| Kifungu 1007 – <i>Procurement Management.....</i> | Sh. 229,172,000 |

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kifungu 1008 – *Research and Library Service*
Unit.....Sh.

90,860,000

Kifungu 1009 – *Information and Communication*
Technilogy Unit..... Sh.

312,220,000

Kifungu 2001 – *Coordination and Advisory*
Services..... Sh.

1,458,072,000

Kifungu 2003 – *Legislative Drafting*..... Sh. 1,758,845,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3002 – *Treaties and Contracts*
Division.....Sh.

1,079,396,000

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kwagilwa Reuben.

MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kama nilivyokuwa nimetangulia kusema kwenye mchango wangu, ukijaribu kuangalia kwenye kifungu hiki cha 3002, sehemu ya mafunzo imetengewa fedha kidogo sana, shilingi 31,730,000 .

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama haipo namna nyingine ya kuweza kuweka fedha mahali hapa, naomba nipate ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri, kwa sababu eneo hili ni eneo la muhimu, hatuwezi kuacha watu wetu wasiwe *trained* halafu tuwe tunakimbilia ku-*hire* watu halafu tunalipa fedha nyingi tu, wakati fedha zinazohitajika kuwa-*train* ni kidogo sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Reuben kwa kuleta hoja hii. Nasisitizia tena sasa, kama ambavyo tumesema,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Reuben ana hoja ya msingi sana. Sisi kama Serikali tumeipokea hiyo hoja. Tunakwenda kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, tukumbuke kwamba tunapitisha Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria, ombi hilo tunalichukua lakini bajeti kuu ya Serikali bado haijapita. Tunaichukua kuweza kuongea na Waziri wa Fedha na Serikali kwa ujumla ili kutendea haki suala hili. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, katika ngazi hii ya mafungu ya aina hii, Mheshimiwa Kwagilwa ametoa taarifa hapa kwamba alitaka kusimama ili apate ufafanuzi. Huo ndiyo ufafanuzi uliotolewa na Waziri.

Hata hivyo, kikanuni, ukishaona hapa fungu la fedha lina fedha kidogo nawe unataka ziongezeke, unazitafuta kwenye mafungu haya ukitaka kuzihame kutoka wapi zielekee hapo. Ndiyo utaratibu wa kikanuni; unatakiwa useme hapa ziko shilingi milioni 31, unataka zitoke zingine wapi ziingie hapa, halafu kule kubaki au zibaki kidogo na jambo kama hilo. Ndiyoo utaratibu wa kikanuni.

Kwa hiyo, kwenye ngazi hii ukisema fedha ziko kidogo, unapaswa wewe utoe maelezo fedha zitoke kwenye fungu gani ili ziingie fungu lingine. Sasa haya maelezo aliyoyatoa hapa Mheshimiwa Waziri, ni kweli wanaweza kwenda kuzungumza huko, lakini sina hakika kama italeti matokeo kwa kadri ya utaratibu wetu wa namna ya kuweka haya mafungu; lakini wacha tsubiri madamu Waziri amelisema hapa.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 5001 – *Regional Attorney General's Office – Dar es Salaam*..... Sh. 165,080,000
Kifungu 5002 – *Regional Attorney General's Office – Arusha*..... Sh. 75,100,000

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

| | |
|---|----------------|
| Kifungu 5003 – <i>Regional Attorney General's</i> <i>Office – Mbeya.....</i> | Sh. |
| 70,080,000 | |
| Kifungu 5004 – <i>Regional Attorney General's</i> <i>Office – Kilimanjaro.....</i> | Sh. 64,584,000 |
| Kifungu 5005 – <i>Regional Attorney General's</i> <i>Office – Mtwara.....</i> | Sh. |
| 74,080,000 | |
| Kifungu 5006 – <i>Regional Attorney General's</i> <i>Office – Mwanza.....</i> | Sh. 67,584,000 |
| Kifungu 5007 – <i>Regional Attorney General's</i> <i>Office – Kagera.....</i> | Sh. |
| 62,900,000 | |
| Kifungu 5008 – <i>Regional Attorney General's</i> <i>Office – Tabora.....</i> | Sh. |
| 72,080,000 | |
| Kifungu 5009 – <i>Regional Attorney General's</i> <i>Office – Tanga.....</i> | Sh. |
| 75,080,000 | |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 19 – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

| | |
|--|-----------------|
| Kifungu 1001 – <i>Administration and Human</i> <i>Resources Management.....</i> | Sh. |
| 8,029,588,000 | |
| Kifungu 1002 – <i>Finance and Accounts Unit.....</i> | Sh. 136,100,000 |
| Kifungu 1003 – <i>Planning Division.....</i> | Sh. 265,581,000 |
| Kifungu 1004 – <i>Internet Audit Unit.....</i> | Sh. 80,280,000 |
| Kifungu 1005 – <i>Procurement Management</i> <i>Unit.....</i> | Sh. |
| 117,850,000 | |
| Kifungu 1006 - <i>Information and Communication</i> <i>Technology Unit.....</i> | Sh. |
| 366,581,000 | |
| Kifungu 1007 - <i>Government Communication</i> | |

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

| | | |
|---|------------------------|---------------|
| | <i>Unit</i> | |
| Sh.123,079,000 | | |
| Kifungu 1008 - <i>Library Services and Research</i> | | |
| | <i>Unit</i> | Sh. |
| 80,327,000 | | |
| Kifungu 1009 - <i>Legal Registry Unit</i> | Sh. | 204,000,000 |
| Kifungu 2001- <i>Case Mgt and Quality</i> | | |
| | <i>Assurance</i> |Sh. |
| 479,780,000 | | |
| Kifungu 2002 - <i>Arbitration Division</i> | Sh. | 1,616,710,000 |
| Kifungu 2003 - <i>Litigation Division</i> | Sh. | 1,312,940,000 |

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 35 – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

| | | |
|--|-----------------------------------|------------------------|
| Kifungu 3001 - <i>Fraud, Money, Laundering and</i> | | |
| | <i>Corruption Offences</i> |Sh. |
| 2,349,240,000 | | |
| Kifungu 3002- <i>Assets Forfeiture Transnational &</i> | | |
| | <i>Specilized Crimes</i> | Sh. 2,464,500,00 |
| Kifungu 3003 - <i>Case, Management Coordination of</i> | | |
| | <i>Criminal Cases</i> |Sh. |
| 5,059,945,00 | | |
| Kifungu 1001 - <i>Admninistration and Human</i> | | |
| | <i>Resources Management</i> |Sh. 6,258,816,00 |
| Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts Unit</i> | Sh. | 916,827,000 |
| Kifungu 1003 - <i>Planning Division</i> | Sh. | 618,114,000 |
| Kifungu 1004 - <i>Internal Audit Unit</i> | Sh. | 396,437,000 |
| Kifungu 1005 - <i>Procurement Management</i> | | |
| | <i>Unit</i> |Sh. |
| 365,475,000 | | |
| Kifungu 1006 - <i>ICT and Information</i> | Sh. | 354,328,000 |
| Kifungu 1007- <i>Government Communication</i> | | |
| | <i>Unit</i> |Sh. |
| 220,475,000 | | |
| Kifungu 1008 - <i>Research and Library Services</i> | | |
| | <i>Unit</i> |Sh. |
| 276,955,000 | | |

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

| | |
|--|-------------------|
| Kifungu 1009- <i>Legal Registry Unit</i> | Sh. 867,930,000 |
| Kifungu 2002 - <i>Civilianization and Prosecutions</i> | Sh. 2,193,335,000 |
| Kifungu 2004 - <i>Regional Office Arusha</i> | Sh. 505,000,000 |
| Kifungu 2005 - <i>Regional Office Dodoma</i> | Sh. 3,042,318,000 |
| Kifungu 2006 - <i>Regional Office Dar es Salaam</i> | Sh. 869,000,000 |
| Kifungu 2007 - <i>Regional Office Iringa</i> | Sh. 385,000,000 |
| Kifungu 2008 - <i>Regional Office Moshi</i> | Sh. 400,000,000 |
| Kifungu 2009 - <i>Regional Office Kagera</i> | Sh. 525,000,000 |
| Kifungu 2010 - <i>Regional Office Mbeya</i> | Sh. 445,000,000 |
| Kifungu 2011 - <i>Regional Office Mtwara</i> | Sh. 355,000,000 |
| Kifungu 2012 - <i>Regional Office Mwanza</i> | Sh. 515,000,000 |
| Kifungu 2013 - <i>Regional Office Ruvuma</i> | Sh. 345,000,000 |
| Kifungu 2014 - <i>Regional Office Sumbawanga</i> | Sh. 340,000,000 |
| Kifungu 2015 - <i>Regional Office Tabora</i> | Sh. 420,000,000 |
| Kifungu 2016 - <i>Regional Office Tanga</i> | Sh. 415,000,000 |
| Kifungu 2017 - <i>Regional Office Shinyanga</i> | Sh. 435,000,000 |
| Kifungu 2018 - <i>Regional Office Singida</i> | Sh. 325,000,000 |
| Kifungu 2019 - <i>Regional Office Lindi</i> | Sh. 295,000,00 |
| Kifungu 2020 - <i>Regional Office Mara</i> | Sh. 510,000,000 |
| Kifungu 2021 - <i>Regional Office Manyara</i> | Sh. 285,000,000 |
| Kifungu 2022 - <i>Regional Office Kigoma</i> | Sh. 345,000,000 |
| Kifungu 2023 - <i>Regional Office Pwani</i> | Sh. 355,000,000 |
| Kifungu 2024 - <i>Regional Office Njombe</i> | Sh. 320,000,000 |
| Kifungu 2025 - <i>Regional Office Morogoro</i> | Sh. 420,000,000 |
| Kifungu 2026 - <i>Regional Office Geita</i> | Sh. 365,000,000 |
| Kifungu 2027 - <i>Regional Office Simiyu</i> | Sh. 340,000,000 |
| Kifungu 2028 - <i>Regional Office Katavi</i> | Sh. 325,000,000 |
| Kifungu 2029 - <i>Regional Office Songwe</i> | Sh. 320,000,000 |
| Kifungu 2030 - <i>Regional Office Ilala</i> | Sh. 316,000,000 |
| Kifungu 2031 - <i>Regional Office Kinondoni</i> | Sh. 342,000,000 |
| Kifungu 2032 - <i>Regional Office Temeke</i> | Sh. 416,000,000 |

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

| | |
|---|--------------------|
| Kifungu 1001 - <i>Administration and Human Resources Management...</i> | Sh. 76,097,212,514 |
| Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts Unit.....</i> | Sh. 527,674,000 |
| Kifungu 1003 - <i>Planning and Monitoring Division.....</i> | Sh. 799,445,000 |
| Kifungu 1004 - <i>Internal Audit Unit.....</i> | Sh. 212,048,692 |
| Kifungu 1005 - <i>Information, Communcation and Technology Unit.....</i> | Sh. 1,156,640,000 |
| Kifungu 1007 - <i>Procurement Management Unit..</i> | Sh. 353,615,000 |
| Kifungu 1008 - <i>Estates Management Unit.....</i> | Sh. 408,673,750 |
| Kifungu 1009 - <i>Records Management Unit.....</i> | Sh. 355,185,000 |
| Kifungu 1010 - <i>Library Services Unit.....</i> | Sh. 173,560,900 |
| Kifungu 1011 - <i>Legal Service Unit.....</i> | Sh. 50,943,500 |
| Kifungu 2001 - <i>High Court Main Registry.....</i> | Sh. 1,561,036,900 |
| Kifungu 2002 - <i>Court of Appeal Dar es Salaam.....</i> | Sh. 2,433,300,099 |
| Kifungu 2003 - <i>High Court Zones.....</i> | Sh. 12,483,441,938 |
| Kifungu 2004 - <i>High Court Divisions.....</i> | Sh. 3,814,711,100 |
| Kifungu 2005 - <i>Resident Magistrate Courts.....</i> | Sh. 4,829,934,000 |
| Kifungu 2006 - <i>District Courts.....</i> | Sh. 7,359,954,072 |
| Kifungu 2007 - <i>Primary Courts.....</i> | Sh. 7,546,248,601 |
| Kifungu 2008 - <i>Case Management Division.....</i> | Sh. 551,305,982 |
| Kifungu 2009 - <i>Judicial Service Inspection, Supervision & Ethics</i> | Sh. 147,953,952 |
| Kifungu 2010 - <i>Judiciary Delivery Unit.....</i> | Sh. 319,940,000 |
| Kifungu 2302 - <i>Case Management Division.....</i> | Sh. 0 |
| Kifungu 2303 - <i>Complaints Mgt and Inspectorate.....</i> | Sh. 0 |
| Kifungu 2327- <i>Judiciary Delivery Unit.....</i> | Sh. 0 |

Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadilikoyoyote)

Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

| | |
|--|-------------------|
| Kifungu 1001 -Administration and Human Resources Management..... | Sh. 2,077,420,295 |
| Kifungu 1002 -Finance and Accounts Unit..... | Sh.213,112,320 |
| Kifungu 1003 -Internal Audit Unit..... | Sh. 134,233,600 |
| Kifungu 1004 -Legal Service Unit..... | Sh. 411,339,760 |
| Kifungu 1005 -Procurement Management Unit... | Sh. 137,714,000 |
| Kifungu 1006 -Management Information System Unit..... | Sh. 260,230,320 |
| Kifungu 1007 -Planning, Mon. and Evaluation Unit..... | Sh. 164,261,625 |
| Kifungu 2001 -Complaints and Investigation Division | Sh. 987,008,800 |
| Kifungu 2003 - Public Education, Comm. Research and Documentation..... | Sh. 512,590,480 |
| Kifungu 3001 - Zanzibar Office..... | Sh. 386,200,653 |
| Kifungu 3002 - Mwanza Office..... | Sh. 189,840,960 |
| Kifungu 3003 - Lindi Office..... | Sh. 126,507,280 |
| Kifungu 3004 - Pemba Branch..... | Sh. 119,019,800 |
| Kifungu 3005 - Dar es Salaam Office..... | Sh. 671,296,107 |

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria

| | |
|---|------------------|
| Kifungu 1001 - Administration & Human Resources Management..... | Sh. 1,033,761,00 |
| Kifungu 1002 - Finance and Accounts Unit..... | Sh. 346,736,000 |
| Kifungu 1003 - Planning and Coordination Unit... | Sh. 196,160,000 |
| Kifungu 1004 - Internal Audit Unit..... | Sh. 185,010,000 |
| Kifungu 1005 - Procurement Management Unit.. | Sh. 135,604,000 |

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

| | |
|---|-----------------|
| Kifungu 1006 - <i>Public Legal Awareness Unit</i> | Sh. 268,954,000 |
| Kifungu 1007 - <i>Law review Unit</i> | Sh. 502,960,000 |
| Kifungu 1008 - <i>Law Research Unit</i> | Sh. 485,144,000 |

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

KITABU CHA NNE

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

| | |
|---|-------------------|
| Kifungu 1001 – <i>Administration and Human Resources Management</i> | Sh. 4,000,000,000 |
| Kifungu 1003 - <i>Planning Division</i> | Sh. 500,000,000 |

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 35 – Ofisi ya Taifa ya Mashitaka

| | |
|--|-------------------|
| Kifungu 1001 - <i>Administration & Human Resources Management</i> | Sh. 8,000,000,000 |
| Kifungu 2002 - <i>Civilianization and Prosecutions</i> | Sh. 30,000,000 |
| Kifungu 3001 - <i>Fraud, Money Laundering & Corruption Offence</i> | Sh. 600,000,000 |

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama

| | |
|--|--------------------|
| Kifungu 1003 – <i>Planning and Monitoring Division</i> | Sh. 39,093,000,000 |
|--|--------------------|

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kifungu 1008 – *Estates Management Unit*.....Sh.
0

Kifungu 2001 – *High Court Main Registry*.....Sh.
0

Kifungu 2302 – *Case Management Division*.....Sh.
0

Kifungu 2327 - *Judiciary Delivery Unit*.....Sh.
0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*....Sh.12,726,570,00

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 55 - Tume za Haki za Binadamu na Utawala Bora

Kifungu 1007 – *Planning Monitoring and Evaluation
Unit*.....Sh.

115,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa
Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya
Matumii imemaliza kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge Lilirejea)

SPIKA: Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja taarifa.

T A A R I F A

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika,
kwa mujibu wa Kanuni 123(3)(a) na (b) ya Kanuni ya Kudumu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

za Bunge Toleo la Juni, 2020 naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi yake. Hivyo naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Sasa nitawahoji kwa mujibu wa utaratibu wetu wa kikanuni Wabunge wanaoafiki hoja ya Waziri wa Katiba na Sheria kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

*(Hoja Ilitolewa lamuliwe)
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2022/2023 – Wizara ya Katiba na Sheria Yalipitishwa na Bunge)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tumehitimisha mjadala lakini pia tumefanya maamuzi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Nichukue fursa hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, pia na watendaji ambao mnaifanya nao kazi kwa kuleta makadirio haya ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2022/2023 na Bunge kuwapitishia, kwa hiyo ninawapongeza sana kwamba Bunge limekubaliana nanyi. *(Makofi)*

Na pia nawatakiwa kila la kheri katika utekelezaji wa yale ambao mmeyaahidi kwamba mnaenda kuyafanya katika mwaka ujao wa fedha, tunawatakiwa kila kheri. Vilevile nichukue fursa hii kuwashukuru sana Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati ya Bajeti lakini pia Kamati ya Katiba na Sheria kwa kazi nzuri walioyoifanya ya kuziongoza Kamati

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hizi mbili ili ziweze kuleta mawazo yao hapa Bungeni na yatuongoze sisi wengine kutoa maoni.

Kwa hiyo tunazipongeza sana Kamati hizi mbili na viongozi wao pia; na Wabunge ambao wamepata fursa ya kuchangia pia tunawashukuru kwa maoni yenu ambayo kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri amesema wataenda kuyafanyia kazi. Kwa hiyo tunawashukuru Wabunge wote waliopata fursa ya kuchangia lakini hata Wabunge ambao hawajapata fursa ya kuchangia Mawaziri bado wako hapa kwa hiyo unaweza kuendelea kupeleka hoja zako. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilishukuru pia Bunge kwa kupitisha kwa kauli moja makadirio haya ya Mapato na Matumizi kwa wizara hii kwa sababu sote tunajua madhara ya kukataliwa kwa hiyo Bunge tunashukuru kwa hatua hii tuliyoifikia. Kwa muktadha huo Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 yamepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo hapa, ama matangazo. Tangazo la kwanza linahusu wageni; wapo wageni walikuja wageni baadaye wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria wakati wengine tukiwa tumeshawatangaza, na hawa ni wageni kutoka Chama cha Wanasheria Tanganyika *(Tanganyika Low Society)* wakiongozwa na Rais wa Chama hiki Wakili wetu Edward Hosea ambaye ni Rais wa *TLS*, ameongozana ndugu Kalebu Gamaya, yupo pia Bi. Mariam Othuman, Karibuni Sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wapo Wageni wengine ambao tuko nao leo hapa, wapo Wanafunzi 100 na Walimu 15 kutoka Shule ya Sekondari ya *Fountain Gate* ya Jijini Dodoma wakiongozwa na Mkuu wa Shule hiyo Mwalimu Karama Arafali. Karibuni sana watoto wetu. *(Makofi)*

Lakini pia tunao wanafunzi 150 wa Chuo cha Mipango kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hawa wanafunzi 100 na walimu kutoka shule ya Sekondari *Fountain Gate* hii ndiyo shule ambayo leo hapa itakuwa inatufuturisha jioni. Kwa hiyo tunawashukuru sana viongozi wa shule hii kwa kutuletea futari hapa Bungeni; ahsanteni sana, na tunaamini kwamba tutawaona pengine baadhi ya wanafunzi Wabunge watatamani kuongea nao lakini pia wanafunzi pengine watakaotaka kuongea na baadhi ya Wabunge watapata fursa hiyo. Kwa hiyo tunashukuru sana kwa sadaka hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine ni kuhusu hiyo futari kuwakumbusha kwamba tumemaliza shughuli zetu za Bunge lakini jioni leo tumeandaliwa hapa futari kwa heshima kabisa ya shule yetu hii ya *Fountain Gate* niwaombe mrejeo wakati huo wa futari. Wale ambao mnaenda kuendelea na kazi kwenye kamati nadhani itawakuta hapa hapa, wale ambao watakuwa wanaenda kwenye majukumu nje ya maeneo ya Bunge msisahau kurejea kwa ajili ya hiyo *Iftar*.

Jambo la Mwisho ni kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge hasa wale mnaopata fursa ya kuchangia lengo la kuweka Hotuba ya Waziri lakini pia lengo la kuweka mawasilisho ya Kamati zetu kwenye vishikwambi ili tuweze kuyapitia yale kwa sababu ndiyo yanayokuwa yanatuongoza kwenye michango yetu.

Na kanuni zetu hapa nimeona watu wengine wanataka kunyanyuka basi inabidi nipige macho hivi ili mtu atulie amuache Mbunge amalizie hoja yake. Lakini ukitoka nje kanuni zetu haziruhusu unatakiwa uchangie hoja iliyopo mezani; na hoja iliyopo mezani ni pamoja na wewe kutokuleta jambo jipya kabisa inalolielekeza Bunge sehemu nyingine siyo sehemu ya kufanya maamuzi; na ndiyo maana tunapitia Kamati zetu, Kamati zinapoleta hapa unazitazama zile hoja unaziwekea nguvu au unazisema kwa namna ambayo unalipelekea Bunge kufanya maamuzi fulani. Lakini usilite hoja mpya kabisa kwa sababu pia upande wa Serikali

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

inapata wakati mgumu kwa sababu haijui hiyo hoja yako wafanye nayo nini maana wanakuwa hawajatafakari halafu na wewe unawalazimisha sasa watoe majibu hapa.

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge tukumbuke kuzingatia hilo. Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 7.00 mchana Bunge Liliahirishwa hadi siku ya Ijumaa,
Tarehe 29 Aprili, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*